ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 20 Juni,2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa na afya njema na tukiwa wazima kushiriki katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa niaba yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao adhimu waliyoitoa katika siku mbili za kuchangia bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kusema kweli michango yao imegusa hisia za watu wengi na vile vile sisi serikalini tumesema kwamba michango hii ina tija. Wakati tunajibu hoja hizi niwahakikishie Wawakilishi wote kwamba tuko tayari kuhakikisha Ilani ya

Uchaguzi ya CCM katika malengo yake yote iliyojiwekea kwa wizara yetu pamoja na Dira ya 2020 na hotuba aliyoitoa Mhe Rais katika ufunguzi wa bajeti tunazitekeleza ipasavyo ili kuhakikisha kwamba Chama chetu cha Mapinduzi kinaendelea kuongoza nchi daima na daima.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa ruhusa yako nami nichukue nafasi hii kutoa majumuisho ya baadhi ya hoja zilizoulizwa na Wawakilishi kwa ufupi tu, nami naanza moja kwa moja katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Spika, masuala mengi yameulizwa kuhusiana na barabara tofauti, imeanza kuulizwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano kuhusu fedha za malipo ya fidia za barabara za *MCC* kuwa kubwa kuliko nyumba zilizopo katika maeneo hayo. Napenda kuiarifu kamati kwamba, hii inatokana na kuwa Shirika la *MCC* wakati inapolipwa fidia waliangalia zaidi viwango vya kimataifa, kwa hiyo, ndio maana ukakuta fidia ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile fidia tunayolipa sisi. Kwa sababu wao huangalia pia na athari anazozipata mtu kama ana duka lake au kama kaikodisha. Sasa kwa muda wote ule wao wanatia mahesabu yao na kupelekea kuonekana kwamba ile fidia ilikuwa kubwa na hizi pesa walitoa wao moja kwa moja, kwa sababu wao walikuwa ndio wahusika wakuu katika huu mradi. Kwa hiyo, hili suala limefanyika kwa mujibu wa taratibu zao za *MCC*.

Vile vile, waliuliza Kamati, Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu hatua zilizofikiwa katika kuondoa changamoto zilizokuwepo katika barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni.

Napenda kuwaarifu kwamba, changamoto zile tumeshazifanyia kazi na wakati wowote ile barabara mwezi wa Julai itaanza kujengwa na tunategemea sana ikifika mwezi wa Novemba itakuwa tayari imeshakamilika. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwaomba wananchi wawe na subira na serikali yao iko makini katika kuhakikisha kwamba kero zote zinazohusu wananchi zinatatuliwa hasa katika sekta hii ya barabara ambayo ni muhimu sana.

Mhe. Spika, pia, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), aliulizia kuhusu barabara yake ya Kwarara-Fuoni. Nataka kumhakikishia kwamba barabara ile ipo katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ukienda katika Ibara ya 88, utakuta barabara zote ambazo sisi kama Wizara ya Ujenzi tutazijenga katika kipindi hiki cha awamu yetu iliyopo sasa hivi katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015-2020. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, avute subira, tunajua kiu yake ya kutaka kuwaletea maendeleo wananchi wake na sisi tunazipongeza sana juhudi

zake na zimeonekana kwa ile barabara kutiwa kifusi. Kwa hivyo, tunamwambia kwamba barabara yake ile tutaijenga kwa kiwango cha lami.

Kuhusu suala lake la *route* basi tunamhakikishia kwamba tutakaa na wahusika ili kuhakikisha kwamba ile *route* inafika mpaka Madina.*(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile, Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Mohamedraza Hassanaali, waliuliza hivyo hivyo masuala ya barabara. Kwa ufupi tu nataka kumwambia Mhe. Mohamedraza kwamba, barabara yake ya Mpapa-Pagali pamoja na Dongongwe-Mchangani zile ni barabara ambazo zimejengwa kwa kifusi kwa kupitia *MIVARF* na sisi *UUB*. Na zile shilingi 20 milioni zake tulizitumia ipasavyo na yeye kama anavyojua isipokuwa kulitokea tatizo la kuharibika kifaa chetu cha ujenzi na kikakaa muda mrefu sana. Kwa hivyo, tunashukuru juhudi zake kwa kutoa shilingi 20 milioni na tumezithamini sana na kila tukipata nafasi tutaendelea kushirikiana naye katika kuhakikisha kwamba kero za wananchi hasa mambo ya barabara tunazifanyia kazi. Kwa hiyo, hizi barabara kweli zipo katika *MIVARF* nyengine na nyengine ziko katika Halmashauri, lakini tutashirikiana na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunazifanyia kazi hizi barabara ambazo wamezitaja Waheshimiwa.

Vile vile, Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Miraji Khamis Mussa, waliulizia kuhusu barabara ya Jendele-Cheju-Kaebona. Kama nilivyojibu katika swali lililopita nililoulizwa hapa Barazani kwamba ile barabara tumeshapewa sisi *UUB* na tunajitayarisha kuifanyia kazi kwa ajili ya kuitia lami katika kiwango ambacho kitakuwa cha kimataifa. Kwa hiyo, utakuta barabara zote ambazo zipo katika *UUB* sasa hivi, hii tumeipa kipaumbele cha mwanzo na karibuni tu hii barabara tutakwenda kuweka vifaa vyetu ili tuanze kazi mara moja.

Mhe. Spika, vile vile, Mhe. Hassan Khamis Hafidh, aliulizia kuhusu ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu, Amani Abeid Karume aliyoitoa kuhusu barabara ya Mtofaani, Hawai. Napenda kumhakikishia kwamba barabara ile tunaijua na vile vile, tunapenda kuwahakikishia Wawakilishi wote kuwa ahadi zote za viongozi wetu wakuu walizozitoa basi ni agizo kwetu na tutahakikisha kwamba pale ambapo tunapata fedha basi maagizo hayo yote tunayatekeleza. Hapa utakuta pia kuna barabara ya Finya-Chika ambayo Mhe. Shehe Hamad Mattar, aliulizia, kuna barabara nyengine ya Konde aliyoiulizia Mhe. Omar Seif Abeid. Kwa hiyo, zile barabara zote zilizowekewa ahadi nyengine tumeshaanza kuzitekeleza na zile ambazo bado hatujazitekeleza pale fedha zitaporuhusu basi tunaahidi Baraza lako tukufu kwamba barabara zile tutazifanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Masoud Abrahman na Mhe. Mihayo Juma N'hunga, waliulizia barabara ya Kizimbani-Kiboje itajengwa lini. Nataka kuwaarifu kwamba barabara hii tunaijua na hali yake ilivyo na *BADEA* imekuwa ndio mfadhili mkuu wa barabara ile. Kuna mambo yametokezea lakini hizo hatua ambazo zilitukwamisha katika ujenzi huu zishatatuliwa na barabara hii katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya 2015- 2020 tutaifanyia kazi kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu *Inshaallah* na wananchi wataondokana na kero ile. Kwa sababu niliitembelea ile barabara kuna mazao mengi sana na wananchi wanapata tabu, lakini tunaomba wastahamili kwani hatuna nia ya kuona wananchi wetu wanapata tabu, serikali ipo kwa ajili ya kutatua kero za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, alileta wazo zuri sana kuhusu alama za barabarani kuondolewa. Sisi hili jambo linatusikitisha sana na tunasema kwamba wale wote wanaofanya hivyo basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao pale watapopatikana wanafanya jambo hilo.

Vile vile, Mhe. Hidaya Ali Makame pamoja na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ussi Yahya Haji na Mhe. Mwinyihaji Makame, waliulizia kuhusu barabra ya Bububu hadi Mkokotoni. Napenda kuwaarifu Wajumbe kwamba ile ni katika barabara iliyopewa kipaumbele na wizara yetu na katika bajeti ya 2016/17 tutahakikisha kwamba ile barabara tunaijenga kwa lami ili kuondoa tatizo lililokuwepo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Nadir, asiwe na wasi wasi barabara ile pia imepita katika jimbo lake la Chaani na tutahakikisha kwamba katika mwaka huu wa fedha ile barabara tunaitia lami.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mtopepo aliulizia kuhusu barabara ziwekewe utaratibu wa kuzihifadhi kwa kuchukua hatua kali wale wote wanaopakia vyuma, nondo na mambo mengine. Hili ni suala linatuuma sana kama ulivyosema, pamoja na Mhe. Ali Salum Haji, aliulizia kuhusu mambo ya uwekaji wa gereji. Napenda kuwaarifu Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kama walivyoweza kulitatua tatizo la ng'ombe na tatizo hili la gereji na kuweka magari mabovu katika njia ambazo hazistahiki basi tutafanyia kazi kwa haraka, asiwe na wasiwasi baada ya kipindi kifupi tu ataona nini serikali imeamua kufanya kuondosha kero hii.

Vile vile, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, aliulizia pia suala hili la barabara ya kwenda ndani kule Mkunazini kwa nini imefungwa. Tumeifunga

barabara ile kwa sababu tunataka tuhakikishe kwamba uhifadhi wa Mji Mkongwe unaendelea kuwa mikononi mwetu kwani uko hatarini kuondosha na hii itakuwa hasara kubwa kwa taifa. Kwa hiyo, tunamuomba atustahamilie na kuna vibali maalum tumeweka kwa wale wote wanaotumia njia ile ya Mkunazini, wakiwepo watu wanaofanya ibada makanisani na wananchi wanaoishi pale, tunatoa vibali vyao maalum na yeye kama anahitaji hicho kibali basi atakwenda Hifadhi ya Mji Mkongwe atapatiwa kibali hicho, lakini hii pia imesaidia kurahisisha usalama wa watu wetu au wanafunzi wanaosoma Skuli ya *Sunny Madrassa* na Skuli ya Mkunazini na sasa hivi wanatembea bila ya wasi wasi wowote na wanafanikiwa kwenda na shughuli zao bila ya ghasia yoyote.

Mhe. Spika, vile vile, kuna suala limeulizwa na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, kuhusu ujenzi wa barabara ya Bumbwini skuli, Kiongwe, je, kuna watu ambao walikatiwa vipando vyao hadi sasa hawajalipwa mafao yao. Napenda kumuarifu kwamba, tumefanya tathmini hiyo na tulikuwa tunasubiri tupate taarifa kutoka kwa Afisa wa Kilimo ambayo mpaka sasa hivi haijaletwa taarifa hiyo katika wizara yetu. Lakini pale taarifa hiyo itapoletwa tu basi tunahakikisha kwamba tutawalipa wananchi fidia ya vipando vyao ambavyo vimeathirika wakati wa ujenzi wa barabara ile ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mhe. Rais.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Mtumwa Peya, kwa sababu barabara yake sasa hivi katika juhudi zake ya Bumbwini Makoba mpaka kwendea Kambini kule sasa hivi watu wetu wa *UUB* wako kule wanafanya kazi nzuri. Hii imetokana na jitihada zake nampongeza sana.

Mhe. Spika, pia, tuliuliziwa kuhusu suala la utumiaji wa barabara ya Bububu-Malindi kwa watu wenye ulemavu. Napenda kuwahakikishia wajumbe kwamba, wazo lao hili tumeliona na tutalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba waendao kwa miguu nao wanakuwa na nafasi zao na hasa walemavu ambao wanaathirika sana kutokana na msongamano wa magari katika barabara.

Mhe. Spika, katika masuala ya barabara Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Mussa Foum Mussa, waliulizia kuhusu barabara ya Ole-Kengeja. Napenda kuwahakikishia kwamba barabara ile tumeichukua sisi *UUB* baada ya Mfuko wa Mafuta wa Maendeleo wanaotoa mafuta kwa wingi kutoa ofa ya kuitengeneza ile barabara. Wakandarasi wengi hawakujitokeza kwa sababu wao waliona pesa zilizotolewa pale shilingi 11 milioni ni pesa chache, kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba zile pesa tunaziokoa sisi tukaamua *UUB* kwa kushirikiana na kampuni nyengine za ushauri tuhakikishe ile barabara

tumeijenga kwa sababu ni muhimu sana katika kuondosha msongamano katika barabara ya Chake-Chake na Wete.

Kwa hivyo, juhudi za *UUB* zimechukuliwa kupitia serikali na ile barabara tumeshaanza kuifanyia kazi na tunaomba sana watustahamilie, lakini tuna wataalamu wenye uzoefu na tutahakikisha ile barabara nayo inakuwa ya viwango. Kilomita 35 ni kweli nyingi, lakini tutahakikisha tunazimaliza kuzijenga kwa wakati na kama muda ulivyopangwa, ikiwa hakutatokea matatizo mengine ambayo yatakuwa hayako katika uwezo wetu basi mwaka 2017 ile barabara itakuwa tayari imeshamalizika.

Kuhusu fidia Mhe. Mussa Foum ni shahidi kuwa serikali tayari imeshatoa pesa shilingi 91 bilioni kuwalipa watu wa Ole shehia yake pale na tutaendelea kulipa pale pesa tutapozipata kutoka Wizara ya Fedha. Sisi tutahakikisha kwamba kama serikali wananchi wetu tunawalipa fidia wakati wote ambapo kutatokea kuharibiwa vipando vyao au nyumba zao kubomolewa. Kwa hiyo, napenda kumuarifu kwamba ujenzi umeshaanza na yeye ni shahidi tulikuwa pamoja na utaendelea kwa kasi kwa sababu hivi karibuni tumeingiziwa pesa kutoka Mfuko wa Uzalishaji wa Mafuta kwa wingi.

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda kumjibu Mhe. Mussa Foum, pia na Mhe. Maryam Thani Juma, kuhusu fidia za watu walioharibiwa vipando vyao vya ujenzi katika barabara ya Mtambile-Mwambe, Wete-Chake Chake na Wete-Gando watalipwa lini. Kweli fidia za nyumba tumeshalipa, lakini vipando na vile vile katika barabara za *NORAD* ambazo tunadaiwa kama shilingi 21 milioni hatujalipa, lakini tunazijua gharama zote hizo na wakati wowote pale ambapo fedha au serikali itapata fedha basi tutahakikisha kwamba waathirika wote wanalipwa fidia zao kwa mujibu wa stahiki zao walizozionesha katika barabara zile.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilali, kuhusu mashimo yaliyokuwepo katika *roundabout* ya Mwanakwerekwe na viraka Amani na hapa Mombasa, kwa nini kila siku vinatiwa viraka. Napenda kumuarifu tu kwamba barabara inakuwa na uwezo wake maalum na muda wake wa kuishi. Sasa barabara zile zinapita magari yenye uzito mkubwa sana na kuna wakati barabara zile inabidi zinapata kulainika lami yake, ndio maana unakuta zinafanya mashimo inapotokea vidimbwi kidogo kidogo.

Mhe. Spika, kila wakati linapotokea tatizo hilo kwa sababu *roundabout* ni muhimu sana, tunahakikisha ile sehemu tunaifanyia ukarabati na safari hii kama walivyoona Mwanakwerekwe na Mombasa tumefanyia ukarabati kwa

kupanua eneo zaidi ili kuhakikisha vile viraka au mashimo hayatokezei tena. Kwa hiyo, nina imani kubwa sana kwamba zile barabara zitaendelea kudumu na hayo mashimo yanayoonekana kila wakati sasa hivi yatapungua sana, kwani tumeona bora tuchukue muda mkubwa zaidi na gharama katika kutengeneza zile barabara kuliko kuziba vile viraka pekee.

Mhe. Spika, baada ya hapo Mhe. Wanu Hafidh Ameir, aliulizia kuhusu barabara ya Kisakasaka machinjioni kwamba ni mbovu. Ni kweli barabara hii tunajua ni mbovu, lakini barabara ile kama nilivyosema iko katika Halmashauri ambayo hivi sasa ni Manispaa ya Wilaya ya Magharibi 'B'. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, keshalisikia suala hili pamoja na barabara nyengine zote ambazo katika Halmashauri basi kwa kushirikiana na sisi wizara tutahakikisha kwamba tunazifanyia matengenezo pale ambapo tutahisi barabara zile hazipitiki.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, ameomba barabara ya Fuoni iendelee hadi Jumbi. Tunataka kumuarifu kwamba, barabara ile itakuwa katika awamu mbili, hivi sasa tumeanza kujenga kuanzia Mwanakwerekwe mpaka Fuoni na baadae ile barabara itafika mpaka Tunguu na itakuwa katika viwango vya kimataifa kama nilivyosema mwazo kutakuwa na pande mbili; huku na huku na vile vile kutakuwa na taa na mitaro na *culverts.*

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda pia kuchangia katika kujibu hoja za Mhe. Naibu Waziri wa Elimu, Mhe. Mussa Ali Mussa, Khamis Juma Mwalimu, Said Omar Said, Mhe. Ali Khamis Bakar, Hamad Abdalla Said na Mussa Foum Mussa, kuhusu barabara mbali mbali za ndani kwa Unguja na Pemba ambazo Wawakilishi wamezungumzia. Barabara hizi zinazohusu Kironi/Mwambani ambayo pia inajengwa na Baraza la Mji la Mkoani, barabara za Ole-Makaani,Uwandani, Chanjamjawiri ambazo ziko chini ya Baraza la Mji la Chake-Chake na barabara ya Pandani tayari barabara hii imeshajengwa kwa hatua ya kifusi na imekamilika. Lakini barabara hii ipo chini ya Baraza la Mji la Wete.

Kwa hiyo, kama nilivyosema mwazo Sheria Nam. 7 ya 2014 ya kuhusu Serikali za Mitaa tumegatua madaraka kwa wananchi na barabara zote za ndani tumezipelekwa kwa wizara inayohusika na mambo hayo ambayo ni Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ.

Mhe. Spika, kuhusu barabara ya Finya-Kicha kama nilivyosema mwanzo ipo katika ilani yetu. Tunaomba sana Wawakilishi wafungue Ibara ya 88 ya Ilani ya Uchanguzi ya Chama cha Mapinduzi watakuta barabara zote ambazo sisi kama wizara tunatakiwa tuzijenge kwa kiwango cha lami na vile vile kama

nilivyosema kuna barabara za *MIVARF* kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tutaangalia zile ambazo muhimu kwa harakati kama ile ya Mwera mpaka Fuoni tuzifanyie hatua ya mwisho ya kuitia lami. Lakini barabara zote ni nyingi sana hata ya *MIVARF*, Zanzibar pake yake hapa Unguja kuna kilomita zisizopungua 70 na pia tunawachukuwa hatua hii kuwapongeza sana *MIVARF* kwa kutusaidia katika hili na sisi tuna hakika kwamba barabara zile si chache lakini uwezo utakaporuhusu basi tutazitia lami.

Mhe. Spika, vile vile, Mhe. Moh'd Mgaza Jecha, alitaka kujua kuhusu barabara ya Mkoani/Chake inahitaji matengenezo. Na mimi nataka kumwambia kwamba serikali hajasahau barabara hii na wakati wowote tutaangalia namna gani ya kuifanyia matengenezo ya haraka na baadae matengezo ya kudumu kabisa.

Mhe. Mussa Foum Mussa, alizungumzia kuhusu barabara ya Mgagadu-Kiwani anataka ifike mpaka Pwani. Nataka kumwambia tu agizo la Mhe. Rais, tutalitekeleza na kwa hiyo, barabara hiyo tutaifikisha mpaka Pwani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaodokana na shida. Tumefanya hivyo kwa barabara ya Chwale mpaka Kojani tumeifikisha mpaka chini kule Likoni, tumefanya vile vile kwa barabara ya Raha mpaka Ukunji. Kwa hiyo, na hii vile vile tutahakikisha kwamba agizo la Mhe. Rais, tunalitekeleza ipasavyo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru wale wote waliochangia katika sekta hii ya barabara na wale waliochangia kwa maandishi na tunawahakikishia kwamba serikali yao itahakikisha hili tatizo tunalitatua pale ambapo fedha zitaruhusu.

Baada ya hapo nakuja kwenye Sekta ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati aliulizia kuhusu upungufu wa tani za mizigo kwa asilimia 2.9 kwa mwaka wa fedha 2015/16 na mamlaka imejipanga vipi kwa kukabiliana na tatizo hilo.

Napenda kumuarifu tu kwamba ni kweli hilo tatizo limetokezea na hiyo sababu ya kutokezea matatizo hayo ni kwamba Mashirika ya Ndege ambayo yanayoleta mzigo *Kenya Airways* pamoja na shirika la *Ultra Aviation* wamepunguza safari zao kutokana na sababu za kiufundi na vile vile, kuna mashirika mengine ambayo yanataka kuleta mizigo, lakini wametupa masharti mpaka tuhakikisihe kwamba tunajenga sehemu zile za kufungia mkanda za kupitisha mizigo na G*odowns* zetu za mizigo na hii tunahakikisha kwamba tumo katika harakati za kuhakikisha kwamba tunajenga hiyo miundombinu inayotakiwa ili wananchi wapate kuhakikisha kwamba serikali yao inapokea

mizigo zaidi na vile vile, kuingizia mapato serikali yao kwa ajili ya kutatua kero za wananchi.

Kwa hiyo, napenda kujumlisha kwamba mashine hizo tumeambiwa tuziweke pale, upo katika mpango wetu wa 2016/17 na tunahakikisha kwamba Mhe. Spika, mpango huo tunautelekeza kwa haraka ili kuhakikisha serikali inapata mapato mengi zaidi.

Mhe. Spika, vile vile, waliulizia kutoridhishwa kwa utumiaji wa kiwanda cha Ndege cha Pemba baada ya kumaliza mradi wa kueka taa, kwa nini ndege hazitui usiku. Napenda kumuairifu kwamba hiyari ya kutua ndege usiku ni ya mashirika yenyewe, lakini sisi tutakaa nao pamoja kuhakikisha kwamba wanapeleka ndege usiku ili kuwaondoshea mwananchi kero. Lakini vile vile napenda kulipongeza Shirika la *Precision Air* limeshaanza kupeleka ndege yake kubwa kule Pemba kutokana na juhudi zetu za hivi sasa za kuhakikisha kwamba kile kiwanja cha Pemba tunakiimarisha.

Vile vile, walizungumzia kuhusu kuvuja kwa *control tower* kule, tunataka kuwahakikishia kwamba Waheshimiwa walioulizia suala hili pamoja na kamati kwamba, hivi sasa Mhe. Spika, hali ya uvujaji haiko kabisa, tumeshaifanyia ukarabati lile jengo na mvua hata ikinyesha basi hutona hata done moja la maji.

Mhe. Spika, baada ya hapo, nakuja kwenye suala ambalo linawagusa watu wengi na limechangiwa na watu wengi sana, kuhusu *terminal II* itamalizika lini. Napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba hili tatizo kweli lipo na sisi linatuuma sana. Lakini kama unavyojua kulikuwa na hitilafu ambazo zimetokezea na hizo hitalafu zimebidi kusababisha kwamba ule mradi uchelewe. Lakini serikali kwa kupitia kiongozi wetu mahiri Dkt. Ali Moh'd Shein tutahakikisha kwamba ile *terminal II* inaendelea na ujenzi na huo mkopo ambao tumewekewa masharti basi tuko tayari kuuchua ili kuokoa jahazi. Kwani tunajua faida kubwa itakayopatikana pale ni ya kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanazidi.

Kwa hiyo, kuna mambo mengine ya kitaalamu imepanuliwa ile *terminal II*, kwa sababu mwanzo tulikisia kuchukuwa watu milioni moja na laki moja. Lakini baada ya *consultant* kutushauri tuongeze abiria zaidi ambao wanaweza kutumia lile jengo na imefikia milioni moja na laki sita, kwa hiyo, vile vile, imezidisha gharama za ujenzi na vile vile, kuna mambo mengine ya kitaalamu imebidi zile gharama ziongezeke. Lakini kwa kupitia wataalamu wetu na wahusika wengine wadau wa Uwanja wa ndege wanaotumia wakiwemo watu wa Uhamiaji na Zimamoto tumekaa nao na tutahakikisha kwamba ule mradi

kama walivyosema watu tunawashirikisha wadau kuhakikisha kwamba unamalizika kwa haraka na vile vile unaleta ufanisi na tija.

Mhe. Spika, pia, waliulizia kuhusu suala la umeme, je, tutakuwa na uwezo wa kuhudumia au kuulipia. Nataka kuwatoa shaka kwamba jengo lile kama likiwa litafanya kazi zake ipasavyo basi ni watu wengi watatumia na mapato ya serikali yataongezeka. Isipokuwa hapa mimi nitaomba Wizara ya Fedha iwaachie Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili waongezewe fungu zaidi la kuchukuwa mapato ili shughuli zao za kila siku ziendelee kufanyakazi kama kawaida. Kwa hiyo, tunajua tatizo la *terminal II* . Kwa hiyo, tunahakikisha kwamba hili tatizo tunalitatua kwa haraka ili kuhakikisha kwamba *terminal II* inamalizika kwa wakati.

Mhe. Spika, baada ya hapo waliuliza kama nilivyosema mwazo matumizi ya umeme na nimesema kwamba tutajitahidi kukusanya mapato zaidi tuhakikishe kwamba matumizi ya umeme yasiwe kizuizi kwetu katika kufanikisha ufanisi wa utekelezaji wa kazi za uwanja wa ndege. Nyote mnajua kwamba sehemu yoyote ambayo itakuwa ya kisasa hata jengo letu hili la Baraza la Wawakilishi linatumia umeme sana katika *AC* basi na lile jengo lina mambo mengi tu, kuna ngazi za umeme na mambo mengine, zote hizo Mhe. Spika, zinahitaji kutumia umeme wa gharama kubwa lakini tuko tayari kuhakikisha kwamba gharama zote hizo tunazikabili kwa kadri ya uwezo wetu.

Mhe. Mwanaasha Khami Juma, alitaka kujua wananchi wangapi wamelipwa fidia katika ujenzi ule wa Uwanja wa Ndege ambao wameathirika. Nataka kumuhakikishia kwamba wananchi waliolipwa fidia takribani wote walioleta maombi yao na iwapo kuna mwananchi yeyote anahisi kwamba bado hajalipwa fidia yake basi namuomba Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, atuletee *list* ya hao watu na sisi tuko tayari kuhakikisha kwamba watu hao tunawalipa fidia haraka ipasavyo ili wapate kuendelea na shughuli zao nyengine hasa ujenzi wa nyumba kama nyumba zenyewe zimeathirika au mashamba.

Baada ya hapo Mhe. Spika, Mhe. Machano Othman Said, alitaka tuimarishe usalama kwa kushirikiana na sekta binafsi. Tunamwambia kwamba ushauri wake tumeuchukuwa na tunaufanyia kazi na hali itaporuhusu baada ya kukaa na pande zinazohusika na mambo ya ulinzi basi hilo suala tutalifanyia kazi mara tu baada ya kuonekana inafaa kufanya hivyo.

Vile vile, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, ndege ndogo na ndege kubwa zinalipa ada ya utuwaji kwa kiasi gani. Napenda kumuarifu kwamba, ada ya utuaji na uwezeshaji wa ndege inapangwa na mamlaka ya usafiri wa

Anga Tanzania, yaani *Tanzania Civil Aviation Authority*. Ada hiyo inatozwa kwa kuzingatia uzito wa ndege wa juu, yaani *maximum take off weight*, ndege hulazimika kulipa ada ya dola tano za kimarekani kwa tani moja au sehemu ya tani moja. Kwa mfano Ndege ya Oman *Air* inalipa jumla ya dola za kimarekani mia nne kila inapotua na ndege ya *Costal Air* inalipa shilingi arubaini na nne elfu kila inapotua.

Ameuliza vile vile kuhusu uegeshaji wa ndege ni kiasi gani. Kama nilivyomjibu suala lake la mwanzo, uegeshaji ndege inatozwa kwa mujibu wa uzito wa dege. Ndege zilizosajiliwa Tanzania zinatozwa shilingi elfu moja na ndege zilizosajiliwa nje ya Tanzania zinalipia dola tano. Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohd Said, alitaka kujua je, kuna haja ya kutenga maeneo ya kutengeneza viwanja vya kutoa helikopta.

Nataka kumjibu kwa kuna Sheria Nam. 9 ya usimamizi wa utuaji wa viwanja vya ndege na kamati imezinduliwa na hiyo kamati inayafanyia kazi masuala haya yote, lakini vile vile nataka kumuarifu kwamba mamlaka ya viwanda vya ndege Zanzibar kwa kushirikiana na mamlaka ya usafiri wa Anga Tanzania imeshafanya utafiti na kugundua baadhi ya maeneo ambapo tunaweza kujenga viwanja hivyo, kuna sehemu kule Paje ambapo Mhe. Jaku Hashim, anaijua sehemu hiyo inaitwa Domo Kuchu na vile vile, kuna sehemu Nungwi ambayo tumeitenga na Pemba tumetenga sehemu ya Mkakata na Kigomasha. Kwa hiyo, sehemu hizo zete tumetenga kwa ajili ya utuaji wa ndege za helikopta na lile suala lake kwamba, je, kule Uzi haiwezekani tukafanya kazi hiyo. Kama yeye mwenyewe alisema kwamba kuna siku tunategemea tutajenga Ikulu ndogo ya Mhe. Rais.

Nataka kumuarifu tu kwamba wazo lako tumelichukuwa na tutalifanyia kazi kwa kadri wa uwezo wetu na kadri ya sheria zitakavyoturuhusu. Baada ya hapo vile vile alitaka kujua kwamba kuna utafiti gani tumeufanya kuhusu takwimu za abiria wa kimataifa waliowasilishwa na wizara na idadi ya watalii wanaotumia katika kiwanja kile cha *Air Port* chetu ya kimataifa cha Mhe. Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, napenda kumuarifu kwamba mamlaka ya viwanja vya ndege kazi wanayofanya wao ni kukusanya *data* zote kwa watumiaji wa viwanja vyetu vyote vya ndege, sisi hatuangalii watalii. Kazi ya kuangalia watalii ni kazi wa wizara husika ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Kwa hiyo, ndio maana unakuta takwimu zinatafautiana na wao kwa sababu wao waangalia zaidi katika utalii na sisi tunaangalia abiria wote kwa jumla wanaofika katika viwanja vyetu vya ndege.

Vile vile, Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, alitaka kujua kuna matatizo ya hesabu katika kukusanya na kutumia. Nataka kumwambia kwamba bajeti yetu inatumia *cash budget,* kwa hiyo, hamna tatizo lolote katika kutumia na mapato yetu na kuna wataalamu, vile vile, *CAG* inafanyakazi zake vizuri, kwa hiyo, mimi namtoa shaka kwamba hatuna tatizo lolote katika suala hili.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir, alituulizia kuhusu uwekaji wa mkanda. Ni suala muhimu sana na sisi tulipoenda kutembelea viwanja vya ndege tulionana na Mkurugenzi Mkuu wa Uwanja wa Ndege na akatuahidi kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2016/17, hatua ya mwanzo ni kuhakikisha kwamba ule ukanda wa kuchukulia mizigo ya abiria pamoja na wale wanaoondoka na wanaosafiri tunahakikisha kwamba ile *belt* tunajenga na sehemu tayari ishatengwa ambayo itakuja kuonekana baada ya kufanyia hiyo kazi.

Mwisho, Mhe. Spika, naendelea zaidi na hapa nimebakiwa na wachangiaji wachache katika Mamlaka ya Uwanja ndege ni Mhe. Miraji Khamis, ameuliza kwa nini Mamlaka imeingia mkataba na Kampuni ya *Transfad* wakati hatujawapatia eneo la mizigo. Napenda kumuarifu kwamba baada ya kusaini mkataba Kampuni ya *Transfad* tumepatiwa eneo la kuwekea mizigo na kwa sasa kuna jengo kubwa zaidi linajengwa kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo za mizigo ili kurahisisha usafiri wa kuleta mizigo na zile tani zitapate kuongezeka kama nilivyosema mwazo na Qatari imeonesha nia ya kuleta mizogo.

Vile vile, Mhe. Maryam Than, anayaomba mashirika ya ndege kupunguza gharama za nauli hasa kule Pemba. Tunamwambia wazo lake tunalichukuwa na tutakaa Mhe. Spika, na wadau kuliangalia kwani wananchi wa Pemba hali zao za kimaisha ni duni, lakini wanapenda vile vile vitu ambavyo vitawarahisishia usafiri wao na vile vile katika kuongeza pato la nchi yetu na pato la mwananchi mmoja mmoja.

Mhe. Spika, baada ya hapo Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), aliulizia kuhusu vikosi kuwanyanyasa watu wanaosimamisha gari. Hili suala kusema la ukweli hatujapa malalamiko mpaka sasa hivi na kama malalamiko hayo yapo namuomba atuletee na vile vile, kwa kushirikiana na vikosi au Wizara ya Tawala za Mikoa, Idara Maalumu ya SMZ tuko tayari kuhakikisha kwamba hilo tatizo halitokei na wananchi wetu hawawezi kunyanyaswa kwani serikali ipo hapa kuwatetea wananchi wake na si kwa ajili ya kuwanyanyasa wananchi wake.

Mhe. Spika, vile vile, alitaka uletaji wa ripoti Barazani. Hili sisi tunavyofamu kwamba huu uletaji wa ripoti tumeuelezea humu katika kitabu chetu kuanzia ukurasa wa 15-20 kuhusu Mamlaka ambazo zinajitegemea zaidi. Kuhusu *ZA* lakini hata hivyo katika sheria yao haioneshi sehemu yoyote kwamba Mhe. Spika, wanatakiwa kuwasilisha ripoti. Kwama hiyo, taarifa ipo basi tutakaa kama serikali kuangalia tutajipanga vipi kuhakikisha kwamba hizo ripoti tunazileta hapa mwaka baada ya mwaka na yeye alikuwepo hapo kabla humu humu kama tulivyokuwa hivi sasa anaweza kutusaidia mawazo namna gani ya kuhakikisha hizo ripoti tunaziwasilisha.

Mhe. Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla, aliulizia kukosekana kwa uzio kwa kiwanja chetu cha Ndege cha Pemba. Nataka kumwambia kwamba uzio tumeshaanza kuujenga sasa hivi kwa kilimota tatu zimebakia kilomita mbili kwa sababu uzio wote ni kilomita tano, lakini hali itaporuhusu tutalimaliza lile eneo na kuhakikisha kwamba tunaendelea na kuwa na usalama nzuri zaidi kwa viwanja vyetu vyote vya ndege vya Zanzibar.

Vile vile, waliulizia kuhusu eneo letu lile la kiwanja cha ndege. Kama alivyosema Mhe. Simai Mohammed Said, vile vile, nataka kumuhakikishia kwamba hilo eneo sisi tunalichukuwa na kulifanyia kazi na kuhakikisha kwamba, kiwanja chetu cha ndege cha Pemba kinakuwa kikubwa zaidi ili ndege tafauti zipate kutua.

Mwisho kabisa nawashukuru wote waliochangia katika sekta hii ya viwanja vya ndege na tunahakikisha kwamba tuko pamoja nao katika kuhakikisha kwamba zile kero zote zilioko pale tunazifanya kazi ili kuleta maendeleo yenye tija kwa wananchi wetu.

Baada ya kutoka hapo Mhe. Spika, napenda kuzungumzia kidogo kuhusu Mamlaka ya Usafiri Baharini. Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Yussuf Hassan Said, Mhe. Spika, walitaka kujua kuhusu ***Maritime Labour Convention*** ambayo *MSL* ya 2006. Napenda kuwajibu kwamba, mkataba huo ni wa *ILO* una lengo la kuweka viwango vya haki na wajibu na wabaharia wa melini ikiwemo masaa ya kazi, masaa ya mapumziko, matibabu, chakula, vitendea kazi, makaazi, maslahi na marupurupu. Huu ni mkataba wa kimataifa ambao meli zote zinapaswa kuutekeleza. Lakini Tanzania kweli bado haijaridhia mkataba huu, hii ni changamoto kwetu sisi kwa sababu Zanzibar inasajili meli zake za kimataifa.

Uridhiaji wa mkataba huo unafanywa na Bunge la Jamhuri la Tanzania. Sisi tutakavyofanya sasa hivi tutawashauri waharakishe kupeleka Mswada wa Sheria katika Bunge ili na sisi tuingie katika mkataba huu wa kimataifa.

Vile vile, Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Simai Mohammed Said, walitaka kujua mapato yatokanayo na usajili wa meli za ndani na meli za nje. Kwa ufupi nataka kumwambia usajili wa ndani kuanzia kipindi cha Julai 2015 mpaka Machi 2016 meli 9 tulizozisajili humu ndani mapato yake yalikuwa ni shilingi milioni hamsini na tatu na sabini na sita elfu, ama usajili wa kimataifa Julai 2015 Mach 2016 ni meli 87 na mapato yake ni milioni mia nane na sabini laki tatu elfu tisa mia nane na tisini na nne.

Mhe. Spika, vile vile, walitaka kujua ujenzi wa Afisi ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba utaanza lini. Taratibu zote za kupata kiwanja zimekamilika na muda wowote tutakapopata hati ya usajili tuaanza ujenzi wa ujenzi wa Afisi kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini.

Vile vile, waliulizia kuhusu upungufu wa wataalamu katika Afisi ya Mamlaka ya Usafiri. Tatizo hilo kweli lipo na tutajitahidi katika bajeti yetu hii ya 2016/17 tuhakikishe kwamba tuna wataalamu wa kutosha Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba kazi zinafanyika kwa ufanisi zaidi.

Baada ya hapo Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohammed Said, alitaka kujua wizara imechukuwa hatua gani katika matayarisho ya kuanza kutumika kwa utaratibu wa kimataifa kuthibitisha uzito wa makontena kabla ya kupakiwa melini. Napenda kumjibu tayari tumeshatayarisha rasimu ya kanuni kuthibitisha uzito wa makontena yanayoita ***containers*** *growth mass pacification* na tayari wizara imeshawasilisha kanuni hiyo kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitiwa kabla ya kutiwa saini na baadae kutangazwa rasmi katika gazeti la serikali.

Aidha, baadhi ya makampuni yameshapeleka maombi ya kupatiwa lesini na mamlaka ya usafiri baharini kwa ajili ya huduma hiyo. Wizara inategemea ikifika tarehe 1/07/2016 matayarisho yote yatakuwa yamekamilika ili tuanze kazi mara moja.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, alitoa ushauri wa kuwa na maboya, mawasiliano, na *life jacket* kwa wenye vyombo vidogo vidogo. Sheria ya usajili wa vyombo vidogo vidogo inawataka kwamba wale wote wenye vyombo hivyo ambao sisi tunasajili vyombo vyenye urefu wa mita nne kwenda juu viwe na simu, wawe na maboya na vifaa vyengine vyote katika mambo ya uokozi na vile vile,

wapate kuwasiliana na kituo chetu kikuu cha mawasiliano. Kwa hiyo, sisi tunaifanyia kazi na kila wakati sisi tuna ukaguzi wa mwaka, tuna ukaguzi wa ghafla na kuna ukaguzi mwengine wote ambao sisi tuna sheria inaturuhusu kuzifanyia hizo meli au mashua zote ambavyo zinastahiki kuingia katika usajili wetu. Na ninamuhakikishia kwamba tupo vizuri na ninahakikisha kwamba hizi mashua ndogo ndogo na meli zote zinaendelea kufanya kazi vizuri bila ya kupata ajali zinapokuwa kazini. Kwa kipindi hichi tunashuhudia kwamba ajali za meli na hata na hizi mashua na meli ndogo ndogo zimepungua sana Mhe. Spika.

Baada ya hapo Mhe. Spika, Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, alitaka kujua kuhusu vibanda vya kuuzia tiketi na matatizo wanayopata wananchi kuuziwa tiketi kwa bei za kuruka. Mimi kwanza ninapenda kutoa wito Mhe. Spika, kwa Waheshimiwa Wawakilishi, washirikiane na wananchi wao wa majimbo yao kuhusu kuwafahamisha kuwa mtu yeyote asikubali kununua tiketi kwenye vituo au sehemu ambazo hazipo kwenye utaratibu wetu. Wanunue kwa mawakala wetu wa tiketi na pale inapotokea tatizo wakauziwa tiketi ambayo si ya bei halali, basi tunamuomba atoe taarifa na hatua kali zitachukuliwa kwa mawakala hao za kuwafutia leseni zao.

Hivyo, Mhe. Spika, ninamshauri Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, watu wake na watu wetu wote tuwashauri kwamba wawe na vitambulisho vyao wakati wa kwenda kununua tiketi, ili kujua kwamba yeye anapata tiketi halali na jina lake linakuwepo. Kumetokezea baadhi ya utaratibu mtu anapokuwa na safari ya ghafla anakubali kuuziwa tiketi ya mkononi, hiyo ndiyo inayopelekea sasa kuuziwa tiketi kwa bei za kuruka na matokeo yake anakuwa hawezi hata yeye mwenyewe yule kwenda kuleta malalamiko kwa sehemu husika. Mhe. Spika, mimi ninawataka sana wananchi wafuate sheria na pale patakapokuwa na malalamiko wasiache kuyapeleka katika mamlaka yetu husika na tutayafanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Hidaya Ali Makame, alitaka kujua kuhusu suala la uhuwishwaji bandari ya Nungwi. Kwanza ninapenda kumjibu kwamba bandari zilizo rasmi kisheria kwa Unguja zipo mbili; ipo Malindi na Mkokotoni na Pemba zipo tatu; Wete, Mkoani na Wesha. Kwa hivyo, bandari ya Nungwi hii mpaka sasa hivi bado haijawa rasmi. Lakini kama kutakuwa na uwezekano wa kuiweka katika bandari zetu basi sisi tupo tayari kufanya hivyo. Hivyo, ninataka kumwambia tu kwamba Mhe. Hidaya, kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kwa kushirikiana na *SUMATRA* kwa upande wa Tanzania Bara kwa pamoja zimekuwa zikiratibu vikao vya Wakuu wa Mikoa kuhusiana na changamoto za bandari ambazo si rasmi.

Mhe. Spika, kuna bandari bubu nyingi sana zisizopungua mia tatu na thalathini. Bandari hizi ni nyingi, lakini sisi kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi za Mikoa na Wilaya tutahakikisha kwamba hizi bandari bubu haziwezi kuwa na nafasi, kwani inaikosesha nchi yetu mapato. Tutahakikisha kwamba hili suala tunalifanyia kazi, tumekaa pamoja na Wakuu wa Mikoa kwa kupitia *SUMATRA*, Wakuu wa Mikoa wote Tanzania wameshakutana Mtwara na Dar-es-Salaam kulijadili suala hili na lipo katika hatua nzuri ya kuhakikisha kwamba hizi bandari bubu ambazo zinatukosesha mapato tunazipiga vita na kuhakikisha kwamba hazina nafasi katika serikali yetu hii.

Baada ya hapo Mhe. Spika, ninapenda kulikumbushia zaidi suala la ukaguzi wa vyombo na kupatiwa vifaa vya usalama. Hili pia nimeshamjibu Mhe. Dkt. Makame na Mhe. Hidaya Ali Makame, ninataka kuwaambia vile vile kwamba tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, mashua, meli ndogo, meli kubwa zote Mhe. Spika, ambazo zinatakiwa kuwa na vifaa yakiwemo maboya, *life jacket*, simu na nanga vile vile kuhakikisha kwamba vinakuwa havileti athari yoyote katika ajali. Na inapotokezea ajali tu basi sisi tunapata taarifa kwa haraka Mhe. Spika, na tunafika eneo la hatari ili kuokoa au kuchukua hatua zote za kuhakikisha kwamba vyombo vile vinakuwa havipo katika hatari na abiria wake vile vile.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninapenda kuwashukuru sana Wajumbe wote waliochangia katika sekta hii ya Mamlaka ya Usafiri Baharini. Baada ya hapo Mhe. Spika, ninaamua kuchangia hoja kuhusu Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kama nilivyokwambia kwamba suala lako la mwanzo Mji Mkongwe ni mji ambao upo katika hifadhi. Na imetubidi tuchukue hatua zile, ni maamuzi magumu, lakini tulikaa na wananchi wetu kuhusu kuifunga ile barabara na wametukubalia. Na ninakuomba na wewe vile vile utukubalie.

Kuhusu kukabiliana na ongezeko la majengo ya kileo. Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe inafanya kazi zake kwa kufuata Sheria Nam. 4 ya 2010. Kanuni za miongozo mbali mbali za hifadhi zikiwemo *Master Plan, Heritage Management Plan* na *World Heritage Guideline*. Baada ya mmiliki kuleta ombi lake, wataalamu hukaa na kujadili ombi hilo na muhusika hutakiwa kuleta vielelezo vyote kutegemea na mahitaji yake hapo ndipo utaratibu husika Mhe. Spika, hufanyika kwa kufuata muongozo ambao huandikwa katika vibali.

Vile vile, Mhe. Spika, alitaka kujua majengo mangapi yamehifadhiwa na mangapi hayamo katika uhifadhi. Ninapenda kumjibu Mhe. Jaku, Mhe. Spika,

kwamba eneo zima la uhifadhi wa Mji Mkongwe ni hekta 96 na *buffer zone* yake ni hekta 84.79. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1994 zilizotumika katika *Conservation Master Plan*, Mhe. Spika, idadi ya majengo ipo kama ifuatavyo. Nitamzungumzia zaidi kiasilia.

Nyumba zote zipo 2,444. Serikali inamiliki asilimia 22.7, binafsi 57.3, Wakfu asilimia 19.2 na mchanganyika ni asilimia 0.8. Kwa mujibu wa takwimu zilizofanywa Disemba 2000-2015 nyumba zote ni 2,628 Mhe. Spika.

Angalizo, Mhe. Spika, kwa vile Mji Mkongwe ni mkusanyiko wa majengo, miti, njia na vyote vilivyomo ndani yake na watu wake hivyo hivyo ni lazima vihifadhiwe kwa mujibu wa sheria na taratibu za uhifadhi. Ndiyo maana tunasema Mji Mkongwe ni *Living World Heritage City* na tutaendelea kutilia mkazo hili na kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe ule hatutakuja kunyang'anywa urithi na tutakuwa wakali kwa hili Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na tutafuata sheria zote zinazoturuhusu hata awe nani hatutakubaliana kwenda kinyume na sheria katika kuulinda urithi wetu wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, baada ya hapo anauliza kwa nini hadi ya leo sehemu iliyoanguka katika Beit Ajaib haijakarabatiwa. Ninapenda kumuarifu kwamba kama nilivyolijibu Baraza lako Tukufu katika maswali ya nyongeza kwamba tulichukua hatua ya mwanzo kulikarabati lile jengo kwa asilimia arobaini. Lakini baada ya hapo ulikuja ujio wa Waziri Mhe. Spika, wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Muscat Oman ambaye alituomba kwamba wao wapo tayari kuhakikisha kwamba lile jengo wanalifanyia ukarabati kutokana na historia yake.

Mhe. Spika, ninapenda kumuarifu kwamba hatua zote kama nilivyojibu kwenye Baraza lako Tukufu zimeshafanyika na wakati wowote baada ya kupata kibali kutoka wenyewe *UNESCO* tutaanza ujenzi mara moja. Na tupo katika hatua nzuri na vile vile, mwezi wa Julai tunakwenda kwenye kikao kitakachofanyika Uturuki ya kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe hauendelei kuwa katika hatari ya kuondolewa uhifadhi wake wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, baada ya hapo vile vile ninapenda kuzungumzia kidogo kuhusu idadi nyumba ngapi za Mji Mkongwe zipo katika hali mbaya. Ninataka kumjibu kwamba nyumba zilizokuwa katika hali mbaya za Mji Mkongwe ni 75 na zote hizo zinajulikana. Tushawaita watu binafsi kwa sababu nyumba nyengine zipo katika mamlaka yao, tumewaita na kukaa nao na kuwaambia kwamba wanatakiwa wahame ili kuokoa maisha yao na sisi tutahakikisha

kwamba watu wale wote wanahama kwa ajili ya kuhakikisha kuwa usalama wa watu wetu ni muhimu zaidi.

Mhe. Spika, alitaka kujua vile vile kuhusu tunatumia sheria gani katika kuwaadhibu wale ambao watahakikisha kwamba hawahami katika majengo. Kama nilivyotaka kumwambia kwamba kuna sheria hapa ambayo Kifungu Nam. 39(1) cha Sheria Nam. 4 ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe inasema kwamba;

"Nyumba iwapo itaanguka wenyewe basi yule ambaye imeanguka atatakiwa aifanyie ukarabati na yule ambaye ataiangusha kimakusudi, basi mtu yule atatozwa faini isiyopungua milioni mbili au kifungu cha miezi kumi na mbili au adhabu hizo zote zitakwenda kwa pamoja".

Mhe. Spika, baada ya kujibu masuala mengi kwa sababu yaliyoulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye ni mdau mkubwa wa Mji Mkongwe na ninashukuru kwa sababu ananisemea kama mimi Mwakilishi wa Jimbo langu la Malindi, ninamshukuru sana kwa hilo. Hivyo, ninaimani kubwa kwamba masuala ya Mji Mkongwe nimemjibu vizuri katika suala hilo na ataridhika na majibu haya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohammed Said, alitaka kujua kuhusu kuna mpango gani wa jengo la Ngome Kongwe ambalo linaitwa kwa Kiingereza *Old Fort*. Mhe. Spika, tunakubaliana na Mhe. Simai, kwamba matengezo ya jengo la Ngome Kongwe ni makubwa na yalitakiwa yafanyike haraka. Mimi ninapenda kumuarifu kwamba sisi tunaendelea kufanya matengenezo madogo madogo na hali itakaporuhusu, matengenezo makubwa tutayafanya. Lakini ninataka nimuarifu kwamba ile haiba ya jengo lile la Ngome Kongwe ndiyo linavyotakiwa liwe vile. Kwa sababu jengo lile limeekwa katika *momentum building class number one*. Kwa hivyo, sisi hatutakiwi kulifanyia ukarabati kule nje wa aina yoyote. Hivyo, kuwepo vile ukongwe wake ndiyo haiba yake inawavutia zaidi watalii, kwa sababu ni ya aina ya kipekee kwenye nchi yetu. Kwa hivyo, tutaendelea kufanya ukarabati kwa kushirikiana na Wizara husika ili kuhakikisha kwamba lile jengo linaendelea kudumu kwa wakati wote Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ninapenda kutoa angalizo vile vile, pamoja na kuwa jengo hilo kwa muda mrefu halifanyiwa matengenezo yoyote, tukumbuke kuwa usanifu namna lilivyosarifiwa ni wa kipekee. Sura yake ya nje pamoja na kuwa inaonekana ni chakavu, inatakiwa ibakie vile vile.

Baada ya hapo Mhe. Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa, aliulizia kuhusu mradi wa ukuta au ukingo wa bahari Mizingani umechukua muda mrefu na unamalizika lini. Ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu lakini hii imetokana na kwamba wataalamu wetu washauri walisema kuwa ule ukuta kama munavyojua chumvi inatakiwa kuwe na vifaa maalum vya ujenzi. Saruji inayotumika pale ni saruji ya kitaalamu ya kipekee ambayo inahimili chumvi na vile vile, hata kokoto zinazotumika pale ni kokoto za kipekee Mhe. Spika, ambazo zinatakiwa zitumike katika ujenzi wa ule ukuta wa Mizingani. Hivi sasa tunaendelea vizuri na ujenzi wa ule ukuta na tumeshafikia asilimia 35 na tunahakikisha kwamba wanaendelea na kazi zaidi ya ujenzi ili waukamilishe kwa haraka zaidi na haiba yetu ya Mji Mkongwe iendelee kuonekana katika Mji Mkongwe hasa maeneo yale ya Forodhani.

Mhe. Spika, suala letu la mwisho lilikuwa kuhusu Mhe. Panya Ali Abdalla, kuhusu Jumba la Treni. Kama nilivyosema mwanzo na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira walipokuja kuwasilisha bajeti yao hapa kwamba lile jengo kweli lipo katika Mamlaka ya Mji Mkongwe, lakini vile vile hivi sasa tumelipeleka kwa *ZSSF* kwa mkataba maalum ili wao walitengeneze na baadae lizalishe kwa kipato zaidi. Lakini wale wote ambao wanastahiki katika jengo lile na wanaostahiki kupata milango ya kibiashara ambayo orodha yao ipo, basi wale watapewa haki yao inavyostahiki na hilo wala asiwe na wasi wasi. Lakini mandhari yake itakuwa kama ile ya zamani kwa sababu ya uhifadhi wa Mji Mkongwe, lakini itakuwa na haina nzuri. Na nina hakika kwamba tulikuwa na maonesho juzi pale eneo la Mnara wa Mapinduzi, nina imani wananchi wengi wameenda pale wajionea wenyewe jinsi ya ile haiba ya jengo lile litakavyokuwa baada ya kumalizika kujengwa.

Baada ya hapo ninashukuru sana Wajumbe wote waliochangia katika sekta hii na tutakuwa pamoja na wao kuhakikisha kwamba zile changamoto walizotwambia tunakabiliana nazo na matatizo tunayatatua kwa maslahi ya nchi yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya hapo ninakuja sasa katika *hot issue* kuhusu Shirika la Bandari. Mhe. Spika, kwenye sekta hii ni sekta ambayo imechangiwa na Wajumbe wengi. Ninapenda kuwashukuru wale wote waliochangia, wameonesha namna gani wanavyoumwa na nchi yao na zaidi mapato kwa nchi yao. Sisi vile vile tunapenda kuwahakikishia kwamba hatulali, mimi mpaka jana nilikuwa ninafuatilia mazungumzo kupitia mitandao ya Waheshimiwa tofauti na wametoa mawazo tofauti na kusema la ukweli michango yao imeonesha wazi kwamba, wanaguswa na wanaumia na suala hili. Kama wanavyoguswa wao, mimi na Mhe. Waziri na timu yetu yote ya wizara

tulikuwa watu wa mwanzo baada ya kupewa tu uteuzi huu na Mhe. Rais, jambo la mwanzo kwenda kuangalia mrundikano wa makontena katika bandari yetu ya Malindi.

Mhe. Spika, kusema kweli hilo suala kweli lipo na hivi juzi tu kama nilivyosema meli sita zimefunga, zipo hapa nje zinataka kuja kufunga gati. Lakini kama tulivyosema mwanzo hali yetu ya pale hairuhusu kwa meli zote kufunga kwa wakati mmoja. Lakini tunajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba zile meli zinapakua makontena yao kwa haraka na wale wenye makontena yao wanayachukua baada ya kufanyiwa taratibu zote za kisheria na yale makontena matupu vile vile yanaondoshwa pale.

Mhe. Spika, ninapenda kuwaambiwa tu Wajumbe wako wa Baraza Tukufu kwamba kuanzia tarehe 6 Juni mpaka tarehe 14 Juni, meli hizo sita zimeweza kufunga hapo na nyengine zinataka kufunga zikiwa na makontena 2,086. Mhe. Spika, ni makontena mengi sana kutokana na ufinyu wa nafasi yetu pale na hii imetokezea baada ya eneo la Bwawani ambalo tulikuwa tukiweka makontena yetu, eneo lile kuchukuliwa na mwekezaji.

Mhe. Spika, ni jana tu tumezungumza na mwekezaji yule pale, kwanza tunamshukuru kwa nia yake ya kuonesha kwamba yupo tayari kutuachia eneo lile mpaka mwezi Disemba ili tuweke tena makontena yetu. Tunamshukuru sana mwekezaji yule. Nitakachoomba tu kwa sababu tayari yule mwekezaji yupo chini ya Wizara ya Fedha, tutakaa na Wizara ya Fedha na yule mwekezaji tuhakikishe kwamba kwa haraka zaidi tunaenda kuweka makontena pale Bwawani kutatua *crisis* hii kubwa ambayo inatukosesha mapato na vile vile, inachangia katika uongezaji wa bei kwa bidhaa za mlaji. Inatuuma sana, hatulali. Hii hatua tuliyofikia ni nzuri na vile vile, kuna wawekezaji ambao pia wanaumia katika hili wameshakuja na mawazo yao ya kutaka kuanzisha bandari kavu, wameshayataja maeneo, tunayafanyia utaratibu na kuyajua. Eneo moja lipo Mtoni huku upande wa Kiwanda cha Ngozi na eneo jengine pale Mtoni Garagara na jengine Fumba. (*Makofi*)

Lakini sisi tutaangalia na sehemu nyengine ambazo zitaturahisisha kwa urahisi zaidi kuyapeleka makontena bila ya gharama zaidi, isiwe kwamba tunayaondosha makontena ndani bandarini, tunayapeleka nje Mhe. Spika, gharama zinakuwa ndiyo vile vile. Kwa hivyo, hili tunalijua sana, tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi wakubali kwamba tuna nia ya dhati ya kuliondosha, lakini muarubaini wa wote ni ujenzi wa bandari yetu ya kiaina ya Mpigaduri.

Kwa hivyo, tutaharakisha pia na ujenzi wa bandari ya Mpigaduri unakwenda kwa haraka. Mhe. Spika, tunaishukuru Serikali ya China wameshakuja kuchukua *sample* ya udongo na harakati nyengine zitaendelea ili kufanikisha ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wawakilishi, tunajua juhudi zenu munazochukua kutushauri na masikitiko yenu na mimi mwenyewe nimejionea nilivyokuwa katika mitandao mpaka saa tisa za usiku, Waheshimiwa, sitopenda kuwataja majina yao walikuwa wakitoa ushauri na ushauri wao tunaupokea na tunaufanyia kazi. Na ninampongeza sana Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Mwadini Makame. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikija kwenye suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu ukosefu wa kuondoshea mizigo. Kama nilivyosema katika kitabu chetu cha bajeti, kuna vifaa ambavyo tayari tumeshavinunua na kuna vifaa ambavyo vipo kweli kwenye sehemu tulivyokwenda kuviagizia na kuna vifaa ambavyo vyengine bado tunamalizia *processes* za kibenki, lakini vifaa hivyo tunategemea kwamba akipenda Mwenyezi Mungu mwanzoni tu wa awamu hii ya bajeti ya 2016/2017 vitakuwa vimeshafika. Kwa hivyo, ninataka kumuarifu kwamba vifaa ambavyo vimeshafika kuanzia mwezi Mei mpaka Juni 2016, ni *folker lift* tatu, *terminal tractor* mbili, na *terminal trailer* mbili, maboya saba na taa za *solar* tano hivyo tayari vimeshafika na vimeshaanza kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Vile vile, kuna *cranes* mbili kubwa ambazo zipo njiani na zinategemea kwamba Julai zitakuwa tayari zimeshafika. Kwa upande wa *reachstacker* ambazo ni muhimu sana katika mambo ya kupakua mizigo na makontena ninavyokusudia. Sasa ninapenda kuliarifu kwamba tushaandika wenyewe wanaita *letter of credit* kwa Benki yetu *People's Bank* tokea Februari 2016. Kuna *processes* zinaendelea na *processes* hizo lakini zimeleta matumaini na wale ambao wanatutengenezea hivyo vifaa, wamesema wao watakapothibitishiwa tu kwamba tayari hiyo hati au hiyo tunayoita *letter of credit* ipo, basi wao vile vifaa ambavyo ni Kampuni ya Ferrari ya Italy, basi watahakikisha wanavileta kwa haraka ili kutatua tatizo hili la kupakua makontena ya kuyaondosha makontena kwa haraka zaidi. Mhe. Spika, kwa hivyo, tupo katika jitihada hizo na hivi vikwazo kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutavishinda na baadae hali ya kawaida itarejea ya kuhusu makontena kupakua na kuyaondosha pale katika eneo letu la bandari.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, anataka kujua Shirika la Bandari kuwachukulia dhamana wafanyakazi wake kwa *NMB*. Ninapenda kumuarifu kwamba sisi hupenda kuwachukulia dhamana wafanyakazi wetu wote wanaotaka kukopa, kwa sababu tunajua kwamba binadamu mahitaji yake yote hayawezi kumalizikia kwa mshahara tu, anatakiwa vile vile apate japo mkopo

wa kufanya kazi zake nyengine. Tatizo lililokuwepo ni kwamba *People's Bank* na Benki za *CRDB* zinaingia mkataba na mfanyakazi moja kwa moja. *NMB* na sisi sote ni mashuhuda humu, wanachotaka wao ni lazima waingie mkataba na Shirika la Bandari. Lakini Sheria ya Bandari...

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, una dakika 5.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante, ninamaliza Mhe. Spika, zimebakia chache tu hizi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Shirika la Bandari haliwezi kuingia katika mkataba huo kwa sababu sheria hii inawazuwia.

Jambo la mwisho, Waheshimiwa Wajumbe, kama Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Shamata Shaame, walitaka kujua kuhusu uendelezaji wa bandari ya Wete. Nataka kuwaambia kwamba uendelezaji utaanza mwezi huu wa Juni, vile vile, tuna mpango wawekezaji wameshaonesha nia ya kutaka kujenga gati pale Wete, ambapo gati hiyo ikiwa tayari basi itasaidia sana kupeleka meli nyengine pale na kusaidia urahisishaji wa usafiri.

Vile vile, waliulizia Bandari ya Mkoani kuhusu, je, hayo makontena yataondolewa kwa chombo gani. Katika hizo *cranes* mbili zitakazokuja zenye ujazo wa tani 25, moja tutaipeleka Pemba na vile vile eneo tumeliweka ambalo sasa hivi tunalisafisha ili baadae meli zile ndogo zitakapopeleka makontena, basi makontena yale yawekwe nje kidogo ya bandari yetu ambapo eneo lile ambalo tayari tumeshaanza kulisafisha.

Suala la mwisho kabisa katika sekta hii liliuliziwa kuhusu uendelezwaji wa Bandari ya Mkokotoni na wafanyakazi wa Kundi C pale Malindi. Wafanyakazi wa kundi C kama mnavyojua wako wengi zaidi ya 500, lakini tutahakikisha kwamba wafanyakazi hawa tunawafanyia utaratibu wa kuwaajiri pale ajira zitakapotokea kwa mujibu wa uwezo wao na uzoefu wao.

Vile vile, kuhusu suala la kwa nini hawapatiwi vile vifaa. Vile vifaa hatuwezi kuwapatia wao kwa sababu wale hawaingii kila wakati na Bandari ya Mkokotoni tumechukua wazo lake Mheshimiwa na tutahakikisha kwamba tunalifanyia kazi.

Mhe. Spika, baada ya hapo, nije kwenye Shirika la Nyumba ambapo kuna masuala kama mawili tu. Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe kwamba, sisi wizara tunawapenda wananchi wetu, Shirika la Nyumba

halikuongeza bei zake kwa kiwango kama wanavyofikiria watu. Tulifanya utafiti, tumejua kwamba nyumba nyingi za mjini sasa hivi zimekuwa ni *big issue*, hata zile nyumba ambazo wananchi wetu wamepewa na Mzee Abeid Aman Karume bure, ama kwa kutoa yeye mwenyewe au kwa kubomolewa, wanakodisha nyumba ile kwa chumba au nyumba nzima kwa zaidi ya shilingi 250,000. Sisi tunachokifanya pale kwa nyumba zote za mjini za Michenzani na nyenginezo, kwa kila chumba tunawatoza shilingi 25,000, kwa nyumba za Mpapa na Bambi shilingi 20,000 na nyumba za vijijini kama kule Pemba na Kengeja na kwengineko tunatoza shilingi 15,000. Tunajua nyumba zetu ziko katika hali mbaya, tulitembelea Kengeja na Kilimatinde zote.

Kwa hivyo, tunawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba, tatazifanyia ukarabati ili ziwe katika haiba nzuri na wananchi wazipende na wakubaliane na hizi bei tulowawekea. Kwa hivyo, sisi hatutowatoza wananchi wa vijijini bei kubwa kwa vile tunajua ni wananchi wenye kipato cha chini. Lakini tutaangalia na thamani ya majengo na wenzetu wanavyotoa kodi zile. Kwa wale waliopewa bure hatuwatozi kodi, wale wanaochukua vilemba ndio tunawatoza kwa nyumba zenye vyumba viwili shilingi 50,000 na vyumba vitatu shilingi 75,000, sio pesa nyingi Waheshimiwa. Tunawaona Wakfu wanatoza pesa nyingi kuliko sisi na hata watu binafsi.

Kwa hivyo, wananchi watuonee huruma serikali kwamba, tunawajali na tuko tayari kuhakikisha kwamba matatizo yao tunayatatua, na pale ambapo wanahisi kuna jambo lolote basi wawatumie wadau wao kukutana na sisi, na sisi tuko tayari kuwasaidia kwa sababu sisi ni Serikali ya Mapinduzi yenye kuwajali wanyonge, wakulima, wafanyakazi, wakwezi na wavuvi vile vile kama alivyosema Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, namalizia kuhusu Shirika la Meli nayo pia kulikuwa na *hot issue* kuhusu meli yetu ya *MV* Mapinduzi. Ni kweli meli yetu ina changamoto, milango yake ya kuchukulia mizigo haifunguki kutokana na kwamba iko chini, haiko juu, lakini sasa tumeamua kwamba ile meli tusiifanyie ukarabati wa aina yoyote yasije yakatokezea kama yalivyotokezea katika meli ya *MV Skagit*, tuyawache katika maumbile yake yale, isipokuwa sisi kama juzi mulivyosikia mtaalamu wetu mmoja ambaye ni Katibu wetu Mkuu napenda kumpongeza kwa hili, alionesha ujuzi wake na ile meli ikafunga Kaskazini kuelekea Magharibi ambapo ndipo ile sehemu ya ule mdomo wetu wa mlango unaweza kukaa chini. Kwa hivyo, ule mlango umeonekana kwamba kwa Pemba Mkoani inawezekana, isipokuwa kuna matengenezo kidogo, na Malindi tutatengeneza sehemu hiyo.

Vile vile, ile meli yetu tunaifanya kibiashara lakini pia tunajali maslahi ya wananchi wetu, ndio maana unakuta hata bei zake ni za chini. Waliulizia mbona haionekana kwenda Dar-es-Salaam, itakuwa inakwenda, lakini pia tunaangalia na mahitaji ya watu zaidi yako Pemba. Wanauliza kwa nini Maendeleo inachukua mizigo mingi. Maendeleo iko zamani na inachukua tani nyingi kwa sababu ile inachukua 600 na Mapinduzi inachukua 200. Magari tunavyoyachukua yale yanavyoonekana pale, tulikuwa tunachukua Mhe. Spika, kwa kutumia *crane*, lakini imeonekana kwamba wananchi wale wenye magari yao wanalalamika kwamba yanapata matatizo na kuharibika. Kwa hivyo, tumesitisha zoezi hilo mpaka tutakapotatua hizi changamoto kwa kutegemea sehemu nyengine baada ya Malindi na sehemu nyengine.

Mhe. Spika, kuhusu wazo lake la kuboresha huduma zetu. Tukumbuke tu kwamba hii ni meli ya serikali ya kuwasaidia wanyonge, lakini tutahakikisha kwamba kwa mujibu wa ilani yetu ya uchaguzi basi meli ile tutaiendesha kifaida na tuna wataalamu wazuri ili ije kuzaa meli nyengine kwa mujibu wa ilani yetu, na baadae shirika liendelee kufanyakazi yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba nimejibu hoja za kutosha kwa Waheshimiwa Wawakilishi na nina imani kubwa kwamba watatuunga mkono na mabuti yatapungua sana, kwani nia yetu sisi ni kuhakikisha kwamba hii serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein inafanyakazi zake kwa ufanisi na inawajali wananchi wake na kuhakikisha kwamba tunatekeleza kwa ukamilifu ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/20 na dira ya 2020 ya kumpeleka mwananchi katika uchumi wa kipato cha kati. Nia tunayo, inawezekana, tutimize wajibu wetu. Ahsanteni sana na nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa wakati wako huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kwa heshima na taadhima, nimwite Mhe. Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili sasa na yeye aje ahitimishe hoja yake. Mhe. Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, nataka kwanza nikushukuru kwa kunikaribisha katika Baraza hili tukufu, ili na mimi nije kutoa shukrani zangu. Kwanza kabisa nataka nimshukuru Naibu Waziri wangu kwa kujibu maswali mengi ambayo yaliulizwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara hii inawagusa watu wengi sana kwa mambo mengi sana. Kwa hivyo, mimi sikushangaa kwamba maswali yalikuwa mengi na maswali

mengine yaliulizwa hapa Barazani na maswali mengine yameulizwa kwa maandishi. Kwa hivyo, nashukuru pia kwamba Mhe. Naibu Waziri, amejibu karibu maswali yote ambayo yameulizwa. Mimi sasa hivi la kufanya ni kushukuru tu, kuwashukuru wale ambao walishiriki katika kutoa michango yao na pia nataka niwataje kwa majina.

Mhe. Spika, waliochangia hoja kwa moja ni:

1. Mhe. Suleiman Sarahani Said
2. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Machano Othman Said
6. Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata
7. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
8. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
9. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
10. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
11. Mhe. Simai Mohammed Said
12. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
13. Mhe. Shehe Hamad Mattar
14. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
15. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
16. Mhe. Omar Seif Abeid
17. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
18. Mhe. Bahati Khamis Kombo
19. Mhe. Mussa Foum Mussa
20. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
21. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
22. Mhe. Hamza Hassan Juma
23. Mhe. Shamata Shaame Khamis
24. Mhe. Suleiman Makame Ali
25. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
26. Mhe. Miraji Khamis Mussa
27. Mhe. Salma Mussa Bilal
28. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
29. Mhe. Maryam Thani Juma
30. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa
31. Mhe. Panya Ali Abdalla
32. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
33. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

34. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
35. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali,
36. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo. Nisimsahau pia,
37. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Namshukuru huyu kwa kufanyakazi nzuri ya kujibu maswali.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nilikua nataka nijenge itikadi katika Baraza lako tukufu, kwamba maswali mengi ambayo yataulizwa wizara hii, au ataulizwa waziri atakuwa anajibiwa na Naibu Waziri. Hii inakwenda sambamba na mfumo wa Kiingereza ambao tunaufuata, wa kusema kwamba Naibu Waziri anakuwa ndiye *Parliamentary Secretary*. Kwa hivyo, Naibu Waziri wangu atakuwa ananisaidia katika hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, nataka niwashukuru wajumbe waliochangia kwa maandishi, ambao ni:

38. Mhe. Omar Seif Abeid
39. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
40. Mhe. Hamza Hassan Juma
41. Mhe. Zaina Abdalla Salum
42. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
43. Mhe. Said Omar Said
44. Mhe. Mussa Ali Mussa
45. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa
46. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
47. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
48. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame
49. Mhe. Ali Khamis Bakar
50. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
51. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
53. Mhe. Ussi Yahya Haji
54. Mhe. Mgeni Hassan Juma
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
57. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
58. Mhe. Hidaya Ali Makame
59. Mhe. Shaib Said Ali

Mhe. Spika, kama nilivyosema maswali mengi yameshajibiwa, lakini kulikuwa na masuala mawili, matatu ambayo yanahusu Sera ya wizara hii, nilitaka hayo

niyajibu kwa ukamilifu. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, yeye alikuwa anaulizia kuhusu wafanyakazi waliopatiwa mafunzo katika Idara ya Usafiri na Leseni kwa kule Pemba. Namuhakikishia kwamba wanafunzi hao watatu tayari wameshapata mafunzo hayo katika mwaka huu.

Vile vile, aliuliza swali kuhusu ofisi na usafiri kwa Idara ya Usafiri na Leseni kwa Pemba. Napenda kumuhakikishia kwamba kazi inafanyika, uboreshaji wa hali ya ofisi unafanyika na kazi ile itamalizika katika bajeti ya mwaka huu 2016/2017.

Jengine alilokua akiuliza ni kuhusu utaratibu ambao tunautumia kutoa leseni. Napenda kumuhakikishia kwamba, ukaguzi wa kila aina unafanyika kabla ya leseni kutolewa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, alikua anaulizia wizara kwa kupitia Idara ya Mawasiliano, vipi inafuatilia suala zima la matumizi mabaya ya mitandano. Hiyo bila shaka Waheshimiwa Wajumbe, mmeshasikia kwamba kwa upande wa Jamhuri ya Muungano sheria hizi zimeshakuwa zinatumika. Kuna mtu huko Tanzania Bara aliwahi kutumia mtandao vibaya na akachukuliwa hatua.

Mhe. Spika, hapa Zanzibar kwa utaratibu ina lazima Baraza lako tukufu liridhie sheria ambazo zinapitishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunategemea kulizungumza suala hilo. Moja wapo tutaamua tuipitishe sheria ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itumike na Zanzibar au tunaweza pia tukaunda sheria yetu wenyewe, uamuzi utakuwa ni wetu wenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohamed Said, kauliza maswali hapa, hasa swali kama serikali imeingia mkataba na Kampuni ya *ZANTEL* katika uendeshaji wa mkonga, mpaka sasa kuna faida na kama kuna faida ni kiasi gani.

Mhe. Spika, kwa ufupi tu nataka kusema kwamba Mhe. Simai Mohamed Said, ujuwe tu kwamba mambo haya ni endelevu yanaendelea kila siku, tunazidi ku-*negotiate* katika mambo haya, mazungumzo yanaendelea, lakini pia yako makubaliano kwamba iwapo mkonga unaharibika basi utatengenezwa na wale ambao walioujenga, ni Wizara ya Fedha na Mipango wamelipia na wizara yetu huku tunasimamia. Kwa hivyo, hilo Mhe. Mjumbe, nakuhakikishia tu kwamba linafanyiwa kazi.

Swali jengine uliuliza nani anawajibika kufanya matengenezo kwa mkonga wa taifa katika barabara ya Mwanakwerekwe. Kwenye hili nitapenda kulihakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba kazi hizo huwa

zinalipiwa na taasisi husika. Hapa katika kujenga njia ile tumekubaliana kwamba fedha zitakazotumika zitatoka katika *road fund*. Kwa hivyo, wao watashiriki pia katika hilo.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, alitaka kujua tatizo la *internet* katika taasisi za serikali Pemba. Napenda kumuhakikishia kwamba suala hilo linashughulikiwa, tunahakikisha kwamba wahusika hasa *ZANTEL*, watalishughulikia suala hilo na kuhakikisha kwamba ile wanaita *last mile connectivity* kwenye maofisi ya serikali, pia, mkonga huo utafika kwa upande wa Pemba.

Mhe. Omar Seif Abeid, alikuwa anataka kujua, anasema *ZANTEL* imekuwa na matatizo ya kutoa huduma za simu katika kiwango cha chini zaidi, ukilinganisha na makampuni mengine ya simu. Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba, *ZANTEL* ni *upgrade*, utaratibu wake wa kutoa huduma za simu na kwamba wameshaanza kazi ya kuleta mitambo mipya kutoka Kampuni ya *Reckson*, tunategemea kwamba ukifika mwezi wa *August* au *September* kazi hiyo itakuwa imekamilika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi, alizungumzia kuhusu Mamkala ya pesa, *M-Pesa, Tigo* na *Airtel Money*. Kwenye hili ningependa kujibu tu kwa haraka sana kwamba inashughulikiwa Kimuungano na kama kuna kodi zinakatwa na *TRA*, na kile kiwango cha kodi ambacho kinaletwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, huletwa kama kawaida.

Mhe. Spika, kuhusu maeneo ya Fuoni kuna matatizo ya *Echo 4G*. Jibu lake ni lile lile kwamba *ZANTEL* wanaboresha mitambo yao na kwamba ikifika mwezi wa nane tatizo hilo litakuwa halipo tena.

Mhe. Spika, kuhusu sheria ya mtandao italetwa lini Barazani. Suala hili itabidi sisi wenyewe tukae tushauriane na tukubaliane, kama nilivyosema awali kwamba tutafuata au tutapitisha ile Sheria ya Muungano au tutaunda sheria yetu hapa, uamuzi uko kwenu Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, Mhe. Shehe Hamad Mattar, alizungumzia kuhusu mkonga wa baharini kutoka Tanga kwenda Pemba. Mkonga wa baharini kutoka Tanga kwenda Pemba bado haujaanza kutumika, lakini mazungumzo yanaendelea baina ya *ZECO* hapa na wahusika ili kazi hiyo ikamilishwe haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, alitaka kujua ni nani anayetoa vibali vya ujenzi. Kwa ufupi tu vibali vya ujenzi hutolewa na *Development Control Unit* ambayo iko hapa Zanzibar, ni kama kamati inayokaa watu wanakwenda kuomba vibali na wakiwa wametimiza masharti wanapewa vibali.

Mhe. Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa, alitaka kujua Bodi ya Wakandarasi imemaliza muda, ni utaratibu upi unaotumika katika bodi hiyo na shughuli zake. Mhe. Spika, kwenye hilo nataka kujibu kwa ufupi kwamba bodi mara nyingi hukaa miaka mitatu mitatu. Bodi hiyo imemaliza muda wake mwaka huu, Mhe. Rais mwenye dhamana ya kuchagua Mwenyekiti, keshachagua Mwenyekiti, na mimi ndiye mwenye dhamana wa kuchagua wale Wakurugenzi na nimeshawachagua hao Wakurugenzi na tunasubiri kuwatangaza. *(Makofi)*

Mhe. Zulfa Mmaka Omar, alitaka kujua *stand* ya magari ya maegesho katika mji wa Chake-Chake. Suala hilo pia limeulizwa na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman na pia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake-Chake alitaka kujua suala hilo. Kwa ufupi tu nataka kusema kwamba shughuli hiyo inaendelea, wahusika wote tunaanza kushirikiana kutafuta maeneo mbadala kufanya kazi hiyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, alitaka kujua ni hatua gani zilizochukuliwa kwa madereva wakorofi wa daladala. Jibu lake ni kwamba madereva wote wanaokwenda kinyume na sheria, wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 *Road Transport Act*. Hapa nataka niongeze tu kwamba kama kuna mtu kamuona dereva wa daladala anavunja sheria, basi aende kumripoti kwenye kituo cha karibu cha polisi hatua zitachukuliwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), alizungumzia suala la *route* ya Madina, hilo limeshajibiwa na Naibu Waziri wangu, natumai jibu linatosheleza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kuhusu madereva wa serikali hawapewi posho. Hili kalizungumzia na mimi nilikuwepo. Nataka nimjibu tu kwamba madereva wa viongozi wote wanapatiwa posho kama kawaida. Kwa hivyo, hilo linaweza kwenda kuangaliwa tu ikiwa hiyo posho inatosha au haitoshi, maana yake maisha ya sasa yamepanda. Kwa hivyo, namshukuru kwa suala hilo tutalishughulikia. Lakini nataka kumuhakikishia kwamba posho kwa madereva wa viongozi inatolewa kama kawaida.

Mhe. Spika, kuhusu barabara ya Fuoni haina *bus day* kama vile barabara ya Benjamini Mkapa. Nataka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe, kwamba kazi hiyo itafanywa na itamalizwa mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, Mhe. Shehe Hamad Mattar, kuhusu abiria kulipa nauli kwa mujibu wa masafa. Jibu lake ni kwamba nauli zote za gari za abiria Unguja na Pemba zinapendekezwa na Jumuiya za magari na abiria kwa bodi ya usafiri ya barabarani na kutangazwa rasmi na Serikali baada ya kuzingatia masafa yenyewe, kwa hivyo, hilo ni jambo endelevu linaendelea na kwamba kila wakitaka kupandisha bei basi lazima waende kwanza kwenye kamati husika ili wakalizungumzie hilo.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, naye alizungumzia suala kama hilo na jibu lake ni kwamba Wizara imeshapendekeza sehemu zote zinazohitajika kuweka vituo vya daladala na *bus stops.* Halmashauri za Miji na Mabaraza ya Miji pia yamehusika.

Mhe. Hamada Abdalla na Mhe. Mgeni Hassan Juma, pia, wanaulizia umuhimu wa ujenzi wa vituo vya daladala hasa kwa barabara mpya, jibu lake ni hilo hilo kwamba wahusika watakuwa wanashughulikia kutafuta sehemu muafaka na zitajengewa ili zijulikane hasa sehemu ambazo daladala zitakuwa zinasimama.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa, alizungumzia magari yanayokwenda kazi, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa kwamba, Wizara itaweka matuta pamoja na alama zinazowaongoza madereva kupunguza mwendo katika sehemu zote zinazohitaji alama hizo.

Mhe. Salum Makame, anaulizia madereva wangapi wamepelekwa Mahakamani kwa kuendesha gari bila ya leseni, madereva kama hao waliopelekwa Mahakamani ni 25 na hatua zinachukuliwa kwa dereva yeyote ambaye anaendesha gari bila ya leseni akigunduliwa anachukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Salma Bilali, aliulizia ufinyu wa ofisi na upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi. Jibu lake ni kwamba kazi hiyo inaendelea na tunategemea kuimaliza katika mwaka huu wa 2016 mpaka 2017.

Mhe. Masoud Abdularahman na Mhe. Zaina Abdalla Salim, wamezungumzia madereva kuendesha gari bila ya leseni wakiwa na umri mdogo, ushauri huu uliotolewa ni kwamba wazee wote wahakikishie kwamba vijana wao waliokuwa chini ya miaka 18 na hawana leseni wasiwape gari kuendesha, lakini wakija wakiendesha gari vyombo vinavyohusika vitawachukulia hatua ipasavyo.

Mhe. Panya Ali Abdalla, alikuwa anataka kujua kuwekwa matuta na alama za barabarani, hilo nimekwisha lizungumza kwamba tunafanya hivyo maeneo yote ambayo tunahisi tunahitajia kufanya haya.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi, anazungumzia vituo vya daladala na magari, naamini kwamba hilo nimekwisha kulijibu kwa ukamilifu.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, nilitaka pia nimjibu Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf, alikuwa anataka kujua Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano haifutilii suala zima za matumizi mabaya ya mitandao, hilo nimelijibu na napenda kumhakikishia kwamba tunafuatilia tena kwa ukaribu sana kuhusu matumizi ya mitandao.

Mwisho, Mhe. Shadya Mohammed Suleiman na yeye alitaka kujua hili hilo tatizo la *Internet* katika taasisi za Serikali za Pemba. Hilo linashughulikiwa na shughuli hizo ambazo zinatolewa na *ZANTEL* kwa Serikali bila ya malipo zinahusika na Pemba pia.

Mhe. Omar Seif Abeid, alikuwa anazungumzia kwamba *ZANTEL* imekuwa na matatizo ya kutoa huduma za simu katika kiwango cha chini, hilo nimekwisha kulijibu na kwamba litatuliwa baada ya mitambo mipya kuletwa.

Mhe. Spika, hayo ndio yalikuwa masuala ambayo nilikuwa naamini niyajibu pembeni kwa sababu ni masuala ya sera, napenda kuwahakikishia Baraza lako tukufu kwamba Wizara hii itaendelea kufanya kazi zake na kutimiza wajibu wake kama kawaida, napenda kuwashukuru wote ambao wametuchangia. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mheshimiwa, amemaliza na hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hii hoja wanyanyue mikono yao, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa, kabla sijamwita tena Mhe. Waziri, naomba nitoe tangazo moja Waheshimiwa Wajumbe, kwamba lile zoezi la ujazaji wa fomu kwa ajili ya huduma ya Bima ya Afya lililoanza juzi siku ya Jumamosi, leo linaendelea katika chumba cha kamati namba mbili. Baada ya hapo sasa naoma nimwite Mhe. Waziri, ili aje atupe taarifa hapo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi,

Mawasiliano na Usafirishaji, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa Baraza lako tukufu limekaa kama kamati, lakini naomba tutengue kanuni ya tisini na nane (3) ili Wajumbe wapate nafasi zaidi kupiga buti katika vifungu ambavyo bado hawajaridhika, baada ya watatu kuongezeka naomba sana Mheshimiwa kwa sababu hii ni nafasi nyeti kabisa na Wizara ina mambo mengi halafu masuali mengi sana hayajajibiwa. (*Makofi*)

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa, nashukuru sana wazo lako zuri lakini sasa wasi wasi wangu kuna Wizara nyingi, kwa sababu tuna tatizo kubwa sana la muda, mimi ningeomba tungeendelea kufuata kanuni, twendani kwa mujibu wa kanuni, nitajabu kwa kadri itakavyokuwa kutoa nafasi kwa mgao ulio sawa, yaani mtu kama amepata mara mbili, tatu niweze kumpa mtu mwengine mpya ili na yeye aweze kutoa alilonalo.

Mnajua Waheshimiwa kwa sababu mliichangia hii Wizara na mambo mengi mliyaeleza, Waheshimiwa, wameyasikia na bahati nzuri Mhe. Naibu Waziri, amejitahidi sana kujibu lakini nina wasi wasi baadhi ya Waheshimiwa, walikuwa wanatoka nje, nilikuwa nikiangalia kwa makini sana wengine wanatoka nje wakati mambo yao yanajibiwa, kwa hivyo, tusitake kutumia nafasi hii ya kupitisha vifungu kuanzisha mjadala mpya tena itakuwa sio nzuri sana, nafikiri tuendeni kwa mujibu wa kanuni ili tuweze kumaliza na shughuli zetu ziweze kuendelea. Kwa maana hiyo Waheshimiwa, naomba tuendelee, Mhe. Simai, kuna.

Mhe. Simai Mohammed Said: Utaratibu kidogo, Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyozungumza, samahani kidogo, kumekuwa na tabia wakati nazungumza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, anakuwa ananiingilia. Hii ni mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, zungumza na mimi tu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati Waziri anatoa maelezo yake alizungumza kwa usia kabisa, alikiri kwamba Wizara hii inagusa

kila mwananchi, na ukiangalia kwa kweli hili fungu lililokuwepo kwa kweli utakuta hatuwatendei wananchi haki, tunakuomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, unachokifanya unaendeleza mjadala ambao nilikuwa nimeshautolea maamuzi na nadhani *issue* ndio hiyo hiyo ambayo Mhe. Abdalla Maulid Diwani, ameinyanyukia na ndio maana tulitoa siku ya Jumamosi ili muweze kuchangia hii Wizara makusudi kwa sababu inawagusa wananchi, bahati nzuri watu wengi sana ambao ni wafanyakazi pia siku ile wako majumbani, kwa hivyo, wamekusikieni, wasi wasi wenu mkubwa ni kusikika Waheshimiwa katika majimbo yenu, nina uhakika mmesikika vizuri sana, tuwachieni hii shughuli iendelee, tufuateni utaratibu, twenda kwa mujibu wa utaratibu, kwa mujibu wa kanuni hiyo hiyo 98(3).

Tutaendelea kwa utaratibu huo huo Waheshimiwa ili kuweza kuokoa muda, hatuna muda, na leo Wizara nyengine inatakiwa ije iwasilishe bajeti yake hapa, tunaendelea Waehshimiwa.

FUNGU P01 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Kifungu P0104	Idara ya Ujenzi	25,000,000
Kifungu P0106	Idara ya Usafiri na Leseni	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, haya ni Mapato, tuendelee.

Kifungu P0106	Idara ya Usafiri na Leseni	1,587,800,000
Kifungu P0109	Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe	150,000,000
	JUMLA KUU	**1,762,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu Vimepitishwa na Kamati ya Matumizi ya Baraza zima bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU P01 WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti: Bado waheshimiwa, naomba mukae.

Kifungu PP0101

Mhe. Mwenyekiti: Bado Waheshimiwa, naomba mukae, endelea.

Kifungu PP0101 Program kuu ya Miundombinu na Huduma
za usafiri wa Barabara
Kifungu P

Mhe. Mwenyekiti: Haya sasa tunaanza nitawaita watu watatu; Mheshimiwa, nitakupa nafasi ya kwanza, Mpakabasi nitakupa nafasi ya pili, na Mhe. Jaku, nitakupa nafasi ya tatu, nitakuongezea moja kwa sababu ya jinsia tu mtakuwa wanne.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti, kunipa fursa hii, mimi katika maelezo yangu nilipochangia hotuba hii, nilichangia juu ya suala zima la barabara ya Mpendae/Jang'ombe na nathubuku kusema kuna kiongozi alitoa zaidi ya shilingi milioni mia moja kuikarabati barabara ile, lakini katika maelezo yako Mheshimiwa, sijapata jibu, naomba unifahamishe nini kinachoendelea juu ya kadhia barabara ile ya Jang'ombe kwa sasa hivi ishakuwa haipitiki tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijibu nilijibu kwa ujumla kwamba, kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya 2014 ya Serikali za Mitaa, barabara hizi ni barabara ambazo ziko chini ya Wizara husika, na kama alikuwa anafuatilia vizuri wakati akiwasilisha kitabu cha bajeti hapa Mhe. Waziri, aliainisha barabara zote ambazo tayari zishafanyiwa upembuzi yakinifu, barabara ambazo zimejengwa, kweli ile barabara tumejenga sisi, lakini kwa mujibu wa sheria ile barabara tumeikabidhi kwa Wizara husika. Kwa hivyo, tukishaikabidhi barabara kwa Wizara husika maana yake Wizara husika ndio wana jukumu la kufanikisha hilo suali.

Tunachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mbunge, kwa pesa alizozitoa na mimi pia ni mdau wa barabara ile, sasa astahamili kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa, basi tutahakikisha ile barabara tunaitia lami pale ambapo pesa zitaruhusu ili wananchi tuwaondolee kero ya barabara kwisha, namuomba astahamili sana, najua ana uchungu, si barabara hiyo tu kuna barabara nyingi tu. Lakini ni sheria imepitishwa humu humu na Baraza la Wawakilishi tuikubali na sisi tuna jukumu la kutengeneza barabara kuu, wenyewe wanaita *Track Road* na hizo nyengine za ahadi za Rais kama nilivyosema mwanzo ndio zitatekelezwa.

Kwa hivyo, ndio zile barabara zote za Halmashauri nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, wazifuatilie kwa Wizara husika, ndio maana mimi sikutaka kuzitolea maelezo hapa, nimezungumza mwanzo kwamba ni Ibara ya 88 ndani

ya Ilani ya uchaguzi wa CCM inaonyesha barabara zote ambazo sisi tunatakiwa tuzijenge, na kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri, kinaonyesha barabara zote ambazo Mhe. Waziri wa Wizara husika Tawala na Idara za SMZ wanatakiwa wazijenge, ni kugawana madaraka.

Miundombinu tumepewa katika Wizara ya Fedha, wenyewe wanatuita UUB sisi tumepewa asilimia 85 ya Mfuko wa barabara wa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa sababu sisi tunatengeneza barabara kubwa, na Tawala za Mikoa wamepewa asilimia 15 kwa ajili ya hizi barabara, tumewaambia barabara ya Kilimani sasa hivi Mhe. Jazira, shahidi tumekwenda kutembelea inatiwa lami, Barabara yangu ya Jimbo la Malindi inatiwa lami, kazi hii hatufanyi sisi, wanafanya Tawala za Mikoa, tuwashukuru na zinatengenezwa barabara kwa mujibu wa mapato ya Halmashauri husika. Manispaa ya Mjini wana pesa nyingi zaidi ndio maana wanatia lami na tuwashajihishe sasa Manispaa nyengine, ndio maana zikawekwa Manispaa za Magharibi B na A ili wakusanye mapato zaidi hizi barabara tuzitengeneze.

Kwa hivyo, tutaitengeneza hii barabara kwa kushirikiana na Wizara husika wakati wa pesa utakaporuhusu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kweli anafanya kazi sana, nafurahi na utendaji wake wa kazi, lakini hata hiyo tulipopitisha Afisi ya Rais Tawala za Mikoa barabara ile haimo, sasa sijui ananambia Kiswahili gani kwamba itatengenezwa. Kwa upande wa barabara zilizozungumzwa katika Manispaa ya mjini ni barabara ya Kodongo Chekundu, Barabara ya Mpendae/Jang'ombe sijaiona, sasa naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomjibu hali ya kifedha ya nchi zote tunaijua, sisi nia yetu ni kutengeneza barabara zote ziwe nzuri, Serikali inataka mapato tunataka *terminal II* imalize kwa haraka, tunataka Mpigaduri imalize kwa haraka, ni kero ambazo tunazijua sisi, lakini 'kupanga ni kuchagua', ashukuru barabara yake ya Kidongo Chekundu imo katika bajeti hii, na ile barabara afadhali sasa hivi ina lami ya maji, tustahamili tunajua utaratibu, tutaangalia huo utaratibu pale pesa itakapokuwepo tutaichukulia hatua.

Mhe. Muwakilishi, namuomba sana, mimi ni mdau wa barabara ile pia natumia na barabara nyingi tu ambazo mimi nazijua lakini aturuhusu na akubali tu kwamba kila kitu kinakwenda kwa uwezo. Ahsante Mwnyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mheshimiwa, ni kweli anavyozungumza, lakini kumbuka kwamba barabara hii ilichangiwa pesa si chini ya shilingi milioni mia moja ambazo mtu mwenyewe kiongozi kajitolea, je, Serikali inaona tabu gani kum-*support* yule mtu kwa sababu sasa hivi barabara iko katika hali mbaya kabisa, si ya kujinasibu mtu na ukitizama kwamba barabara ile ni ahadi ya Rais, nakubali yote hayo ninayosema, kwa hivyo, aniahidi mimi ili iwe kauli ya Serikali pindi mwakani nitakapokuja niwe na nguvu za kuhoji tena.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti *concern* ya Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe Mhe Abdalla Maulid Diwani, Serikali inaifahamu na inaitambua na inaithamini, lakini nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu ya Serikali yaliyokuwa mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaelewa kama Serikali na tunampongeza sana Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mpendae kwa juhudi ambazo alizifanya za kazi za awali katika kuitengeneza barabara ya Mpendae/Jang'ombe. Na kwa sababu serikali ilitambua juhudi zile ndio maana ikachukua ahadi ya kusema kwamba palipobaki serikali itapamalizia. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Abdalla Diwani, hata kama barabara ile hakuiona katika bajeti yangu, lakini sisi kama serikali tunajenga barabara zile kupitia Mfuko wa Barabara. Na kama nilivyosema siku ya bajeti yangu tunachofanya sasa na Mfuko wa Barabara kuhakikisha kwamba tunazungumza na kuongeza *percentage* ile iliyopo ili tuweze kujenga barabara nyingi zaidi za mjini kuliko tunavyojenga sasa.

Sasa atukubalie kwamba hili jambo sisi kama serikali tunalichukua na tutakwenda kukaa na ndugu zetu wa Mfuko wa Barabara chini ya Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha anasikia, ili tuone ni namna gani tunaweza tukafanya kazi ya kuweza kukamilisha barabara ile kwa sababu sisi tusingependa zile nguvu zilizoekezwa zikaweza kupotea. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Abdalla Diwani, aturuhusu tuendelee ili atupe muda sasa badala ya kupoteza muda humu ndani, atupe muda tukakae serikalini tuone namna gani tunaweza tukaishughulikia barabara ile. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ningeshauri na yeye mwenyewe angeshirikishwa kwenye hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, tutakapokaa tutakaa *as* serikali, sasa kama tutaiachia jukumu kamati ya mawasiliano na ujenzi, mjumbe yeyote

anayo haki ya kushiriki katika mazungumzo ya kamati, lakini kwenye mazungumzo ya serikali ningekuomba sana Mhe. Mwenyekiti, atuachie serikali tuzungumze, halafu matokeo yake tutayaleta kwako Mhe. Spika, tumeamua nini, halafu kama Kamati inashughulikia, mjumbe sijui yuko kwenye kamati gani. Kama yuko kwenye kamati hiyo sawa, kama hayuko kwenye kamati hiyo utaratibu wa Baraza unaruhusu mjumbe kushiriki kwenye kikao cha kamati nyengine hata kama sio ile ambayo umemteua.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana pamoja na maelezo mazuri ya serikali, naweza kukubali lakini roho yangu kidogo imenyongeka. Nakubali lakini roho yangu imenyongeka.Tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri na nilikuwa nazungumzia kuhusu barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni juu ya wakati wanakarabati ujenzi na utunzaji wa miundombinu kwenye kifungu hiki, ni suala la *Fiber Optic* ambalo nililizungumzia linalotoka Mwanakwerekwe mpaka Fuoni ambalo limeharibika na kwa mujibu kutokana na mazingira yalivyo ule waya ulikuwa bado ni mpya, ni *Fiber Optic* bado ni mpya na kwa vile tayari ile *Fiber* inatumika kufanyia kazi kupeleka hizo huduma pamoja na taasisi nyengine ambazo serikali imeingia mkataba, je, ni kiasi cha gharama cha fedha wizara itatakiwa ilipe ili kutengeneza ule waya mpya na mbona hicho kiwango cha fedha katika mafungu ya Bajeti Kuu ya Serikali iloomba hilo fungu halipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Simai, kwamba serikali ina utaratibu wake na zile sehemu zote ambazo kama kunakuwa mkonga unaharibika sisi tunajua namna gani ya kufanya matengenezo hayo. Sasa mimi ninamuomba tu kama ana uthibitisho wa hicho kitu basi naomba atuletee kwa maandishi tulifanyie kazi hilo suala. Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri serikali imekiri kwamba, ule waya kweli kuna uharibifu umefanyika kutokana na utengenezaji. Suala ni kwamba ile *Fiber Optic* ni kiasi gani cha fedha kinatakiwa kulipwa ili kutengenezwa na kutokana na uharibifu uliotokezea ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa, kwa sababu mwisho wa siku ni Wizara hii husika ambayo iliyoweka hio *infrastructure* huo waya na wao wao ndio wanaotengeneza hiyo barabara. Sasa nataka kujua ni kiasi gani cha gharama cha fedha kitakiwa kulipwa na kwa sababu tangu barabara imeanza kujengwa ni muda sasa tangu ilipoanza kuchimbwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said, swali lake kama ifuatavyo:

Kwanza kama uharibifu umetokea ni lazima tukafanye tathmini ya uharibifu huo ili tuweze kujua gharama kamili ya ku-*replace*, kwa hivyo, atupe muda Mheshimiwa, tathmini ifanyike, lakini kutoiona bajeti kwa sababu ni kitu ambacho hatukukitarajia, ina maana kwamba baada ya kujua gharama kamili ya *replacement*, basi uko utaratibu ndani ya serikali wa kupata fedha hizo za *emergency* kwa ajili ya *replacement* ya *cable* hiyo. Lakini vile vile kazi hiyo itafanyika baada ya kukamilika ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, swali langu nililouliza kabla kuja nilitoa hizi taarifa tangu Ijumaa wakati Jumamosi ninachangia na niliomba kwanza ni gharama ya kiasi gani, hisia ninazozipata ni kwamba serikali haitaki kulipa gharana hapa ili nikajua ni kiasi gani, hicho ndio ninachokipata. Kwa sababu tangu hii barabara imeanza kutengenezwa ni karibu miezi 6 tangu imeharibika hii *Fiber* na tayari Kampuni za simu ambazo zinatumia hii *Network Fiber* wanaomba hii huduma ipate kuendelezwa kwa haraka. Sasa cha msingi ni kwamba kwa sababu ile *Fiber* ilikuwa ni mpya na wizara hii husika ndio wanaotengeneza hii barabara na wao ndio *responsible*, wanao-*keep clear* katika hili suala.

Mimi nataka kujua ni gharama gani zile pesa za wananchi zimetumika kuharibika kwa makusudi kutokana na ujenzi wa hii barabara ambapo hadi hivi sasa hii huduma imesimama na tayari Wizara ya Fedha waweze kutwambia ni kiasi gani hizo fedha pamoja na wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai, kama nimemsikia vizuri Mhe. Waziri wa Fedha, ni kwamba uwape muda waweze kufanya tathmini ili wapate tathmini halisi. Wewe ulipoliuliza hilo ninafikri kama ni kwenye mchango wa bajeti muda huu usingetosha kufanya hiyo tathmini ambayo inahitajika.Kwa hivyo, waruhusu waweze kufanya tathmini iliyokamilika kuhusiana na hiyo *cost* inayohitajika, halafu Mhe. Waziri wa Fedha kasema wanao utaratibu wakisha kuipata hiyo yapo mafungu yatakayoweza kutoa fedha hiyo ya dharura kuweza kutatua hili tatizo. Sijui hujafahamu wapi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipotoa hotuba yake hapa ya masuala ya fedha sikuona sehemu ya *emergency funds* ambazo zinasema kwanza pesa ambazo zimetajwa za vitu vya uzembe, yaani pesa za uzembe tuzichukulie, hazikuwepo katika fungu kama hilo. Hapa ni kwamba wizara inayohusika imejenga hii barabara na tayari wao ndio

walikuwa wametandika hii *Fiber Optic* na huu waya umeharibiwa kwa makusudi sasa na muda uliotumika ni muda wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Sehemu hiyo imeshafahamika, ninafikiri, hebu muwache Mhe. Waziri wa Fedha, akutosheleze.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza Mhe. Simai, akubali kwamba huo si uzembe. Katika ujenzi wowote unapotengeneza unaweza ukatokezea uharibifu, kwa hivyo, huo si uzembe na tunapotaka kujenga lazima saa nyengine uharibu, ni kitu cha kawaida. Lakini fedha hizi nilisema kuna utaratibu wa *emergency* na fedha hizi zinaweza zikatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na Mfuko Mkuu wa Serikali hizo ndio shughuli zake za *emergency*. Mbali ya shughuli nyengine lakini mambo ya dharura basi Mfuko Mkuu ndio utakaotufika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa na kwa roho safi, *issue* yangu mimi ni ndogo, kwanza nilikuwa nataka kujua fedha, haya twende mbele fedha hazipo, lakini wizara hii wakati inakwenda kutengeneza barabara walikuwa wanajua chini kuna *cable* mpya ya *Fiber* imetandikwa ambayo gharama yake ni dola 18,000,000. Sasa leo tunaambiwa kwamba serikali ilikuwa haitambui sio kwa sababu uzembe kama sio uzembe ni kitu gani, tuelezwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kujaribu kumsaidia Mhe. Simai.

La kwanza, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe, wenzangu kwamba tutambue hadhi na heshima ya chombo hiki na kauli zetu tuzipe uzito huo huo unaostahiki kwa mujibu wa chombo hiki.

Mhe. Simai, anazungumzia suala la kuharibika kwa *Fiber Optic* ni uzembe wa wizara, ama ni uzembe wa serikali. Kwa kweli hii si kauli nzuri, wala si kauli sahihi, naomba nimkumbushe Mhe. Simai, barabara husika ilikuwa na upana wa mita 6, maendeleo yanayofanywa sasa hivi na wizara ni kwenda katika barabara yenye upana wa mita 14, *twabaan*. Miundombinu ambayo anayoisema ilikuwa imejengwa mita 2 kutoka mita 6, maana yake ilikuwa mita 8 ya pale ambapo barabara ilikuwa na upana wa mita 6. Unapozichukua mita 8, unapoongeza mita nyengine 6 maana yake bila shaka yoyote kipande cha *Fiber Optic* kitakuwa katika eneo la barabara. Sasa ni kweli maendeleo ni kupanga na

kupanga ni kuchagua. Sisi tuliamua kupanga kwamba tuongeze upana wa barabara kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Hivyo hivyo, tuliamua kuwa na *Fiber Optic* kwa ajili ya mawasiliano ya nchi yetu. Nimuhakikishie Mhe. Simai, kwamba *concern* ya serikali, tunajua kwamba kuna wananchi wanapata tabu ya miundombinu ya maji, wanaendelea kutuvumilia tumalize ujenzi wa barabara, turejeshe huduma za maji ili uweze kupata maji ambayo yanamuwezesha binaadamu kuishi kwa kila siku, seuze huu mkonga ambao unahitaji mawasiliano.

Kwa hivyo, Mhe. Simai, nimuombe kwamba atambue uzito wa kauli yake anayoitoa, haina uzito wa kutaka kuwasaidia wananchi, ina uzito wa kutaka kuichonganisha serikali na wananchi wake. Sisi serikali tunalitambua kwamba tumejenga mkonga wa mawasiliano upo katika eneo la barabara, tumekusudia tukimaliza kujenga barabara mkonga wa mawasiliano tutaujenga na tutaurejesha kama zilivyo huduma za maji na umeme ili wananchi wetu waweze kufanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mjumbe, atuachie tukamilishe upitishaji wa bajeti hii wende wenzetu wakafanye kazi katika kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

TAARIFA

Mhe. Said Soud Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii napenda Mhe. Simai, asimame na afute kauli yake, kwa sababu kilichomleta hapa ni hiyo serikali anayosema 'zembe', afute kauli yake mara moja. Hatuna serikali zembe, tuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hakuna serikali zembe, hapa afute kauli yake mara moja.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani taarifa aliyokwishaitoa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, imetosha tu kuwa elimu kwa Mhe. Simai na ndio maana nilitaka tuendelee. Kwa hivyo, tusiende huko. Mheshimiwa, huwezi kuendelea kwa sababu ni zaidi ya mara tatu ushakizuia hiki kifungu, vyenginevyo, kama bado unayo tutapiga kura ambayo itakuwa sio nzuri. Naomba sasa nimwite Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana na nimpongeze Mhe. Waziri katika waziri anaechukua muda mfupi kujibu hizo hoja za wananchi katika chombo hiki, nimpongeze sana. Mhe. Mwenyekiti,

misemo haitukatazi katika Baraza letu 'umleavyo ndivyo akuavyo' na 'huruma hailei mwana'.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilikaribia kulia, *UUB* kitendo kinachofanyiwa, bajeti yao ya kutegemea shilingi mia kwa kutia mafuta hairidhishi, wana mashine nzito na wao kazi yao ku-*repair* barabara, lakini inafika wakati kuthubutu wakajenga barabara mpya kwa kweli hatuwatendei haki na barabara zote sisi Waheshimiwa, tunakuwa tunalalamika barabara mbovu, lakini kwa kweli hawatendewi haki. Kwa shilingi mia mpaka mtu akanunue mafuta kwa Mfuko wa Barabara, aa. Kwa vyombo vilivyoko pale, chombo kidogo cha mwanzo milioni mia sita au mia saba na vyombo hivyo ninafikiri tangu urembo ungali tunguja, wazee wetu wanavaa tunguja mashikioni ndio mpaka leo vyombo vile. Serikali inatoa kauli gani kuhusu bajeti ya wizara ile baada ya kutegemea njia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyojibu Mhe. Waziri, kwamba tunajua hali ya kifedha ilivyo ya serikali. Sisi tunajua kazi kubwa wanaifa *UUB* na tunajua kwamba wanahitaji vifaa vya kisasa kama zilivyo kampuni nyengine na tunamshukuru sana Mhe. Jaku na sisi hili suala lake linatuumiza na kweli tunawajali wafanyakazi wetu pamoja na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa. Na kama ukiangalia bajeti ya uzinduzi aliyoitoa Mhe. Rais, pia *concern* yake hivyo hivyo kwamba Wizara yetu hii lazima iwe na vifaa vya kisasa, sio hapo tu mpaka na Idara nyengine kama Karakana. Na sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tutahakikisha kwamba shauri lake tunalifanyia kazi na tunamuunga kwa hilo na tuko pamoja naye.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio majibu ya kisiasa, muda wote zile mashine tukenda kuziangalia kama Kamati ya Miundombinu ukiangalia utalia, kuna *low bed* kuna *scavater* kuna *roller*, wafanyakazi hali zao wako katika hatarishi, usalama wao mdogo. Halafu sisi huku tunalalamika barabara mbovu, barabara mbovu, kama hawakuwezeshwa hawa, yeye Naibu Waziri kaja juzi, Waziri kaja juzi lakini mambo hayo ni ya muda mrefu. Tangu yuko *comrade sir* Gavu, sasa ukija ukahoji humu unaambiwa unaidhalilisha serikali. Mimi Mhe. Simai, niko pamoja nae na kwa mujibu wa Katiba hii, mimi anambie tu lini angalau kufikiria kwa njia ile moja hawawezi kupata pesa kwa shilingi mia, barabara zitazidi kuwa mbovu tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuarifu kwamba sasa hivi wizara inaandaa mpango wake au muundo wa wizara na katika *concern* zetu pia tumeliangalia hili

tunataka idara zetu zote zifanye kazi kwa ufanisi na vile vile, pale ambavyo tutahisi kazi ukiwapa watu wengine tutafanya hivyo. Lakini ninamuhakikishia kwamba hiyo kazi tunaifanya sasa hivi baada ya muda hiyo kazi ikisha kukamilika itapelekwa sehemu husika na *UUB* nao watakuwa kama vile anavyotaka yeye. Lakini mimi ninamwambia hatujibu majibu hapa kisiasa, sisi huwa tunaongozwa kwa mujibu wa sheria zetu na vile vile, tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria na tunapokuja hapa tunasema kile ambacho tuna uhakika nacho, hatusemi kwa kufurahisha watu. Kwa sababu hili Baraza baadae litakuja kutuhukumu.

Kwa hivyo, mimi ninakubali *concern* yake na ninamuomba sana Mhe. Jaku, sisi tunaumwa zaidi kuliko anavyofikiria, hatulali tunaona kwamba kuna kweli uchakavu wa vifaa, tunaona ile kazi wanafanya katika mazingira magumu na hilo lote tumeliona, tunasubiri kwa sababu bajeti ya 2016/2017 itatue utatuzi wa mambo haya yanataka yaonekane kwamba yana kasoro. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, unajua kumetokeza mgogoro ndani na kwa mujibu wa barabara msimamizi ni yeye. Leo Manispaa yeye anataka barabara mpaka *parking* barabarani wanaweka, huu mgogoro wanasababisha nao vile vile, yeye ndie mwenye dhamana ya barabara kwa mujibu wa sheria. Yeye anasema hajibu kisiasa, kama hajibu kisiasa angetekeleza kwa vitendo wala asingeulizwa. Asikatae sisi nia yetu sio mbaya kuisemea serikali, yeye mengine hayaoni, sisi ndio tunaokosea tunamfahamisha njia hii, wala hatukuja kushindana hapa, tupo kwa niaba ya wananchi. Kwa hivyo, asitake kushindana, hakuna aliekuwa mbora hapa, aliekuwa mbora ni yule anaesujudiwa, *samia llahu liman hamida, rabana lakal hamdu, samawati wal ardhi* ndie aliekuwa mbora. Hapa tumekuja kuikosoa serikali, mawaziri hawaoni na wangeona, mtihani kabisa. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka kujua hatma ya barabara ya Mgelema. Kama nilivyosema katika Wilaya ya Chake Chake huku ndiko kunakotoka karafuu nyingi, kwa hivyo, katika majibu Mhe. Naibu Waziri, alipokua akijibu sikusikia kuhusu hatma ya barabara ya Mgelema.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema tulikuwa na muda mchache ilibidi kuna mambo mengine tuyapitie kwa haraka haraka. Lakini ni kweli, naomba radhi kwa hilo kwa sababu hii ni barabara muhimu na ni ahadi ya Rais, kuna barabara tatu ikiwa ya Mgelema na nyengine ya Tau pale ambazo Mhe. Rais, kwa sababu

kuna mazao ya karafuu mengi sana amezitaka tuzijenge. Moja tumeshaianza na hii ambayo yeye anaisema kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara tutahakikisha kwamba hii kazi tunaifanya ili kutimiza ile ahadi ya Mhe. Rais. Naomba atupe muda na kwa mashirikiano, kwa sababu kuna wizara tatu ambazo tumetakiwa tushirikiane katika hilo. Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara na sisi Wizara ya Ujenzi, ni ahadi ya Rais na tunalijua hilo ni tatizo, avute subra kwa kutukumbushia lakini hiyo kazi tutaifanya, kwa sababu mawaziri wote tunafanya kazi vizuri sana, tunashirikiana vizuri na hili *ZSTC* wamelichukua na wamelileta kwetu tutalifanyia kazi, awe na subra tu Mheshimiwa.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee, maana naamini hili ni jembe, muda mfupi tumeona kazi zake, kwa hiyo tuendelee.

Kifungu SP 01001	Programu Ndogo ya Ujenzi, Utunzaji na Matengenezo ya Barabara	1,244,538,000
Kifungu SP 010102		

Mhe. Mwenyekiti: Haya nitawaita watu watatu tena Mhe. Shamata, Mhe. Shihata na Mhe. Hassan *Diaspora*.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa lakini tatizo langu kubwa mimi jana sikuunga mkono bajeti hii. Lakini nilikuwa na tatizo au nilikuwa na maelezo ambayo sababu zangu zilikuwepo kwenye barabara, na ndio maana nilikuwa nanyanyuka kila wakati kutaka kuonekana waziri akumbuke, nilisema kwamba mimi kama hakuna yale ambayo nimeyasema barabara za Micheweni hazipitiki na ndiko ambako kunatoka maliasili nyingi, na haiwezekani kuonekana Naibu Waziri anasema *kupanga ni kuchagua*. Lakini hatimaye kule ambako zinatoka zile maliasili hakujengwi barabara, kunaenda kujengwa kwengine, nikatoa sababu kwamba mimi hili sitounga mkono bajeti hii.

Kwa hiyo, nadhani hiki kipengele kimepita lakini bado naendelea kuwa na msimamo huo huo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Micheweni ndipo ambapo mitambo yetu na vifaa vyetu ambavyo vinafanya kazi kule. Sasa mimi napenda kumuomba sana Mhe. Shamata kwamba suala lake hili tunalifanyia kazi, na kama tulivyoahidi

na tukazungumza naye tunatambua kama kule kuna Chuo cha Kiislamu ambacho mambo mengi yanafanyika kule ya shughuli za kisiasa na kijamii.

Katika kutilia mkazo basi tutahakikisha tunashirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa tunazingatia barabara zake zile katika mpango wetu. Namuomba sana Mhe. Shamata airuhusu bajeti yetu hii asizuie kifungu, lakini tunajua tatizo lake hilo na ndio yalipo maeneo huru na kwenye maeneo huru kunahitaji barabara za kisasa, hivyo tutalishughulikia. Kwa hiyo, tunamuomba atustahamilie na muda utaporuhusu namuhakikishia kwamba tutayafanyia kazi malalamiko yake na kero zake hasa kuhusu barabara ya Micheweni.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, mimi siwezi kuzuia fungu moja kwa moja, nilikuwa namuomba tu Mhe. Naibu Waziri awaambie wananchi wangu wasikie kwamba ni lini hiyo kazi itaanza katika ujenzi wa barabara hiyo, na mimi niridhike na baada ya hapo akishatoa tamko basi naweza nikamruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyojibiwa Mhe. Abdalla Diwani na Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa kuhusu barabara yake, basi tutakaa sisi na Mhe. Waziri kuangalia hili tatizo, na vile vile namuahidi kwamba hali ya kifedha itaporuhusu, kwa sababu hatutaki kutoa ahadi baadaye Baraza hili tukufu kama nilivyosema inabidi tuseme yale mambo ambayo tunaweza kuyatekeleza. Lakini tunachukua *concern* yake na tutaifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwamba Mhe. Naibu Waziri basi tuweke ahadi twende pamoja katika maeneo yale tukaione hiyo hali halisi ilivyo, na baada yake mimi niseme tu kwamba naruhusu, lakini pamoja na kuruhusu bado nina masikitiko. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Shamata namuelewa anavyowapenda sana wananchi wake hasa wa Jimbo la Micheweni. Nimekubali uamuzi wake huo na tuko tayari mara baada ya Ramadhani na sikukuu tutafuatana naye pamoja kwenda kuangalia hali hiyo na kuifanyia kazi.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa majibu yao mazuri

sana waliyojibu kwa upande wangu na kwa baadhi ya wengine. Lakini niseme tu kwamba leo hii ni bajeti tunatafuta utaratibu mzuri kwa ajili ya wananchi wetu, usafiri na usalama ni jambo moja zuri ili wananchi wetu kuwapatia usafiri katika maeneo yao.

Nataka kukwambia tu Mheshimiwa katika jibu lake hakunieleza, je, wizara, angalau pamoja na hili tunaambiwa iko katika Manispaa atanisaidia vipi kifusi katika maeneo yangu ili daladala hizo ziende vizuri, hasa huko Madina kwa sababu anapajua fika yeye huko kwahala.

Pia, njia ya Mshelishelini mpaka huku Taveta/Magirisi nao pia wana huduma mbaya, kwamba wananchi wanakosa raha ya kutembea katika nchi yao kwa ajili ya ukosefu wa usafiri bora. Anieleze hilo tu Mheshimiwa halafu tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Ali Suleiman (Shihata) kwa juhudi zake anazozionesha.

Hivi karibuni kule kulikuwa na wenyewe wanasema mambo haya ya mwenge na barabara ile ilikuwa haipitiki, lakini kwa juhudi zake na Halmashauri akachangia kiasi kikubwa cha pesa na sisi tukashirikiana naye mpaka sherehe zile za mwenge zikafanikisha.

Mimi napenda kumuahidi tu kama nilivyosema mwanzo Mhe. Mtumwa Peya ni shahidi barabara yake ile sasa hivi kuanzia Bumbwini Makoba kwenda mpaka mwisho kule kwa kupitia juhudi zake na zetu tunaitia kifusi na itaendelea kuwa vizuri na hii haijawahi kutokezea kwa kipindi kirefu. Hata wazee wenyewe hapo kabla mfano wa Bumbwini walikuwa hawataki ile tuwatilie kifusi, lakini sasa hivi wananchi wengi wamehamasika na wanajua nini maendeleo hasa ya hizi barabara zetu. Nachukua ahadi kwamba tutaenda na tutashirikiana naye katika kumuwekea kifusi barabara yake ile ili ipitike zaidi, kwa sababu ipo katika ilani yetu ile barabara, tunaijua wakati wowote tutaifanyia kazi, na ile ya Mshelishelini pia tushazungumza pamoja na Mbunge wake tutaifanyia kazi, na hata daraja analojenga Uzi pia ametushirikisha sisi nampongeza kwa hilo.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri hayo sina tatizo naomba Mwenyezi Mungu atujaalie serikali yetu tupate fedha ili tufanye kazi. Tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh (*Diaspora*): Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake makini na yaliyopangika. Mimi Mheshimiwa kama nilivyosema nilipokuwa nachangia kwamba barabara ya Hawaii ina agizo la Rais na agizo ni sheria, na huu ni mwaka wa tatu na nusu haijatengenezwa, wananchi wangu wa Welezo upande wa Hawaii wanaisema vibaya serikali dhidi ya kutotekeleza agizo la Rais.

Sasa ninaumia mimi kama Mwakilishi wao kuona wananchi wanasema vibaya serikali inayoongozwa na Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pia yameshaanza kunikuta na mimi. Sasa nauliza nipewe majibu yaliyokuwa ya kimapinduzi, lini barabara yenye agizo la Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itajengwa. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti: Moja tu Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nakuomba kwa heshima na taadhima hiyo hiyo barabara.

Pili, barabara ya Fuoni nilisema iwekwe mipindo ya kuegesha magari kama daladala, ili tuepuke ajali. Leo hii barabara yangu ya *Mkapa road* kila siku ina ajali ili ile barabara iwe na vigezo kama alivyovisema Mhe. Naibu Waziri, barabara ya kimataifa, haitokuwa ya kimataifa ile pasi na viegesho vya kusimama daladala.

Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi tusije tukajenga barabara haina maegesho ya kusimama daladala, halafu tukaja tukatumia tena pesa za wanyonge kuja kufanya hayo, na tukija kuyasema tutakuja kuambiwa tuombe radhi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hili la pili lichukueni tu kama agizo mlifanyie kazi, mjibu hilo la mwanzo tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nitamuomba Mhe. Hassan akubali kwamba sisi huwa hatupendi na inatuuma sana kwamba agizo la Mhe. Rais tusitekeleze.

Ni kweli ilikuwa agizo hilo tokea la Rais mstaafu na tutahakikisha kwamba tunalifanyia kazi, lakini pale tu hali ya fedha itaporuhusu. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hiki ni kikao kitukufu na adhimu, kuchukua ahadi ambayo huna uhakika nayo baadae hawa Wawakilishi watakuja kutuuliza. Kwa hiyo, namuomba sana kama alivyokuwa mwana Mapinduzi basi aamini na sisi

wizara yetu kuna wana Mapinduzi wengi tu, tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba barabara ile tunaifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili linajibika katika barabara ile kuna vituo vya kisasa vitano kila upande, ambavyo vyote vitakuwa kumi, tumejitayarisha kuvijenga katika barabara ile hatutaki kuona kwamba wananchi wetu wanapata tatizo lolote. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Naibu Waziri ni *comrade*, mwenzetu, hodari lakini bado aniambie atakuja kuitengeneza ili wananchi wasikie, leo nipite kule kwenye jimbo langu nikiwa *hero*, ndio ninalolitaka mimi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na ahadi mimi na Mhe. Mwakilishi ya kwenda kuiangalia hii barabara, lakini yeye mwenyewe anajua kwamba tulitingwa na mambo. Kama tulivyosema kwamba nilimuomba kama siku tatu kabla akaniambia tuache kwanza, na kweli mimi namuhakikishia tutakwenda kuangalia, na sasa ile barabara mimi naijua kwa sababu jana kwa bahati nzuri nilipita barabara nyingi za kule kabla ya kuja huku mimi na dereva wangu, barabara ile kama ilivyokuwa ya Fuoni/Mwera imeharibika kutokana na mvua.

Sasa katika kuchukua hatua za mwanzo tutaifanyia marekebisho ya sehemu korofi ili ile barabara ipitike wakati wote kabla ya hayo matayarisho makubwa ya kuitengeneza ile barabara. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* nampenda sana Mhe. Naibu Waziri asiniambie leo wala asiniambie kesho, lakini nataka kauli yake tunakuja kutekeleza agizo la Rais. Hapo tu ndio ninapotaka mimi, leo nitapokwenda jimboni kwangu mimi nitapita vizuri, agizo la Rais litakuja kutekelezwa. Hivyo tu ndio ninavyotaka mimi, asiniambie kwamba muda na nini, anikubalie tu nakuja kutekeleza agizo la Rais, mimi nitakuwa niko sawa tu hata kama sio leo, hata kama si kesho. Lakini kauli itakuwa imetolewa katika chombo hiki kitukufu, chombo cha wananchi, watu wote wanachokisikia kauli na namuamini, Muislamu, amefunga basi atakuja kuitekeleza kama sio leo kesho. Lakini ataweza kusema kwamba nakuja kutekeleza agizo la Rais, ndio ninalolitaka mimi Mhe. Mwenyekiti. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo namjua ni jembe mkubwa sana Mhe.

Mwakilishi wetu, na anaumwa na wananchi wake na yeye anatokana na mishipa ya wakulima na wakwezi wa nchi hii na wafanyakazi.

Napenda kulitumia Baraza lako hili tukufu kumuahidi kwamba mimi nitakwenda naye nitaangalia barabara ile, nitaangalia tathmini, je, ni kiasi gani kinataka cha kutengeneza barabara ile.

Baada ya hapo ndio nitakaa na wataalamu wangu, na kupitia wizara nyengine ya Tawala za Mikoa ili hiyo ahadi ya kuwaambia wananchi lini tutaitekeleza. Lakini mimi namuomba sana barabara zote tunataka tuzitengeneze, lakini hali ya fedha inaporuhusu sisi tunataka kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na barabara.

Kwa hiyo, nisimwambie lini, lakini nimwambie mara tu tutapokwenda kuifanyia tathmini na pesa itapopatikana tutamtengenezea anikubalie kwa hilo, lakini wananchi wake wamemsikia kwamba yeye ni mpiganaji mzuri, anatetea maslahi yao na yeye nitamshauri vile vile kwa kuanzia kama walivyoanzia wenzake, basi anaweza akachangia mafuta kwa kusafisha zile sehemu ambazo yeye anaona ziko tofauti.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru mimi niko tayari kuchangia chochote kauli yako umezunguka sana lakini kidogo kasema atatengeneza, wananchi wamesikia, watu wote wamesikia, na hiyo kauli leo siku ya Ramadhani naomba sana apite yeye ni jembe, najua ataweza kufanya. Ahsante.

Kifungu SP 010102	Programu Ndogo ya Usimamizi ya Usafiri wa Barabara	561,430,000
Kifungu PP 0102	Programu Kuu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi	
Kifungu SP 010201		

Mhe. Mwenyekiti: Nimemuona kama Mhe. Zaina ndiye eeh. Aaah! *Okay*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile hoja ni mbili nafikiri niko peke yangu nitatumia hoja mbili…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa itabidi uendelee kustahamili kwa sababu hii ni PP 0102, wewe unatakiwa uhoji kwenye SP 01…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni 0201.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! Bado hatujafika huko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Umeitaja Mheshimiwa SP 010…

Mhe. Mwenyekiti: Ni PP 0102, na bado hata kuihoji pia haijawahi kuhojiwa wewe umesimama, naomba ukae. Tuendelee.

Kifungu PP 0102 Programu Kuu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi
Kifungu SP 01

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hapo pako sawa, tena nitaanza kwa Mhe. Miraji, Mhe. Panya halafu nitamalizia kwa Mhe. Jaku.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niipongeze sana serikali kwa nia njema ya kuwatumikia wananchi wake.
La pili serikali hii hii yenye nia ya kutumbua majipu pale yatakapotokezea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Niliuliza kuhusu Bodi ya Wakandarasi, nikajibiwa kwa kitu kidogo tu kuonekana Bodi kweli Mwenyekiti amepatikana, Wajumbe wako njiani watachaguliwa. Sawa, lakini nikauliza ni kiasi gani cha fedha ambazo zimepatikana na bodi hii kwenye *class* "A" ya *civil*, class "A" ya *building* tokea kuanzishwa kwa bodi hii.

La pili pia katika mchango wangu nikauliza wamefanyiwa *auditing* lini ya kujua mapato na matumizi katika eneo hili, kwenye mchangio wangu. Pia nikaendelea katika mchango kutaka…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoji jambo moja tu ili uwape nafasi na wale wengine niliowataja waweze kuwasilisha.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Suala langu tokea kuanzishwa kwa Bodi hii na kupitia *class* "A" ya *civil* na *building* bodi imepata kiasi gani na zimeingia kwenye mfuko gani wa serikali kuu, wa bodi au mfuko wa idara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hivi sasa hizi pesa zinaingia katika mfuko wa bodi, isipokuwa hivi sasa kuna mazungumzo na Wizara ya Fedha katika utaratibu mzima kuhusu hizi fedha ziingie katika Mfuko wa Hazina. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hajanijibu vizuri nataka kujua tokea ianzishwe bodi hii imeingiza kiasi gani cha fedha, maana hizi fedha za wananchi, na kwenye *class* hizi zilizotoka *class* "A" na *civil* wazitaje ngapi kwa sababu viwango vyako tumeviweka katika sheria yetu.

Sasa aniambie kwa ufasaha maeneo haya mawili ambayo nimeyahoji ili wananchi wajue pale sisi tunaingiza kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hili suala la kitakwimu sana lakini ngojea tumsikilize waziri pengine majibu anayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema hili suala ni la kitakwimu, na huwa hatupendi hapa tukaleta takwimu ambazo si za uhakika. Kwa hiyo, nitalijibu kimaandishi ili apate kuridhika na Baraza hili lipate ufafanuzi zaidi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilisema mwanzo kuwa serikali hii ina nia njema ya kushughulikia wananchi wake, na nikasema yatapotokezea majipu imeahidi kuyatumbua. Nimechangia juzi hili, leo kuwa hizo takwimu hazijapatikana mpaka dakika hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba pamoja na kuwa suala la kitakwimu lakini siku moja nzima takwimu hiyo serikali hii inashindwa kupata. Mimi hili naendelea kuzuia bora tupige kura kama kuna watu ambao hawana nia thabiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea kuzuia mpaka nipate *figure*, na kama kuna watu hawana nia thabiti ya utumbuaji wa majipu katika hili nitawaona leo. Lazima serikali tufike pahala tulinde hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahitaji fedha ambazo zimepatikana katika bodi hii na kwa kuwa nimeuliza juzi muda wa kutosha ulipatikana, mimi naendelea kuzuia fungu na natoa shilingi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabla ya

kujibu nimuombe sana Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chumbuni abadilishe dhamira yake tusifike pahali pa kupiga kura.

Ni kweli *concern* yake kwamba aliuliza juzi kwa maana ya kwamba siku ya Jumamosi, na ni kweli alihitaji kutaka kujua takwimu halisi ya mapato ambayo yamepatikana kutokana na jambo hili, suala la leseni na wakandarasi. Lakini nimkumbushe tu Mhe. Miraji kwamba Jumapili hakukuwa na ofisi na jambo lenyewe lilihitaji *intervention* ya wizara, kwa maana kwamba Wizara husika ya Ujenzi ifanye *intervention* na Wizara ya Fedha ambao wao ndio wahusika wanaweka zile takwimu, na sote tunajua utaratibu wa serikali kwamba fedha zinakusanywa *center* moja na serikali; kwa hiyo nimuombe tu Mhe.Miraji atusaidie, kwa maana ya kwanza akamate kauli ya Waziri kwamba atapatiwa majibu yake hayo kwa njia ya maandishi ambayo yatakuwa yamehakikiwa yana uthibiti kulikoni kutaka sasa hivi alazimishe kupewa takwimu ambazo zinawezekana zikapotosha Baraza hili na zikapotosha wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba tu nimuombe Mhe. Miraji abadilishe dhamira yake.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, nimehisi kama, samahani Mhe. Waziri ulikuwa na kitu cha ziada sijui, nilihisi kama mtu anataka kunyanyuka hapo, haya Mhe.Miraji.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri Issa Gavu kwa nasaha zake kwangu na kwa Baraza hili. Nishamkubalia ila naomba sitazuia hili wala hiyo shilingi yangu nimeiondoa. Ila naomba Mhe. Waziri anijibu kwa maandishi kwa uhalisia lakini pia ajue anayemjibu ni Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, naomba tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya majibu ambayo ameendelea kutujibu, kwa kweli tunaridhika lakini kwa kuwa bado tunahitaji kuelewa mambo mengine inatubidi tuulize.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia niliuliza majengo mawili; niliuliza jengo lile la treni pale lakini niliuliza jengo la maendeleo ambalo liko Kengeja. Mimi nilikuwa Mjumbe wa kamati hii kipindi kilichopita, hilo jengo lilikuwa lina hali mbaya na lilikuwa likitengewa fedha lakini zilikuwa haziingizwi zikaweza kurekebishwa lile jengo. Nilikuwa ninaomba niulize jengo lile limefikia wapi kwa sababu jengo lilikuwa bovu na watu wanaendelea kuishi mule ili tusije tukawaumiza watu wetu, serikali imechukua hatua gani juu ya jengo lile la Kengeja kulifanyia matengenezo ili watu waendelee kuwa salama, Mheshimiwa naomba majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Panya swali lake hili kuhusu majengo yale ya Kengeja.

Ni kweli sisi wenyewe tulienda na Mhe. Waziri na timu yetu yote ya wizara, kwenda kutembelea lile jengo la Michenzani la maendeleo la Kengeja, na tumelikuta katika hali mbaya ya kusikitisha sana, na kinachonisikitisha kwamba vipi wananchi wenyewe pia wanashindwa kulitunza lile jengo, jengo lile halina umeme, halina maji, hata vyoo vyake viko katika hali mbaya sana, hali hiyo pia iko katika baadhi ya majengo ya Wete pale inatusikitisha sana, kwamba mtu unakaa katika nyumba yako mwenyewe zile huduma za dharura pia huzitunzi.

Sisi kwa kutumia Shirika tumejipanga kwamba kuhakikisha haya majengo yetu sisi tunayafanyia ukarabati, na Mhe. Simai hapa alitoa wazo zuri tu juzi kwamba tuliendeshe hili shirika kimapato na vile vile tujifunze kwa wenzetu, wataalamu wetu wameshaenda kujifunza kwa shirika la nyumba la Tanzania Bara, na hivi sasa pia wapo katika mpango wa kwenda katika nchi tafauti ili kutumia uzoefu wa wenzetu katika kuhakikisha kwamba yale majengo tunayaenzi na kumuenzi Mzee wetu Abeid Amani Karume, kwani kajenga kwa ajili ya wananchi wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tunalolipata pale wanasema kwamba hali ya uwezo hawana. Tuliwapa mfano sisi kwamba nyinyi mmepewa majumba yana kila huduma, leo hii mnasema hata kufanyiwa ukarabati hamtaweza kulipia, tunawafahamisha na tutakaa nao tena kuwapa uelewa zaidi ya nini jengo na wao wawe tayari kutuchangia kwa ajili tu katika kuhakikisha yale majengo tunaendelea kuyatunza ili kumuenzi Mzee wetu Abeid Amani Karume.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe msisitizo kwa Mhe. Waziri kwa sababu jirani aliyekaa naye pale jirani yao ni Waziri wa Afya, kwenye afya kuna msemo 'kinga ni bora kuliko tiba', sasa pale jengo lile wananchi wamo wanaishi na bado linaendelea kutumika, namuomba sana Mhe. Waziri ajue kama kulifanyia marekebisho ni vizuri kuliko likaja likaleta maafa tukapoteza wananchi wetu pale, Mheshimiwa tuendelee napenda msisitizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja yangu ilikuwa barabara ya Mkunazini kuelekea Mji Mkongwe na uzuri Naibu Waziri ndio wapiga kura wake. Sasa kama atatengeneza siasa alokuwa kasema hajibu kisiasa, sasa sijui atajibu kiufundi gani. Tunataka kujua Mamlaka ya Mji Mkongwe barabara ile wamefunga kwa kigezo gani, *power* hiyo wameipata

wapi, uwezo huo wana mamlaka gani kufunga barabara ile, na kwa mujibu wa sheria kwanza kabla ya kufunga barabara ile wakae na Bodi ya Barabara halafu ndio wakae wafike pahali. Nataka maelezo hayo, kwa nini wakafunga barabara ile, watu wanateseka wengine viwete, wengine vilema wanataka kwenda skuli, wengine jua wengine mvua na kipande kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Jaku kwamba kwa mujibu wa *Cap* 134 na marekebisho yake, kwamba Waziri kisheria anao uwezo wa kuangalia barabara ipi kwa maslahi ya wananchi akaifunga au akataka ifanyike katika hatua gani. Vile vile Mhe. Waziri ana uwezo wa kutaja sehemu, mfano kasema hii hifadhi ya barabara kisheria ndio walipitisha wenyewe hapa akiwemo Mhe. Jaku, na kuangalia nilimwambia pale kabla kwamba watu wa hifadhi ya Mji Mkongwe wamelalamikiwa sana na *UNESCO*, kiasi ya Mji Mkongwe wetu kuingizwa katika hatari ya kunyimwa nafasi hiyo adhimu, ambayo inatusaidia sana katika kuitangaza Zanzibar kiutalii, wametutaka kwamba tupunguze msongamano wa magari ndani ya Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku namuomba sana akubaliane na sisi kwamba tulolifanya pale ni la nia nzuri, na si kwamba watu hawaruhusiwi kwenda, watu wanaruhusiwa kutumia kwa kibali maalum hasa wale wananchi wa kule, watu wanaokwenda kufanya ibada, watu wanaotumia *CRDB Bank* na mambo mengine. Kwa hiyo ile imefungwa lakini haikufungwa rasmi moja kwa moja bali imetolewa vibali. Sasa namuomba Mhe. Jaku akubaliane na sisi kwamba urithi wa Mji Mkongwe ni muhimu sana kwetu, na mimi ikiwa kama Mwakilishi wa jimbo lile nitafurahi kwamba ule mji wangu ukiwa unaendelea kutangazwa kila siku duniani, kwamba ni katika mojawapo ya miji yenye hifadhi katika Afrika na ni miji michache tu.

Kwa hiyo Mhe. Jaku kwa hili aniangalie na mimi kama ni Mwakilishi kwamba nimelichukulia hili ni suala kubwa, lakini kwa vile vile nikiangalia maslahi ya nchi na serikali na wananchi akubaliane na sisi kwamba tusiendelee kuondoshwa katika hii hifadhi ya Mji Mkongwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri huu ni mwezi mtukufu wa ramadhani, na mimi kwa hili nimejipanga nafikiri sheria huna mimi nimekuja nayo na nitakusomea; Mhe. Mahmoud Thabit Kombo utamtafsiria pengine. *"A Minister may, by order published in the Gazette restrict the use of the road on one way traffic, either permanently or such as period as may be certified on such order*". Hiyo ndiyo kanuni na imesainiwa na Khamis Juma Chande Katibu wa enzi hizo, hii ndio barua kama hana.

Mamlaka ya Mji Mkongwe hana mamlaka ya kufunga barabara ile, walikuwa wakae na Bodi ya Mamlaka ifike na tena sheria itangazwe kwenye Gazeti aje anioneshe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe.Jaku amekwambia waziri anao uwezo huo sio mamlaka waziri, waziri ndio ana mamlaka hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sisi tumefunga, ile barabara hakufunga waziri, huyu hapa, barabara imefungwa na Mji Mkongwe, na Mji Mkongwe hauna mamlaka ya kufunga barabara, sheria hii hapa Mheshimiwa ninayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuendelea kutoa mchango wangu katika masuala mazima ambayo yanaendelea katika Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niendelee ku-*furnish* yale maelezo ambayo aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri, kuhusiana na suala zima la mamlaka husika ya Mji Mkongwe lakini mamlaka husika ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jaku amekuja na sheria, na mimi nimuombe tu aende akasome Sheria nambari 3 ya mwaka 1994, sheria ya Mji Mkongwe, aende akasome ataona mamlaka ambayo amepewa Mji Mkongwe, miongoni mwao ni jambo ambalo limechukua muda mrefu, sheria ya Mji Mkongwe inakataza kuingia Mji Mkongwe gari linalozidi tani mbili, sasa muda mrefu sana serikali ilikuwa tumekaa kimya tunaendelea kutaka kuona hili wenzetu ifike pahali tuweze kuzoea hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili Mhe. Waziri ameeleza pale *Cap* 154 tumefanya marekebisho sote mashahidi hapa mwaka 2013 kuhusiana na suala zima la usimamizi na uendelezaji wa barabara.

Lakini pia Mhe. Jaku nimuombe akasome sheria nambari 7 ya mwaka 2003 sheria hii imempa mamlaka ya wazi, waziri anayesimamia masuala ya usafiri na barabara kwa maana mamlaka ya kufunga barabara, ana mamlaka ya kufanya *no entry*, kwa hiyo nimuombe kwa kuwa bahati imeangukia mamlaka haya ya Mji Mkongwe yameunganishwa mmoja mwenye mamlaka ya kusimamia barabara sioni kama kuna mantiki au hoja ya Mhe. Jaku ya kuja kuuliza swali hili. Nimuombe sana Mhe. Jaku arudi akazipitie tena sheria

ambazo amesoma *either* kwa kuelewa au kwa kufundishwa, lakini akasome sheria nambari tatu ya 1994 itamuelekeza, akasome sheria *Cap* 154 itamuelekeza na akasome sheria nambari 7 ya 2003 itamtosha.

Kwa hiyo, kuendelea kubaki hapa kuhoji suala la mamlaka ya Mji Mkongwe, suala la ufungaji wa barabara sidhani kama atatutendea haki, na sababu za kufunga zimeelezwa kwamba sote tunajua mji wetu unafanya shughuli gani sasa hivi, mantiki ya kufunga imeelezwa, sasa kuja kuhoji hapa kwa kuwa suala lake la msingi lilihoji na suala la mamlaka ya wizara ama mamlaka, mamlaka kufunga suala la barabara hii, naamini kwamba sheria zetu ziko wazi wala hatuna haja ya kupoteza muda kwenye suala hili. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub*:* Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna sheria ya ubaguzi ya Afrika ya Kusini maana yake wanaita *apartheid* na sisi hapa kuna sheria, katiba na kanuni, sheria ndio kubwa kuliko kitu chochote.

Sasa Naibu Waziri labda skuli alikuwa akinipakia mimi kwenye baskeli akanipeleka nilikuwa sijui skuli, sasa anazungumza kitu gani, mimi simfahamu, sheria

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:Mimi aniletee sheria yake iko wapi, mamlaka ya Mji Mkongwe, barabara imefungwa kabla hapajawa na waziri, waziri huyu hapa tukatie udhu mimi, sasa hivi akamate msahafu na yeye akamate msahafu, barabara imefungwa na Mji Mkongwe, mimi niko tayari kukaa itikafu kwa hili, yuko tayari kukaa itikafu yule, tusifike pahali tukahangaisha wananchi. Mheshimiwa ndio yale tunasema historia isije ikajirudia, tupige kura nitoke tuliachie basi, lakini ni uongo, nasema tena ni uongo

Mhe. Mwenyekiti: Basi naomba niwahoji. Waheshimiwa

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, la kwanza namuomba sana Mhe. Jaku mimi namuheshimu...
Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae, zima hiyo *microphone* yako. Kifungu hichi kinakubaliwa.
Wajumbe: Ndiyo!

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu ASP 010201 Programu Ndogo ya Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi 372,165,000

Kifungu ASP

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, langu ni dogo kwa nia njema kabisa. Wakati ninachangia na nilipata majibu lakini Mhe. Waziri alipojibu suala langu la Ngome Kongwe (*Old Fort)* ambayo ataendelea kulisimamia na kulienzi, lakini kwa ninavyofahamu mimi Ngome Kongwe ndani ile ndani kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo ni Wizara ya Habari, Utalii na Michezo ambayo imekodisha maduka ndani na fedha zinazopatikana kutokana na ile kodi zinaingia moja kwa moja katika wizara husika zikisimamiwa chini ya Mkurugenzi wa *Director of Antiquities.*

Swali ni kwamba ni wizara ipi itakuwa ni *responsible* inayosimamia katika kulilinda, kulihifadhi na kuhakikisha kwamba lile jengo la Ngome Kongwe linakuwa salama?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema yale majengo yote tulizungumza mwanzo yapo katika uhifadhi wa Mji Mkongwe, lakini kwa jengo lile la Ngome Kongwe liko chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Nashukuru hilo. Mimi ninachokizungumza ni kwamba kwa kuwa mamlaka ipo chini ya wizara yake, na hili jengo alilizungumza kwa hisia kabisa ni katika majengo ambayo yako katika hadhi ya juu kabisa katika *heritage*.

Swali ni kwamba, nimeuliza swali langu nililouliza narudia tena pale pale, kwa kuwa zile fedha ukodishwaji wake zinaingia katika Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na katika miaka yote lile jengo linavyotumika kwa uhakika hakuna matengenezo yanayofanyika katika kuhakikisha kwamba suala la kulihifadhi kutokana na mazingira yake ya ndani sio ya nje kama alivyoongea na yeye. Ni njia gani atakayotumia sasa kuhakikisha kwamba yale mapato ya ndani yanayopatikana yanatumika moja kwa moja katika kuliendeleza lile jengo, kwa sababu kodi inayopatikana ndani watu wanakodi maduka, kuna huduma zinatolewa ndani lakini matengenezo hayapo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa.

La pili napenda kumfahamisha Mhe. Simai, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu kwamba mapato yanasimamiwa na kukusanywa kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, lakini mapato yale yanaingia katika mfuko mkuu wa Hazina, na mfuko mkuu wa Hazina ndio unagawanya yale mapato haya yaingie Wizara ya Ujenzi, haya yarudie Wizara ya habari, haya yaingie wizara nyengine kwa mujibu wa kazi na bajeti hii ambayo tunaipitisha hapa leo.

Mhe. Mwenyekiti, mujue napenda nimfahamishe wazi kwamba mapato yale sio kwamba yanaweza yakakusanywa kwa wingi wake yakaweza kutengeneza lile jengo, bado inabidi turejee kwenye vifungu vinavyoweza kuelekezwa kwenye mamlaka husika ya kutengeneza lile jengo, na mamlaka husika ya kutengeneza majengo yote yaliyokuwa kwenye hifadhi ni mamlaka ya Mji Mkongwe kutokana na zile taratibu za *UNESCO* ambazo wanaziagizia. Hivyo basi jengo lile bado litabakia katika mamlaka ya kutengenezwa na Mji Mkongwe kwa mujibu wa hifadhi zake, na mapato yataendelea kukusanywa na Wizara ya Habari na kupelekwa mfuko mkuu Hazina ambao ndio watagawa hayo mapato.

Mhe. Simai Mohamed Said: Kwa nia njema kabisa Mhe. Mwenyekiti, suala ninalozungumza hapa sijui kama limefahamika, kwamba lile jengo limekuwa *classified* na mamlaka ya hifadhi ya maendeleo ya Mji Mkongwe ni kwamba katika majengo yenye hadhi ya juu, lakini pia hili jengo linaingiza mapato mule ndani na mazingira yake ya ndani yanahitaji kukarabatiwa, sasa hivi ni miaka mingi, sitaki kuingilia kwa undani kabisa nikazungumza maana yake vipi na vipi. Suala ni kwamba hapa ikiwa hili jengo lina umuhimu kiasi hicho na linaingiza mapato yenye nambari moja, tumeangalia kwenye bajeti hapa ni kiasi gani, sasa Mhe. Waziri atwambie atafanya mpango gani kuhakikisha hili jengo sasa linarudishwa katika hadhi yake hasa mazingira ya ndani sio mazingira ya nje, mazingira ya nje na ya ndani ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema kwamba lile jengo liko katika majengo ya uhifadhi wa hali ya juu sana, kwa hiyo sisi tunalichukulia suala lake vizuri sana, kwa sababu yeye pia alikuwa mdau wa *ZIFF*, namshukuru kwa hili, anajua nini kinachoendelea basi tutalifanyia kazi na atustahamilie kwa hilo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee kumpongeza sana Naibu Waziri na leo tumeona darasa kubwa leo kuwa Naibu

Waziri kila wakati anainuka yeye na nafikiri huku mbele itakuwa fundisho mawaziri wengine

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja yako usimsifu Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mheshimiwa, hoja yangu ni ndogo nafikiri hii Waziri atainuka mwenyewe ataijibu. Nilimpa barua maswali na majibu ya Baraza la Wawakilishi tarehe 16/4/2015 imeandikwa na Mhe.Mohammed Abood, "tafadhali barua hii nakuletea *Hansard* kwa majibu niliyoyatoa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi siku ya tarehe 25/5/2015 wakati nikijibu swali No. 49 Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, naomba uipokee na kuifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu za sheria zinazohusu ujenzi wa Mji Mkongwe".

Mhe. Waziri, mimi nafikiri dogo wala tusibishane, nambie lini nije tulimalize.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ndio nyanyuka Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, tumepokea na *In shaa Allah* tutalifanyia kazi baada ya kumaliza bajeti pia tuko pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri lakini ni suala la muda mrefu nitasubiri wakati wa bajeti, nimeshakaa karibu miaka miwili nitaendelea kustahamili. Ahsante tuendelee.

Kifungu SP010202	Programu Ndogo ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe	360,900,000

Kifungu P0103 Programu Kuu ya Huduma za Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Kifungu SP010301

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kama kawaida. Mimi nimeuliza maswali manane yamejibiwa matatu na hayo matatu yenyewe yamekosewa, ningeomba nimuulize Mhe. Waziri maswali matatu tu ili niridhike.

Mhe. Mwenyekiti: Ni hoja moja tu Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu nilizungumzia suala la *internet*. Hili suala Mhe. Waziri alinijibu lakini mpaka lini Zanzibar tutangojea tuige watu kwenye sheria, kwamba labda Tanzania Bara wanayo sisi hatuna, huyu kafanya hivi na sisi tufanye, hili suala Rais anatukanwa kila siku kwenye mtandao, serikali inatukanwa kila siku na watu wanajulikana. Kwa sababu watapokwenda kwenye *internet* au kwenye ile *system* inayo uwezo wa kumuonesha mpaka aliyefanya vile ndani ya mita mbili akamkamata kwa *GPS* inavyofanya kazi. Lakini mpaka leo hatua hakuna, tunangojea sheria na hivi vitu vinaendelea.

Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri, ni lini hasa sheria hii atahakikisha inaingia japo kuwa sisi ndio wapitishaji, lakini kwa hivi sasa kwa kuwa hakuna sheria ni hatua gani stahiki zinachukuliwa kwa wale wanaotukana viongozi na serikali pamoja na chama. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bado sijamaliza, vile vile barabara yangu ya Chaani itazibwa lini.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ni hoja moja tu ya barabara haiingii hapo, angalia hiki kifungu tunachohoji Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Hilo nimempa *extra* anijibu ataziba lini. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema hili suala limepitishwa Bungeni ni suala la Muungano na sisi tunamaliza hatua kabla ya kuleta ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuridhiwa.

Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi karibuni kama alivyopewa katika hotuba ya Mhe. Rais ya uzinduzi aliyazungumzia hayo. Kwa hiyo, yeye yanamuuma na sisi yanatuuma, hivyo kikao kijacho tutaileta hiyo sheria kwa ajili ya kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi.

La pili, kama alivyosema tunashirikiana na Mamlaka ya *TCRA* kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanatumia vibaya hii mitandao basi tutawachukulia hatua pale ambapo tutathibitishwa hivyo au wale watu wa idara wanapopata taarifa hizo. Kwa hivyo, hili ni jambo gumu kama anavyosema huwezi kuingia moja kwa moja kwenye mtandao ukaanza kumchukulia mtu hatua, kuna taratibu zake zinatakiwa kufuatwa kwa sababu ni jambo la Muungano,

tunashirikiana nao kwa karibu na pale ambapo Mhe. Mwakilishi anahisi kuna mtu kakiuka sheria hizo za kutukana watu basi aje na tutamchukulia hatua.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi ya wizara na wizara, ninachoomba isilale, kila siku watatukanwa viongozi tu. Mimi kwanza nimeangalia mwenyewe binafsi hii *time* ni yao sio ya Mwakilishi. Wao wawe na watu maalum wanaoangalia kwenye mtandao wanaotukana wakakamatwe. Mimi nikiangalia anavyotukanwa Rais, serikali yetu naweza nikampiga mtu hata risasi nikiona mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimuulize tena mpaka lini atangojea hii sheria wakati sasa hivi watu wanazidi kutukana. Mimi nataka anambie wanaoanza kutukana kipindi chote mpaka hiyo sheria iletwe atawachukulia hatua gani, sio tukae tu hapa tufanye mambo ya kitoto. Wizara isilale ifanye kazi haraka iwezekanavyo isingojee sheria wakati mwengine ikamate.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nachukua ushauri wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, kwa hiyo wizara haitalala hapa ni kazi tu, tutayafanyia kazi na karibuni ataona matokeo yake.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Mwenyekiti, sawa nimemsikia sana lakini nitaomba aifanye hiyo kazi, kwa sababu tukiliachilia hili suala litakuja kufikia hatua anatukanwa kiongozi lakini mpaka itafikia siku anakuja kupigwa kibao kiongozi kama hatukulichukulia hatua. Namuomba sana tusiliachie hili suala. Tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nashukuru kunipa nafasi, pamoja na hayo napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza waziri kwa majibu yake mazuri aliyonipa wakati nilipochangia kwa maandishi.

Mimi nilitaka kujua huduma duni za *Zantel* zinazotolewa na akanijibu kwamba mwezi wa nane tunategemea watafunga mitambo mipya. Lakini ikumbukwe kuwa huduma za simu si kwa ajili ya kupiga simu na kupokea tu, *Zantel* inayo huduma nyingi ikiwa pamoja na huduma ilizokuwa ikitoa ya kununulia umeme kwenye *Ezy-Pesa*. Huduma hizi wamezikatisha na imeleta usumbufu mkubwa kwa wananchi hasa vijijini huko ukitilia maanani kwamba wananchi wetu wote vijijini sasa wanategemea huduma ya umeme. Sasa mimi napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri lini Shirika hili litarejesha huduma zile ili wananchi waendelee kupata huduma hiyo iwapunguzie usumbufu kupitia huduma ya *Easy Pesa* kupata kununua umeme. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kwanza kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa swali lake. Kama tujuavyo swali hili liliulizwa kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na likatolewa ufafanuzi kwamba wanaendelea na utaratibu wa kuagizia hicho kifaa na kitapokuja tu mara moja kuanzia mwezi wa Septemba basi tatizo hili litatatuliwa.

Kwa hiyo, tunamuomba astahamili na utapofika huo muda aje kutuulizia zaidi hilo suala, lakini nina hakika kwa sababu na sisi tunaipata hiyo kero sio kwa wananchi wa vijijini hata wa mjini vile vile kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba foleni inafika mpaka Kisonge kule, halitufurahishi jambo kama hilo. Serikali imechukua na italifanyia kazi kwa haraka ili kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri, haya tuendelee hakuna tatizo.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, ahsante, kama Ibara ya 88 ya Katiba yetu ya Zanzibar inavyotuelekeza juu ya wafanyakazi wetu pamoja na kifungu cha 66(b) kwa kutumia vikao vya Baraza na Kamati kulinda haki na maslahi ya wananchi, basi na mimi sina budi pia katika suala zima la *Fiber Optic part 2, part 1* ilikuwa *draw* hii ni *part 2* tunakwenda sasa.

Kwa kuwa wizara iliingia mkataba na Kampuni ya *Zantel* ambayo ule mkataba unatambuliwa kama ni mkataba wa *Zanzibar Terrestrial and Submarine Network***,** mkataba huu umefungwa zaidi ya miaka mitatu, na huu mkonga unaotumika sasa hivi ambao umetandikwa kote unatumika na makampuni ya simu pamoja na makampuni ya *ISP, Internet Services Providers* kutoa huduma ambazo zinawapatia *Zantel* mapato.

Katika swali langu niliuliza ni kwamba kiasi gani cha fedha kwa muda wa miaka mitatu tangu mkataba huu ulipofungwa ambao walikubaliana kwa asilimia 70 kwa 30, lakini majibu sijayapata ya kifedha, nataka kujua ni kiasi gani cha fedha ambacho kinapatikana.

Tumemsikia hapa Waziri wa Fedha na Mipango amekuja amesema anahitaji bajeti zaidi ya shilingi bilioni mia tatu na kitu kutoka *internal revenue* kukusanya. Sasa hapa kuna mapato makubwa nataka kufahamu ni kiasi gani, kwa sababu tayari Katibu Mkuu wa wizara hii ni Mjumbe wa Bodi pia wa Kampuni ya Simu ya *Zantel* ni kiongozi pia. Sasa tuelezwe ni kiasi gani ya

mapato yanayopatikana katika mkataba huu kwa muda wa miaka mitatu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Simai Mohamed Said suala hili aliliuliza kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Nataka kumjibu tena hapa kwamba mambo ya mapato yote yako chini ya Wizara ya Fedha, sisi kazi yetu miundombinu, lakini tutakaa na Wizara ya Fedha pia kuangalia mambo yote hayo faida yake na itakapoonekana huu mkataba hauna faida basi hatutosita kuchukua hatua nyengine za kisheria.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu, nasema kwa Kiingereza ni *three years* tangu huu mkataba, huo mkataba kama ulifungwa kwa Kiswahili au kwa Kizungu lakini lazima kuna sehemu ambapo wizara inapoandika inafunga mkataba inakubaliana ni kiasi gani cha fedha watakuwa wanalipana, na kila mwaka serikali inakaa vikao vya bajeti na kupitisha mambo tofauti, leo ni mwaka wa tatu nasema ni *three years* tangu mkataba huu umefungwa na tayari huduma hizi zinapatikana katika kutumia huu mkonga kuna kesi tofauti.

Ukiangalia katika bajeti ya serikali yote, wizara zote, mambo yote yanayohusiana hapa labda niseme tu ngoja niisome. Nasoma katika hii Programu ya P0103, Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); haijasema Wizara ya Fedha ni TEHAMA ndio kazi yao.

Suala la *E-Government* lilikuwa linatupwa linaambiwa wahusika ni hawa, hawa na hawa; na hapa Mhe. Mohamed Said Dimwa aliuliza ni wizara gani itakuwa ni muhusika wa suala la *E-Government* ambao ni *component* moja, suala zima hili kwenye mkonga ulivyotandikwa.

Sasa hapa tunataka kujua katika hii *component* ambayo tayari wamesema katika hiyo *last mile connectivity* watapeleka katika taasisi na wizara zote ili hiyo huduma ya kupata *internet* pamoja na *data* kuweza kuzitoa na serikali moja kwa moja tu kutumia. Lakini katika hili kwa sababu serikali wao katika hii *bandwidth* wanahitaji asilimia 10 ndani ya ule *wire*, asilimia 90 walisema watafanya biashara, ndio maana wamefunga mkataba na *Zantel* ina maana hapa kuna fedha. Sasa ikiwa serikali hawawezi kutoa kauli katika suala hili ni kiasi gani cha fedha muda wa miaka mitatu nijibiwe tu, lakini sio nipigwe danedane, mimi ni mtu mzima, mimi ni Mwakilishi wa wananchi wa Tunguu. Miaka mitatu niambiwe ni fedha kiasi gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa usiendelee huko, Mhe. Mwanasheria Mkuu majibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana inaonekana Mhe. Simai Mohamed Said anazo taarifa nyingi lakini hazisemi kwa uhakika, kama anao ule mkataba angejua mkataba ule umeingiwa na *Zantel* na Wizara ya Fedha wala sio Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kwa hiyo, kama kuna masuala ya mkataba ule nadhani *the appropriate ministry* ni Wizara ya Fedha ambao ndio *signatory to the contract*. Sasa asubiri Wizara ya Fedha inakuja keshokutwa hayo masuala yake yote aje awaulize Wizara ya Fedha sio wizara hii ambayo haikuingia mkataba. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, unajua hizi kanuni inabidi zibadilike kwa sababu unaposimama mmoja huku nyuma unakuwa unapigwa na wengi huko kutoka mbele, sasa inakuwa wewe mmoja hutoshi. Lakini niendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohamed Said serikali ni moja unapomuuliza waziri...

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, sawa tuendelee tutakuja kwenye kanuni zetu huko mbele.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali na majibu aliyotoa Mhe. Mwanasheria Mkuu, hizi taarifa zilizungumzwa na *Zantel* kwenye vyombo vya habari sio kama mimi nimepata mkataba, mimi mkataba sina. Lakini haya mambo nayafuatilia kwa sababu ni uelewa tu basi, sio kwamba suala unaweza kupata ni wenyewe wanayazungumza huko nje tunapata vitu kwenye mtandao, kwa vile hiki kilikuwa ni jambo kubwa la serikali, kwa sababu fedha nyingi zilitumika za wananchi zaidi ya US$ 18 milioni kutandika hii *Fiber Optic* na hadi hivi sasa kwenye suala la *E-Government* faida zake zilizozungumzwa haziendani kutokana na maelezo ambayo serikali iliazimia katika kipindi kilichotoka, na hasa baada ya Rais kuzindua mpango mzima wa *E-Government* katika Sherehe za Mapinduzi. Hiyo ni *component* moja.

Hii *component* ya pili katika suala zima la kutaka kupata fedha kuingia na *Zantel* kuuza hiyo *bandwidth* na mbali inayotumika, hizi fedha mimi wanambie tu katika huo mkataba waliofunga ni kiasi gani tutapata serikali, ikiwa hayo majibu hawana ya fedha hayajulikani kiasi gani kimepatikana hakuna jibu hata moja. Sasa unachangia kitu ambacho hupewi jibu, sasa ninachoambiwa mimi

hapa niisubiri Wizara ya Fedha, nikija Wizara ya Fedha nitaambiwa nenda Wizara ya Mawasiliano, nikitoka Wizara ya Mawasiliano nitaambiwa nenda katika Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naona napelekwa kila pahala.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba tuendelee. Tunaendelea.

Kifungu SP010301	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Mawasiliano	336,260,000
	Jumla ya Program Kuu:	**336,260,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu P0104 Programu Kuu ya Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Kifungu SP

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana, wakati nikichangia katika hotuba yangu nilichangia sehemu ya Junguni iliyokuwa katika jimbo la Gando palipita barabara ya Wete-Gando lakini wananchi wake walivunjiwa nyumba zao au ziliharibika baada ya barabara ile kutengenezwa.

Sasa nilikuwa nimeiuliza wizara sikupata jibu, kwa sababu tathmini imefanyika, ni lini watapatiwa angalau chochote ili nao basi wajisikie wajenge vibanda vyao vyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu kipindi kilichopita katika maswali yaliyoletwa Barazani kwamba tuna utaratibu ambapo huwa tunalipa fidia kabla ya ujenzi na tunaangalia baada ya ujenzi ima nyumba kuathirika kutokana na barabara tuliyojenga. Ni kweli tunayajua madai hayo na pale ambapo serikali itapata pesa basi watu sio wa Junguni tu, wako wengi kama nilivyosema katika majibu yangu, wako watu wa *NORAD* wale ambao vipando vyao vimeharibika wanatudai shilingi 21 milioni bado hatujawalipa, wapo wenye barabara ya Gando-Wete, wapo watu wa barabara ya Konde-Wete. Kwa hivyo, namuomba atustahamilie na kadiri uwezo utavyoruhusu basi tutawalipa wahusika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana ndugu yangu Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini nataka kusema jambo hili linafika mwaka wa tatu mpaka wa nne, serikali itafika lini mbio hizi au itapata wapi pesa za kuwalipa masikini wale wana-*suffer* kabisa hawana pa kukaa, nyumba mbovu, hebu watueleze tu *commitment* ya serikali lini itawalipa angalau waseme mwakani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tumekaa na kuangalia madeni yote tunayodaiwa na wahusika na vile vile wakandarasi. Kwa hiyo, ni jitihada zetu kuhakikisha kwamba wale wote ambao nyumba zao zimeathirika baada ya ujenzi wa zile barabara tunawalipa. Sasa kumwambia lini hasa tunaweza kumwambia, lakini tutajitahidi katika bajeti hii inayokuja basi tuanze kuyapunguza madeni ya wale walioathirika baada ya ujenzi wa barabara hizo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru lakini nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri na ameona *concern* yangu iko wapi, lakini wananchi wa Junguni wameona jinsi gani Mhe. Naibu Waziri anavyojibu na lini atawapa. Sasa tutasubiri hapo mwakani sio mbali, kwa sababu wamesubiri miaka mitatu tutasubiri na mwaka wa nne ili tuone katika bajeti ya mwakani inakwendaje. Tuendelee.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo anasimama na serikali kutujibu Wawakilishi wao.

Mhe. Mwenyekiti, jana wakati wa kuchangia niliuliza eneo la Kwa Nyanya ni eneo hatarishi ambalo wakati wowote ukikaa maeneo yale unaweza ukapata ajali kwa ajili ya magari mengi ambayo yanatoka Kitope, Mahonda, Nungwi, Mkokotoni; magari ya mchanga na magari ya mawe yanayokaa pale.

Kama Halmashauri tulikwenda kuwaomba watu wa Mipango Miji ili pale tuweke kituo cha muda cha daladala ili kuondoa lile tatizo ambalo linajitokeza mara kwa mara la ajali. Sasa nimuombe Mhe. Waziri atwambie ni lini eneo lile angalau watapewa Halmashauri kujenga kituo cha muda mpaka hapo serikali itakapokuwa na mpango mwengine wa kufanya ili kunusuru maisha ya wananchi walioko pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua utaratibu unakuwa ni hivi, Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ huwa wanaangalia zile sehemu kupitia Halmashauri ambazo wanataka kuweka vituo. Baada ya wao kuangalia tunakaa nao pamoja na kufanya tathmini na baadae kuwakubalia.

Kwa hiyo, vituo vyote vya daladala viko chini ya Halmashauri, sisi tunatoa ruhusa tu. Hivyo, tutakaa na wizara husika ili kuhakikisha kwamba iwapo pale panahitajika kituo basi tutafanya hiyo kazi ili kunusuru maisha ya watu pale kutokana na msongamano na taratibu ambazo si nzuri sana za upangaji wa magari. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini bahati nzuri mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri na Tawala za Mikoa ilikuwa ndio ya kwetu, wao watu wa Tawala za Mikoa na sisi Halmashauri ndio waliotwambia tuwafuate watu wa Mipango Miji ili watupe kauli, Tawala za Mikoa pamoja na sisi kama Halmashauri. Lakini karibu sasa hivi miaka minne tumepeleka barua jibu halipatikani na wananchi wanaendelea kupata ajali, wengine wanakufa wengine wanakuwa walemavu.

Sasa nimuombe Mhe.Waziri anambie ni lini watatupa ruhusa ya kwenda kuweka japo kituo cha muda pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Masoud, kwa suala lake hili ambalo amelileta Barazani kwa kuliulizia. Lakini ninataka nimshukuru sana Mhe.Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyaeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimthibitishie Mhe. Masoud kwamba wizara tatu tutakaa; Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mawasiliano na wizara yetu ya Tawala za Mikoa ili tuweze kuliendeleza hilo jambo ambalo lilianza kutokea kwenye Halmashauri na hatimaye wizarani, tuone tunaliharakisha ili usalama kwa wananchi uweze kupatikana. Kwa hiyo niombe aturuhusu tupitishe kifungu hichi tutakaa wizara tatu; wizara inayohusika na masuala ya ardhi, Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Tawala za Mikoa tuliharakishe ili tuone tunapata kituo ili tuwaepushe wananchi na ajali za mara kwa mara katika eneo lile la Chuini. Nikuombe sana utuache tuendelee ili sisi tukakae na kuweza kulifanyia vizuri zaidi hili jambo, ahsante sana.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe.Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe.Waziri wa Tawala za Mikoa kwa majibu yake mazuri na ufafanuzi alioutoa na wizara hizi tatu ambazo alisema kwamba tutashirikiana naye pamoja ili kuweza kuhakikisha suala hili linatatuka. Lakini nimuombe sana tu Mhe.Waziri kama alivyoniomba mimi hili suala lisikae muda mrefu, kwa sababu wananchi wetu wengi wanapoteza maisha na wengine wanapata ulemavu. Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa hii.

Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka kujua kuhusu suala zima la sheria hii ya usafirishaji wa barabara, lakini naona Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu sikupata kusikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ah! Mhe. Mwenyekiti, samahani sana, kama alivyosema Mhe. Shadya kwamba sheria hii ya barabara hii ambayo ameipitisha hapa ina mambo mengi na mambo hayo imekuwa majukumu ya waziri, kuna jukumu la waziri kama alivyosema mwanzo, yako mengi sana kama nilivyomjibu Mhe. Jaku na Mhe. Gavu alivyomjibu, sasa nilikuwa nataka nijue anakusudia katika kipengele gani anachotaka tumfahamishe, na niko tayari basi kumpa ufafanuzi.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua ile sheria ya barabara ya kutozwa papo kwa papo, kwa sababu sasa hivi kama tunavyojua mambo yamekuwa mengi, mafaili yanapelekwa mengi Mahakamani bila ya kushughulikiwa, kwa hiyo nilikuwa nataka kujua sheria hii yaani ya tozo ya papo kwa papo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana suala hili pia liliulizwa na Mhe. Simai Mohamed Said ambapo kuna vifungu hivi hapa ambavyo walitaka maelezo, tuna kifungu namba 8 ambacho ni kazi ya Mhe. Waziri, kuna kifungu 160 ambacho hichi kifungu kinaelezea kazi za jeshi la polisi kuwachukulia hatua wanaofanya makosa barabarani ikiwa ni pamoja na kuegesha kiholela, kusababisha vizuizi njiani na kadhalika, kufunga njia au kubadilisha njia inapotokea dharura kama kuungua moto nyumba kuharibika njia na kadhalika.

Ama kifungu namba 183 kifungu hiki kinasema kwamba kinampa waziri uwezo wa kutengeneza kanuni za kutoa adhabu za papo kwa papo kwa makosa

yote yaliyotajwa katika sheria ya usafiri barabarani ambayo hayatozidi dola ishirini, ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu ASP 010401 Programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika sekta ya ujenzi, mawasiliano na usafirishaji 1,022,331,000

Kifungu ASP 01

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na kubwa nina dogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba wizara hii inapofanya ujenzi wake wa bandari, barabara huwa inatumia sana eneo la Muwambe la kuchukua kifusi na mawe na huwa wanachimba maeneo makubwa tu kwenda chini na wananchi wanashindwa sehemu zile kuzitumia tena kwa kilimo. Lakini Mhe. Waziri, alipokuwa anatoa majibu yake alisahau kunipa maelezo kwamba nilisema je watupe maelezo, alau kufukia yale mashimo ili wananchi wapate kuendelea na kilimo chao, lakini Mhe. Waziri alisahau kujibu naomba maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi kama nilivyosema mwanzo masuala yalikuwa mengi na muda ulikuwa mchache, tushaanza kuchukua hatua na kuanza kufukia ile sehemu ili kuhakikisha kwamba inarudi kwenye hali yake ya kawaida. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na majibu hayo kwa sababu mimi niko Muwambe, na bado wananchi wanapata mashaka kulima sehemu zile, mimi ningeliomba Mhe. Waziri akaniahidi tu kwamba kuanzia hivi sasa yale mashimo akayafukia kidogo kwa udongo, haiwezekani kuyafukia yote, lakini alau afukie yote kwa udongo ili wananchi wapate kuendelea na kilimo, naomba ahadi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema tutayafukia kwa udongo na namuahidi kwamba hiyo kazi tutaifanya.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia bajeti hii nilieleza kwa niaba ya wananchi wa Uzini makubaliano ya wananchi wa Uzini na Wizara ya Mawasiliano kuhusu barabara ya Pagali - Umbuji, Ndagaa - Ndondongwe, Kwakibawa - Mkuki na Ndondongwe - Mkuku.

Haya yalikuwa makubaliano lakini majibu niliyokuwa nimepewa sikuridhika kwa sababu yalikuwa ni makubaliano hayo kati ya wizara na wananchi wa Jimbo la Uzini kupitia mimi Mwakilishi na tulikubaliana kwa mkataba, nimetakiwa kutoa milioni 20 ili kazi hii yote iende ikafanyiwe na hii risiti ya serikali. Kwa hivyo nilikuwa ninaomba tu kwa ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa namjibu inawezekana kidogo hakunisikia vizuri.

Nilimjibu kwamba kuna barabara hizo alizozitaja kuna nyengine zimejengwa na Wizara ya Kilimo kupitia mradi wao wa *MIVARF*, na hiyo barabara anayosema yeye ya Pagali tunakubaliana nilimjibu hapa katoa milioni 20 kwa bahati mbaya *grader* yetu iliharibika kule na ilikaa muda mrefu kweli, na matengenezo yake kama unavyojua makubwa sana kupita hata hizo milioni 20, na ile barabara ilikuwa tayari tushaitia kwenye mpango wa kifusi. Sasa nadhani kuna makubaliano tutakaa naye ili kuhakikisha kwamba hayo makubaliano yanatekelezwa, kwa sababu hakika ahadi ni jambo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi, ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, hili suala tulikuwa nalo hapa kwa miaka mitatu, nataka nikumbushie tu mwaka juzi nilipozuia kifungu hichi Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakaniambia Raza kupitia wananchi wa Jimbo la Uzini pitisha kifungu ili twende tukayakamilishe haya makubaliano.

Kwa hivyo, halafu akasimama vile vile Mhe. Naibu Waziri, namuheshimu sana Mhe. Gavu naye vile vile, kwa bahati mwaka juzi hapajatekelezwa tukaja katika bajeti ya mwaka jana, bajeti ya mwaka jana niliposimama Mheshimiwa nikaambiwa mashine imeharibika, nikawaambia je, mnahitaji pesa ya mashine hii ya kutengeneza, wakaniambia aah!

Mhe. Waziri ndiye ambaye ninamuheshimu sana kaka yangu Mhe. Haji Omar Kheri akaniambia aah! Mhe. Raza pitisha hii bajeti ili na mashine ikatengenezwe litatuliwe hilo tatizo, namuheshimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikaendelea nikawa sijakubali, kwa sababu ni mwaka wa tatu na makubaliano. Akasimama kiongozi wa serikali Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi na akisimama akaniambia mwanangu Raza nakuomba pitisha kifungu ili tukafanye hiyo kazi na tukakubaliana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa mbele kote suala hili limeshakuwa, na pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar walipowaita barua ninayo wakaambiwa wakaitekeleze. Sasa Mheshimiwa hapo ndo nilipo, kwamba mpaka kiongozi wa serikali ambayo *Hansard* ipo akaahidi kwamba pitisha kifungu mwanangu, na mimi nikasema sikio halipandi juu wewe baba angu kiongozi wetu, mpendwa wetu, muasisi wetu ninakubali. Sasa Mheshimiwa leo nimesimama tena hapa, baada ya miaka mitatu na wenzangu kaka zangu wote mbele nawaheshimu na nitaendelea kuwaheshimu, naomba Mheshimiwa tamko la serikali kwa hili, kwa sababu yako makubaliano.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Raza, milioni 20 hazijengi barabara, hizo anazozitaka yeye, barabara Dongongwe - Mchangani *MIVARF* washamtengenezea, barabara ya Bambi - Umbuji tumemtengenezea. Nashukuru kuna wenzake hapa wa Micheweni walilalamika yeye hata barabara moja kutengenezewa, atukubalie kwamba tuna nia nzuri, na kama nilivyosema mwanzo barabara hiyo aliyoitaja tumeitengeneza kwa kifusi kilomita 2, lakini kimeharibika kifaa chetu cha kutengenezea.

Mimi namuheshimu sana Mhe.Raza ni mdau mzuri wa maendeleo na anaumwa sana na wananchi wake, kwa hiyo kama alivyostahamili kwa barabara ile ya Miwani mpaka Kizimbani na kwa hili alistahamili serikali italifanyia kazi, ahsante Mwenyekiti, namuomba sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, hii inadhihirisha wazi leo katika Baraza hili Mhe.Naibu Waziri anapinga kauli ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar na kiongozi mkuu wa serikali, inasikitisha sana.

Mheshimiwa haya ni makubaliano si suala la hisani. Kwa hiyo ninachotaka kusema bado naomba msimamo wa serikali, bora niende mbele kwa Mwenyezi Mungu ninayemuogopa tupigeni kura kifungu hicho kwa sababu huu ni utovu wa nidhamu kwa viongozi, kwamba Makamo wa Pili wa Rais, kiongozi wa nchi ametoa kauli leo unasema kwamba ni jambo la hisani nafanyiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimeshakufahamu ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kabisa kwanza kabla ya kumjibu Mhe. Mohammedraza Hassanali nichukue nafasi hii ya kumuomba ashushe munkari, ashuke munkari ili sote tuwe tunaimba nyimbo mmoja, nyimbo ya kutaka kulisaidia taifa letu, nyimbo ya kutaka kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba suala ambalo amelisema Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali ni la muda mrefu, na ni kweli imechukua hadithi ndefu na ni kweli kwamba Serikali kwa kushirikiana na viongozi wa majimbo tumekuwa tuna kawaida hiyo ya kushikana mikono si kwa mantiki kwamba tunachangishana aha! ni kwa madhumuni ya kushikana mikono katika kuharakiza maendeleo katika maeneo husika kwa faida ya wananchi wetu, na ni kweli kwamba kiongozi wao huyu wa Uzini alishirikiana na Wizara ya Miundombinu kwa wakati ule ambapo sasa hivi ni Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, na madhumuni makubwa ni kujenga barabara kwa kiwango cha kifusi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri ameeleza vizuri sana kwamba katika Jimbo la Uzini tayari serikali imeshaweka mkono wa kusaidia maendeleo. Lakini Mheshimiwa. Mjumbe anavyosema kwamba bado kuna barabara ambazo anaiomba Serikali iendelee kushirikiana naye. Nimuombe tu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwamba ahadi ya serikali kutoendelea kushirikiana naye katika kutekeleza na kuendeleza maendeleo katika jimbo lake.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hizi anazosema ni nyingi, lakini kama zilikuwa kumi na tano naamini sasa hivi tano tayari zimeshachukuliwa hatua na Serikali. Sasa na hizi kumi kwa mantiki ile ile, na nimuombe tu asichoke, mchango alioutoa mwanzo serikali saa nyengine tutakutana naye tutaendelea kutaka kushikana naye mikono ili tuendeleze gurudumu hili la maendeleo kwa wananchi wetu kwa haraka kama vile yeye mwenyewe angependa iwe hivi.

Mhe. Mwenyekiti, barabara anayoizungumzia Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali *specific* ni barabara ya Pagali, ambapo kuna kipande kilikuwa kirefu kinatokea Umbuji, Kidagoni pale kwenye kituo cha daladala ndipo ambapo ilikuwa inaishia, na ni kweli serikali ilifanya kitendea kazi kile kikawa kimeharibika baadae serikali tukatengeneza tukaendelea na maeneo mengine.

Kwa hiyo nimuombe tu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwamba kwa nia ile ile ya awali kwamba ahadi ya serikali kuendelea

kushirikiana naye katika kupeleka maendeleo katika jimbo lake, sio tu kwa barabara hii na barabara nyengine ambapo serikali imeendelea kuzifanya nazo pia zitafanywa kama zinavyofanywa katika majimbo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna maeneo ambayo kweli yalikuwa maeneo *critical*, kwa mfano daraja la Dongongwe. Mimi naamini kwamba serikali imeshaliona na itachukua hatua ya dharura kwenda kulihami ili wananchi waweze kupita vizuri hasa kipindi ambacho kutakuwa mvua imenyesha iwe katika mawasiliano baina ya upande mmoja na upande wa pili wa ng'ambo ya kijiji husika.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Raza kwa heshima kubwa sana atukubalie serikali tupitishe kifungu hichi ili twende kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru Mhe. Waziri na namuheshimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, haya yalikuwa makubaliano na nilivyoambiwa toa milioni 20 na nyengine zitachangiwa, yalikuwa ni makubaliano, sasa haya mimi nayasimamia, ni makubaliano, na kipindi chote mpaka kiongozi wa serikali aliposema na ikathibitishwa, na ninaomba nitoe nyaraka yalikuwa makubaliano, kwa hivyo ninachotaka niambiwe hapa kesho, kesho kutwa, kwamba yale makubaliano ya serikali na wananchi wa jimbo la Uzini.

Mhe. Rais kalitolea kauli yatekelezwe si kwa nini ya makubaliano, kwa hiyo lini, kesho, kesho kutwa, mimi Mheshimiwa nataka lugha ya kesho, kesho kutwa ili tuweze kufahamiana, haikuwekwa hivyo, mimi namuomba Mungu tupigeni kura.

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa tushatumia mara...

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Sikuridhika Mheshimiwa na kauli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Tushatumia mara tatu kwa mujibu wa kanuni itabidi twende kwenye kura tu moja kwa moja. Naomba niwahoji wale wanaounga mkono tuendelee, wanyanyue mikono yao, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji nakumbuka kama nilikwita na wewe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwisho na nimeamua kulizuia fungu hilo linalohusiana na utawala kwa sababu ipo kadhia moja niliizungumza katika michangio yangu inayohusu watendaji, na watendaji hawa katika kutengeneza mikataba na wajenzi wa barabara na nikaizungumzia hiyo barabara ya *DB SHAPRIA*, nikataka pia nije nieleze hapa hatua ambazo serikali imezichukua lakini katika kipengele cha *performance security* ambacho mara zote kimkataba inakuwa kina-*deduct amount* fulani ya fedha katika malipo ya awali ili mkandarasi yule akishindwa serikali iwe inakuja kutumia fedha zile ili ni sehemu yake ya fidia. Sasa nilitaka kujua haya waziri hakunijibu. Naomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niendelee kumshukuru Mhe.Miraji Khamis Mussa Kwaza Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chumbuni kuhusiana na suala lake zima la barabara *SHAPRIA*.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza naomba nimtoe khofu Mhe. Miraji kwamba mikataba hii sio tu kwamba inasimamiwa na watendaji, mikataba hii inasimamiwa na serikali nzima chini ya maelekezo na usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo katika mikataba hii serikali inachukua jitihada kubwa na tahadhari kubwa kwa kuona kwamba kwanza tunatimiza wajibu wetu katika kutekeleza matakwa ya mkataba, pili tunasimamia, na tatu tunataka kuhakikisha kwamba na upande wa pili nao pia unasimamia vizuri mkataba husika.

Mhe. Mwenyekiti, Mkandarasi ambaye anazungumzia Mhe. Miraji ni Mkandarasi ambaye alipewa kazi ya kujenga barabara tatu za vijijini Unguja, barabara ya Jendele-Cheju-Kaibona yenye urefu wa kilomita 11.7, Jumbi-Koani yenye urefu wa kilo 6.8 pamoja na Kizimbani-Kiboje. Bahati nzuri katika mradi *portion* ya Kizimbani-Kiboje ikawa imetolewa, sasa Mkandarasi amefanya kazi amefika pahali kwamba ameshindwa ku-*perform* kwa mujibu wa mkataba. Maelezo ya serikali yapo wazi, kwamba kwa vile mkandarasi ameshindwa kutekeleza kwa mujibu wa mkataba, serikali tunavunja naye mkataba.

Katika kuvunja naye mkataba kuna mambo ya msingi ambayo sisi kama serikali tutachukua na yeye kama mkandarasi atapaswa kuyasimamia ama

kukubali yale ambayo serikali itayachukulia hatua. Miongoni mwa hatua hizo ni:-

1. Serikali ku-*retain* kile kiwango cha fedha ambacho kimekuwa tangulizwa awali kama vile mkataba unataka.

2. Kuna vifaa ikiwemo ndani ya uhifadhi wa mfanyakazi kwa mujibu wa mkataba wa vitendea kazi huyo kuwa vya kwetu tutavichukua na tutavitumia.

3. Ikibidi jengine lolote kwa mujibu wa mkataba kama sheria inaturuhusu basi sisi tutazifanyia kuweza kufanya kwa mujibu wa sheria na mkataba kama vile ambavyo mkataba unavyoelekeza.

Lakini kuhusiana na suala hili, tayari Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshafikia maamuzi na serikali ipo katika hatua za mwisho kuona kuwa kunapatiwa utaratibu mzuri wa barabara hizi kuweza kuzinusuru na kuzijenga yenyewe chini ya usimamizi wa Idara yetu ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia na ile nia ya serikali inapofika pahala ya kutumbua majipu ndiyo ninaiona. Lakini bado pia ningetaka kujua *amount* ambayo niliielezea wazi katika ile *performance security* ni asilimia ngapi na wali-*deduct* kiasi gani.

Nilichokuwa ninahitaji yale yote, ya hatua walizozipeleka ninamshukuru sana Mhe. Waziri nimemfahamu, sasa ninataka kila mkataba hivi vitendo vinafanyika. *Amount* sasa waliyo-*deduct* katika ile sehemu yake ya mwanzo ambayo hii inakuja kutulinda sisi pale ambapo mkandarasi anashindwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninahitaji majawabu katika eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ningependa kusema sana na kwa ufafanuzi mkubwa sana, lakini suala hili mwenzetu huyu hakuridhika na yale maamuzi ambayo tumeyafanya. Suala hili amelikimbilia Mahakamani. Sasa kuendelea kusema *details* za ndani, maana yake nitakuwa ninaendelea kuvuruga utaratibu ambao ni kinyume na Kanuni zetu.

Nimuombe tu Mhe. Mwakilishi uweke *concern* yako subiri imalize Mahakama na ikabidi kuja kusema baada ya utaratibu na sheria kuturuhusu tunayo mengi ya kusema kuhusiana na suala hili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe.Mwenyekiti, nataka ninapata mashaka sana. Majibu ya mwanzo nimepewa Mahakama haikutajwa. La pili Mahakama inatajwa. Sasa si vyema wakati fulani serikali ikawa inatengeneza majibu kwanza baadae inasema suala hili lipo Mahakamani.

Lakini kwa sababu utaratibu kwa kuwa lipo Mahakamani na mimi ninaheshimu, lakini tokea mwanzo ningeiomba serikali isitupe majawabu kwa suala ambalo lipo Mahakamani, wazungumze *direct*. Lakini tumepewa jawabu mwanzo lakini la pili ninaambiwa hili lipo Mahakamani haiwezekani kujibiwa.

Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Nafasi tatu zimekamilika Mheshimiwa tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mheshimiwa tafadhali kaa.

Kifungu SP 010402	Programu Ndogo ya Mipango na Sera katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	Shs.183,198,606,000/-

Kifungu SP 01

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii. Katika maelezo yangu nilivyokuwa ninachangia niliuliza suala zima juu ya tozo linalotoka kwa *shipping agent* yaani Shirika la Meli. Tozo linalotozwa *consignee*, wakati wao siyo mamlaka wao, hawa ndiyo moja kwa moja mawakala lakini sikupata jibu. Ijapokuwa siyo pahala pake kwa sababu ndiyo maana pale nikamwambia tulikuwa turekebishe angalau tuseme, kuna mambo mengi sana tunabinywa huko mbele tusiseme.

Ndiyo maana pale nikatoa hoja kwamba angalau tuongezeke watu watatu mpaka sita kwa sababu kuna mambo mengi tunatetea wananchi hatupati nafasi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Kifungu ni uratibu wa shughuli za wizara Pemba. Kwa hivyo kama halihusiani na hapo nakuomba kwa heshima na taadhima, nimwite mtu mwengine tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba hizi nafasi ukaturuhusu tukauliza maswali yetu, ningeomba sana lakini nitakwenda huko huko.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir kama halihusiani na hapa pia usitupotee wakati tafadhali.

Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf Al-Wardy: Tutakwenda huko huko. Kwa kuwa Wizara ya Pemba katika ujenzi wa barabara inapojengwa barabara haichukui muda hasa upande wa Pemba na Unguja inakuwa inafanya matuta, inaharibika. Je, mimi niliuliza swali moja. Ni kiasi gani cha fedha kwa kilomita wanalipa serikali na *tons* ngapi ya barabara, kwa kuwa barabara zikijengwa muda tu zinafanya matuta kama njia ya resi. Naomba anijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hili ni suala la uratibu. Matuta ya barabara Pemba ni sehemu gani unakusudia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ni barabara iliyojengwa ya lami lakini baada ya mwezi, miezi miwili tu inafanya matuta, ile barabara yenyewe inafanya matuta. Kiwango kidogo au kiwango kibovu. Ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kinalipa serikali kwa kilomita moja kumlipa mkandarasi na *tons* ngapi ya barabara inakuwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hili swali halihusiani na hichi kifungu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Kifungu ni uratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Ni uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ndiyo Pemba. Mhe. Mwenyekiti, Pemba bandari ipo. Kwa hivyo suala langu litagonga bandari.

Mhe. Mwenyekiti, bandari ndiyo kiini chetu.

Mhe. Mwenyekiti: Bandari ya Mkoani au vipi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ni ya Zanzibar, kwa hivyo bandari ikiwemo ya Pemba. Kwa vile shughuli za Pemba. Bandari ndiyo kiini chetu.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara wanalalamika sana dhidi ya mambo ya bandari. Sasa kuna hoja kwamba nilipokuwa ninachangia tuliambiwa kwamba Wizara ya Fedha ndiyo itakuja kujibu masuala haya. Sasa kuna tetesi kwamba pale Bwawani kwa vile ni bandari. Je, huyu mwekezaji anataka kulipwa au atatupa pale pahali *free*.

Kwa sababu kuna tetesi anataka kulipwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa tumekusikia lakini halihusiani na Pemba. Naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia tena nafasi. Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango niligusa Pemba hasa katika jimbo langu kwa kuwa kule Makangale Kigomasha kuna kituo chetu kikubwa cha bandari ambako kuna mnara ule wa Kigomasha na kuna wafanyakazi wa bandari. Kuna tatizo kule la usafiri na huduma za maji kwa wafanyakazi wa kule.

Je, wizara inawaangalia vipi wale wafanyakazi kuwapunguzia tatizo la usafiri wale wafanyakazi waliopo mnarani, wafanyakazi wa bandari. Na vile vile kutatua lile tatizo la maji la wafanyakazi wanaokaa kule ikichukuliwa maanani kwamba serikali inatumia pesa nyingi kukodi gari kutoa maji sehemu nyengine kuwapelekea wafanyakazi kule.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua ni kweli tuna tatizo hilo la usafiri si kwa wafanyakazi wetu waliopo kule tu bali pia Mhe. Waziri kalihimizia kuhusu wafanyakazi wetu wa Kitengo cha Leseni na idara nyingi tu wana tatizo la usafiri.

Tunayachukua hayo matatizo na kuyafanyia kazi na kuhusu tatizo la maji basi tutakaa na wizara husika kuangalia namna gani tunalitatua kwa wakati huu hasa kuwaondolea shida wafanyakazi wetu wa kule Kigomasha.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi pale ndiyo kwenye wapiga kura wangu na ni kilio, na kwa sababu mimi ninakaa pale pale ninafahamu shida waliyonayo. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri alichukulie suala hili kama dharura, ili wale ni binadamu waliopo pale wapate huduma. Huduma ya maji ni kitu muhimu. Kwa hivyo, ahsante sana, ninaomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, tunaendelea, zile nafasi tatu...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hawakujibu.

Mhe. Mwenyekiti: Zilikuwa *covered* Waheshimiwa.

Mhe. Mjumbe Fulani: Mhe. Mwenyekiti, bado mbili.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa. Niliyemwita ilikuwa imekwenda ile nafasi kwa sababu ameshindwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hawakufahamu wale utaratibu, kwa sababu hili suala la Pemba hili na hili ni moja tu.

Mhe. Mwenyekiti: Huyu nimempa ya upendeleo kwa sababu kwanza anahusiana na huko huko. Tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa ninakuomba.

Kifungu SP 010403	Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba	Shs.1,457,810,000/-
Jumla		**Shs.185,678,807,000/-**
Jumla Kuu		**Shs.188,554,100,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya fedha ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kazi nzuri hii ya kupitisha bajeti ya wizara yake. Pia nichukue nafasi hii kukupongezeni kwa namna ambavyo mumeonesha hamu kubwa sana ya kuwasilisha hoja mbali mbali ambazo mumepewa na wananchi wenu na hatimaye zimeweza kufika na baadhi kujibiwa. Ingawa ninajua siyo kila mmoja atakuwa ameridhika vile alivyokuwa anataka, lakini kimsingi wizara imesikia na watayachukua hayo kwenda kuyafanyia kazi kama ambavyo mulikuwa munahitaji iwe hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya kumaliza hapo, sasa naomba nimwite Mwenyekiti aje achukue hii nafasi kabla hatujaendelea na shughuli inayoendelea na simuoni, Katibu kwa shughuli inayoendelea.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Afya kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Afya:

UTARATIBU

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, ninashukuru tumepitisha Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji lakini tunaingia katika wizara moja muhimu sana kwa maslahi ya wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa ninajua leo ni Ramadhani ya kumi na nne, tunataka tukuombe tutengue Kanuni ya 98(3) ili tuweze kuwa na Wajumbe wengi wachangiaji pale inapofika wakati kupiga mabuti, kwa sababu Mhe. Spika, kazi yetu sisi Wawakilishi ni kuwatetea wakwezi na wakulima ili tuweze kuwaletea maslahi mazuri. Halikadhalika kushirikiana na Serikali hii ya

Mapinduzi inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika kuwaletea maslahi bora wananchi wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, tumekaa tumejadili sana na tumeliona sana, tumelifikiria sana, tumehisi watu watatu hawatoshi. Tunakuomba Mhe. Spika, Ramadhani ya leo ya kumi na nne utukubalie hili. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi ningependa sana tu tupate siku tatu tatu kwa kila wizara ili ichangiwe na watu mpaka wamalizike. Lakini ratiba yetu imebana mno na ndiyo maana mulitoa siku ya Jumamosi juzi katika kujaribu kuipa nafasi hii ratiba. Na nyinyi pia mutakuwa mashahidi siku hizi tumekuwa na *style* ya kutoleta maswali ili kuzidi kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe muweze kuchangia hizi wizara zinapowasilisha bajeti.

Leo ninamwita sasa hivi Mhe. Waziri wa Afya anasoma lakini kwa ratiba jinsi ilivyobana kwa vyovyote vile, kesho saa tisa tuwe tunamaliza wizara hii. Kwa maana kwamba itaanza kuchangiwa kama mutaipa nafasi sasa hivi, lakini pia itachangiwa na kesho. Na pia ninajua katika kuchangia kwa kesho mpaka amalizie Mhe. Waziri hatopata wasaa mzuri wa kukaa na wataalamu wake kuweza kukupeni majibu ambayo yatakuwa yanakuridhisheni, kwa sababu kwa kiasi kikubwa mutakuwa munapiga buti kama ambavyo itakuwa imezoeleka.

Waheshimiwa Wajumbe *concern* yenu ninaiona na ninaifahamu na ninatamani sana tungekuwa na nafasi ya kufanya hivyo, lakini muda haupo pamoja na sisi au haupo rafiki na sisi. Kwa maana hiyo kwamba sikubaliani na hii hoja kwa sasa hivi kwa sababu hizo. Hivyo tuendelee kuchangia, yaani tuendelee kuifuata ratiba ambavyo inatuongoza, muda hatuna. Tutajaribu kwa kadri inavyowezekana kuyaahirisha maswali ili wengi muweze kupata kuchangia hizi bajeti zinavyoendelea kusomwa. Waheshimiwa muda hatuna ingawa hili jambo ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo na kabla sijamwita sasa Mheshimiwa mtoa hoja Mhe. Waziri wa Afya, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shehe Hamad Mattar aje achukue kiti kwa niaba yangu. Njoo Mheshimiwa. (*Makofi*)

Hapa Mhe.Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikatia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Katibu tuendelee. Mhe. Waziri wa Afya, katibu tafadhali tuendelee

.

Mhe. Waziri wa Afya: *Bisimillahi Rahmaani Rahiim.*

Mhe Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Baraza hili likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2015/16 na hatimaye liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na kuwa katika hali ya usalama ambao umetuwezesha kukutana katika Baraza hili katika kikao chake cha mwanzo tangu kufanyika kwa uchaguzi wa marudio mwezi wa Machi, 2016.

Aidha napenda kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar walioitikia wito wa kushiriki katika uchaguzi huo wa marudio na kuifanya nchi kuwa katika hali ya utulivu, usalama na amani, na ninaomba wananchi wote waendelee kuilinda amani hiyo.

Mhe. Spika, pili naomba nitoe shukurani zangu za dhati binafsi kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini mimi binafsi na kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Nimefarijika sana kwa imani yake hiyo kwangu mimi binafsi na ninamuahidi kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na *in shaa Allah* sitomuangusha, na ninamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie katika kutimiza wajibu wangu huo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia naomba uniruhusu kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri ni Mwenyekiti sasa hivi aliyepo na siyo Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: *In shaa Allah* nitakapotamka Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Spika, basi naomba unichukulie kwamba natamka Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya, kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuchaguliwa tena kwa ushindi wa kishindo kuwa Rais wa Zanzibar kwa kipindi cha pili katika uchaguzi uliofanyika mwezi wa Machi, 2016. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na ampe nguvu ya kuweza kuongoza sana kwa hekima na busara katika kipindi chake chote. *(Makofi)*

Vile vile, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mahonda, kwa kuteuliwa tena kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nikiwa sijakupongeza wewe Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili la tisa, pamoja na wajumbe wako wote wa Baraza wa Baraza la Wawakilishi, waliochaguliwa na kuteuliwa kuwa wasimamizi wa utekelezaji wa mipango ya serikali. *(Makofi)*

Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yenu, na kuliongoza Baraza hili kwa ufanisi, busara na hekima kubwa likiwa na Wawakilishi vijana wengi mara hii. Naomba pia kuchukuwa fursa hii adhimu ya kumpongeza Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, ukiwemo na wewe Mhe. Mwenyekiti pamoja na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Kamati za Uongozi wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa fursa hii kumpongeza Katibu mpya wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wake wote wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi, ambao daima wamekuwa wanatuunga mkono katika kutekeleza majumkumu yetu ya Kiserikali. Tunawashukuru sana watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi. Naomba pia nimtakie kila la kheri Katibu wa Baraza aliyepita Dr. Yahya Hamad Khamis pamoja na familia yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kuwapongeza wananchi wote na kuwashukuru sana wa Jimbo la Kiembesamaki, jimbo ambalo Baraza la Wawakilishi limo katika jimbo hilo, kwa kunichagua kwa mara nyengine kuwa mwakilishi wao wa jimbo hilo kupitia Chama changu cha Mapinduzi. Aidha, namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kufanya uteuzi wake wa mawaziri wote wa serikali, ambao tuko pamoja tunashirikiana kwa umoja wetu kulitimiza lengo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii pia kuwapongeza sana na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu, viongozi wa Mikoa, Wilaya na kwenye Jamii, pamoja na wananchi wote. Wizara inatambua michango yao mikubwa ya hali na mali wanayoendelea kuitoa ambayo imeshajihisha kwa kiasi kikubwa kujenga dhamira, ari na imani kwa wafanyakazi wa sekta ya afya kutoa huduma zilizobora. Aidha, naomba nichukue fursa hii pia kuwapongeza watendaji na wataalamu wa wizara yangu kwa juhudi kubwa na mashirikiano waliyonipa katika utendaji wangu wa kuwahudumia wananchi kwa uadilifu na kupelekea kufanikisha kazi zilizopangwa na kufikisha huduma za afya kwa Wanancho wote Zanzibar yaani Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kipekee napenda kuishukuru Kamati mahiri ya Wizara ya Afya, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, chini ya mwenyekiti wake Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Dimani, kwa ushauri na maelekezo waliyotoa katika maandalizi ya bajeti hii. Ushauri wao walioutoa umeweza kuzingatiwa na hivyo kufanikisha utayarishaji wa hotuba hii. Wajumbe wote wa kamati hiyo walishiriki kikamilifu na tunawaashukuru sana na tunatarajia pia watachangia kwa kiasi kikubwa sehemu ya hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika kwa njia moja au nyengine kutokana na majanga mbali mbali yaliyowafika hususan waathirika wa maradhi ya kipindupindu, ajali za barabarani, walioathirika na mvua pamoja na majanga mengine. Namuomba Mwenyezi Mungu awape subira *Insha Allah* na kuwatakia faraja pamoja na jamaa zao wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi zangu hizo, naomba niendelee kuwapongeza wale wote ambao sikuwataja kwa njia moja ama nyengine wanachangia katika Wizara ya Afya moja kwa moja ama kwa kupitia wizara nyengine. Pia uniruhusu nitoe maelezo ya mapato na matumizi, ya utekelezaji wa majukumu na malengo makuu pamoja na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Hatimae nitoe malengo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, wizara ilitengewa jumla ya Tsh. 84,980,100,000 kati ya hizo Tsh. 16,120,900,000 kwa mishahara na maposho, Tsh. 870,700,000 kwa ajili ya ruzuku na Tsh. 12,893,400,000 kwa kazi za kawaida. Pia Tsh. 5,650,000,000 zilitengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi zilitengwa kwa mujibu wa programu ambapo programu ya Kinga na Elimu ya Afya ilitengewa jumla ya Tsh. 32,963,434.000, programu ya Tiba imetengewa jumla Tshs. 37,860,771,000 na kwa upande wa programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na utawala ilitengewa jumla ya Tsh. 14,155,895,000. Matumizi ya programu hizi hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016 yanaonekana katika kiambatisho namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya ilipangiwa kuchangia kiasi cha Tsh. 168,738,000 katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Machi

2016 jumla ya Tsh. 90,496,000 zilikusanywa sawa na asilimia 54.7 na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Idara ilitengewa jumla yaTsh. 8,004,500,000 kati ya hizo Tsh. 6,704,600,000 kwa mishahara na maposho na Tsh. 1,299,900,000 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, idara ilitekeleza programu kuu mbili ambapo Programu ya Uchunguzi na Matibabu ilitengewa jumla ya Tsh 669,743,000 na Programu ya Uongozi na Utawala ilitengewa jumla ya Tsh.7,334,757,000. Matumizi ya programu hizi hadi kufikia Machi yanaonekana katika kiambatisho namba 2. Aidha, kwa upande wa mapato Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangiwa kukusanya Tsh. 902,973,000 hadi kufikia Machi 2016, Tsh. 478,965,632 zilikusanywa sawa na asilimia 53.

MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA 2015/16

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake wizara inazingatia sera, mipango na mikakati mbali mbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (*Sustainable Development Goals*), Dira ya Zanzibar 2020 , Sera ya Afya 2011 na Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya 2013/14-2018/19. Aidha, wizara iliendela kutekeleza malengo yalioainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, yapo mafanikio mengi yaliyopatikana katika sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2015/16, kwa sasa naomba niyataje mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hicho:-

Miundombinu ya Afya

1. Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Abdalla Mzee na inayotarajiwa kukabidhiwa rasmi mwezi wa Septemba 2016 chini ya ufadhili wa SMZ na Serikali ya Watu wa China, ambapo wajumbe wako wote wa Baraza la Wawakilishi wataalikwa rasmi katika ufunguzi wa hospitali hiyo ya Abdalla Mzee Pemba.

2. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya afya vya Kinuni, Bumbwisudi na Ukongoroni na nyumba ya wafanyakazi ya kituo cha afya Kiongwe.

3. Asilimia 80 ya ujenzi wa wodi ya watoto ya Hospitali ya Mnazi Mmoja umekamilika chini ya ufadhili wa pamoja kati ya SMZ na Serikali ya Norway.
4. Kukamilika kwa ujenzi wa wodi mbili za wanaume na jengo la huduma za matibabu ya nje katika Hospitali ya Kivunge

Nguvu Kazi ya Sekta ya Afya

5. Kuajiri madaktari 25, mtaalamu mmoja wa viungo bandia, mtaalamu mmoja wa mionzi na kupeleka wafanyakazi 134 masomoni, kati yao wakiwemo madaktari saba wanaosomea fani za udaktari bingwa. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya haikuwahi kupeleka idadi kubwa kama hii ya wafanyakazi kuliko ilivyofanya katika miaka mitano hii iliyopita.

Utoaji wa Huduma

6. Kudhibiti maradhi ya malaria kuwa chini ya asilimia 0.5. Jambo ambalo sasa hivi Zanzibar tuna fahari nalo kubwa sana, kwamba maradhi ya malaria yako chini ya kiwango kile cha asilimia 1.

Uongozi na Utawala

7. Kuimarika kwa utendaji wa mabaraza na bodi za afya, ambazo zote sasa hivi zimeshamiri na kuimarika vizuri zaidi.

CHANGAMOTO

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kuwa yapo mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/16, hata hivyo wizara bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji mashirikiano yetu sote kwa pamoja katika kuzitatua changamoto hizo. Changamoto kuu za kiutekelezaji zinazoikabili Wizara yetu ya Afya ni kama zifuatazo:-

1. Uhaba wa fedha za ununuzi wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba hali ambayo husababisha mrundikano mkubwa sana wa madeni.

2. Ongezeko la maradhi yasioambukiza yakiwemo shindikizo la damu, kisukari, saratani na ajali za barabarani. Ukuaji wa maradhi haya yenye gharama kubwa ya matibabu imeathiri uwezo wa sekta na wananchi ambao wanaohitaji huduma hizo uliopelekea kuongezeka kwa deni kubwa kwa wale wanaokwenda nje ya nchi kwa ufadhili wa serikali kwa ajili ya matibabu.

3. Kuharibika mara kwa mara kwa vifaa tiba kutokana na upungufu wa utaalamu wa kukarabati vifaa hivyo na kuongezeka kwa wagonjwa wengi sana wanaohitaji huduma hizo za vipimo.

4. Kuongezeka kwa bidhaa ambazo hazikidhi viwango zinazoletwa na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao hupitisha bidhaa zao katika bandari na njia zisizo rasmi, zinazoathiri afya ya mtumiaji na kuzidiwa kwa upande wa gharama za kuangamiza vifaa hivyo ambavyo ni *fake*.

VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 vipaumbele vya bajeti vinavyotumia bajeti ya programu ni vifuatavyo:-

Programu ya Kinga na Elimu ya Afya

Kuimarisha huduma za kinga ikiwa ni pamoja na huduma za uchunguzi wa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kwa jamii. Utekelezaji wa kipaumbele hivi unaonekana katika mikakati ifuatayo:-

1. Kuongeza uwezo wa wafanyakazi wa afya katika kutambua na kutibu magonjwa ya watoto.
2. Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa, zana za huduma za uzazi salama, huduma za mama na mtoto na huduma za uzazi wa mpango (*family planning commodities*).
3. Kufuatilia vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga.
4. Kuendelea kutoa huduma za chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano na kinamama walio katika umri wa kuzaa.
5. Kudhibiti na kufuatilia maradhi ya miripuko yakiwemo ya kuambukiza na yasiyoambukuza.

Programu ya Tiba

1. Upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba ili kuhakikisha kutokuwepo kwa upungufu wa dawa muhimu katika hospitali na vituo vya afya.
2. Kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi kwa ajili ya maabara.
3. Kumalizia kuandaa rasimu ya sheria ya Bohari kuu ya Dawa.
4. Kuendelea na mchakato wa ujenzi wa Bohari ya dawa Pemba.

Kuendelea kuiboresha mifumo ya uendeshaji kwa kazi za Bohari. Mfumo wa *m-Supply* katika kuhifadhi, kutoa na kusambaza dawa, na mfumo wa moneywork kwa kazi za fedha na uhasibu na mfumo wa *eLMIS.*

Programu ya Usimamizi wa Sera ya Afya na Utawala

1. Kukamilisha sheria ya uanzishwaji wa mfuko wa Bima ya Afya.
2. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mkakati wa III wa Sekta ya Afya 2013/14-2018/19.
3. Kuimarisha nguvu kazi katika sekta ya afya.
4. Kuimarisha miundombinu ya Afya ikiwemo:-
   i. Kujenga nyumba za wafanyakazi wa hospitali ya Abdalla Mzee.
   ii. Ukarabati wa jengo la macho katika Hospitali ya Mnazi mmoja.
   iii. Kuendelea na ukarabati pamoja na ununuzi wa vifaa vya jengo lililokuwa kiwanda cha madawa kwa ajili ya huduma ya mama na mtoto.
   iv. Ukarabati wa vituo 19 vya afya ya msingi. Vituo hivyo vingi vya wawakilishi ambavyo watakuja kuuliza baadae vimo katika hivi vituo 19.

Programu ya Hospitali ya Mnazi mmoja

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya hospitali ya Mnazi Mmoja vipaumbele ni:-

1. Kuimarisha huduma za uchunguzi ikiwemo ununuzi wa mashine ya *MRI.*
2. Kuimarisha huduma za tiba kwa kuanzisha huduma za kusafisha damu kwa wenye matatizo ya figo (*Dialysis*) ikiwemo ununuzi wa mashine husika.
3. Kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba na vya uchunguzi.
4. Kuziimarisha kambi za matibabu kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.
5. Kuendelea na mchakato wa kuifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika bajeti iliyopita kwamba Wizara ya Afya inatekeleza programu kuu tano:-

Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Programu ya Tiba, Programu ya Usimamizi wa Sera na Utawala na programu mbili za Hospitali ya Mnazi Mmoja ambazo ni Programu ya Uchunguzi wa Matibabu na Programu ya Uongozi wa Hospitali na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nianze kuelezea utekelezaji wa kila programu kwa ufupi, ambazo zimegawika katika programu ndogo ndogo na huduma, kama ifuatavyo:-

PROGRAMU NAMBARI 1: PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kinga na Elimu ya Afya inalenga kutoa huduma bora za afya katika ngazi za vituo vya afya vya msingi, daraja la kwanza na la pili na kuwa na jamii yenye uelewa wa jinsi ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Utekelezaji wa Programu hii unaonekana kupita huduma tofauti kama utakavyoelezwa.

Huduma ya Kumaliza Maradhi ya Malaria

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za kumaliza maradhi ya malaria zimeendelea kutekelezwa kupitia mkakati wa kitaifa wa "Kumaliza Malaria Zanzibar". Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mkakati huo ni usambazaji wa vyandarua, utiaji dawa za kuulia mbu waenezao malaria, uchunguzi sahihi wa wagonjwa wa malaria, ufuatiliaji wa wagonjwa wa malaria, ufuatiliaji wa tabia na wingi wa mbu katika ngazi ya shehia na uhamasishaji jamii kupitia njia za redio, televisheni, vipeperushi na mikutano.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kwamba tumefanikiwa kupunguza malaria chini ya asilimia 0.5, bado zipo Wilaya ambazo zinaripotiwa kuwa na maradhi haya kama vile Wilaya Kati, Kusini, Kaskazini A, Kaskazini B na Magharibi kwa Unguja na kwa Pemba ni Wilaya ya Micheweni na Wete. Wilaya hizi bado zinaendelea kuripoti wagonjwa kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

Mhe. Mwenyekiti, upigaji dawa majumbani umefanyika na kushirikisha Shehia 55. Matokeo yameonyesha kuwa nyumba 27,455 (92%) zimepigwa dawa ikilinganishwa na nyumba 29,632 zilizopangwa kupigwa dawa. Haya ni mafanikio makubwa yanayokwenda sambamba na viwango vya Shirika la Afya Ulimwenguni. Aidha, jumla ya vyandarua 72,602 viligawia kwa jamii kupitia mpango wa vyandarua endelevu, kati ya hivyo vyandarua 20,236 vimegaiwa kwa watoto chini ya mwaka mmoja, 22,277 kwa mama wajawazito na 30,089

kwa watu wengine ndani ya jamii. Sambamba na kazi hii, Wizara inakusudia kugawa vyandarua 780,000 kwa nchi nzima.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa wagonjwa wa malaria wanafuatiliwa majumbani kwa lengo la kuchunguza wana kaya ili kuzuia maambukizi mapya. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, jumla ya wagonjwa wa malaria 2,480 waliripotiwa, kati yao wagonjwa, 2,290 sawa na asilimia 92.3 walifuatiliwa majumbani na maofisa wa ufuatiliaji, na wagonjwa 190 hawakupatikana kutokana na kutoa taarifa na anuani zisizo sahihi. Uchunguzi wa kina ulifanyika kwa maeneo yenye kutoa wagonjwa mara kwa mara. Katika uchunguzi huo jumla ya watu 16,529 waliokuwa hawana ishara na dalili za malaria walichunguzwa vimelea na kati ya hao 713 walikutwa na vimelea vya malaria na kutibiwa kwa dawa husika ili kukata kasi ya maambukizi.

Huduma za Kinga Dhidi ya Maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma

Mhe. Mwenyekiti, huduma hii inalenga kupambana na maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma kwa kutoa huduma za kinga na tiba zinazohusiana na maradhi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha tiba na ushauri nasaha, jumla ya kliniki 12 zinatoa huduma na tiba (8 Unguja, 4 Pemba) kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI (*VVU*) kliniki hizo ni Mnazi Mmoja, Muembeladu, Al-Rahma, AYADESA Miembeni, *MAT Clinic* ya Kidongo Chekundu, Bububu Military, Kivunge, Makunduchi, Wete, Mkoani, Chake Chake na Micheweni . Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Disemba 2015 jumla ya wagonjwa 8,721 walikuwa tayari wameshasajiliwa kwenye kliniki hizo, miongoni mwao wagonjwa 6,251 (71.7%) walianzishwa dawa za kupunguza makali ya *VVU* (*ARVs*), wagonjwa waliobaki kwenye dawa mpaka kufikia Machi 2016 ni 3,978.

Mhe. Mwenyekiti, kazi nyengine iliyofanywa ni kukusanya sampuli za damu za watoto ambao mama zao wameambukizwa na virusi vya UKIMWI na kupelekwa Muhimbili kwa ajili ya uchunguzi. Jumla ya sampuli 171 zimepelekwa katika hospitali hiyo kati ya sampuli 146 zilizotolewa majibu watoto wawili (1.4%) wamegundulika kuwa na maambukizo ya *VVU.*

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2015 – Machi 2016, jumla ya watu 69,155 (wanaume 35,679 na wanawake 33,476) walichunguzwa katika vituo

vya ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya UKIMWI,kati yao watu 810 (1.2 %) waligundulika kuwa wanaishi na *VVU*. Idadi ya watu waliochunguzwa imefanywa katika vituo 98 (Unguja 67 na Pemba 31) na kupitia huduma za masafa (*outreach*).

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kupunguza athari kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya, Wizara imeendelea kuwapatia dawa ya *methadone* vijana hao ili kuachana na matumizi ya dawa za kulevya, jukumu hili la methadone lipo chini ya Wizara ya Afya. Jumla ya vijana 168 wanaendelea na matibabu hayo katika kituo maalum kilichopo katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu ambapo kwa masuala ya utawala Kamisheni inayohusiana na dawa za kulevya ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Kifua Kikuu, jumla ya wagonjwa 390 (202 Unguja na 78 Pemba) waligundulika kuwa na Kifua Kikuu. Sambamba na hilo, jumla ya wagonjwa 193 wamefuatiliwa katika familia zao, watu 667 walipata elimu juu ya kujikinga na maradhi hayo, kati yao wanne walikuwa na dalili na mmoja alithibitika kuwa na kifua kikuu. Madhumuni hasa ya kazi hii kujua kama familia wanaoishi nao hawajapata maambukizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kupunguza ulemavu utokanao na Ukoma, zoezi la kuwafuatilia watu walioambukizwa na ugonjwa wa ukoma limefanyika Unguja na Pemba, kwa lengo la kuwatambua wale ambao wanaweza kufanyiwa urekebishaji wa viungo (*reconstructive surgery*). Katika zoezi hilo, jumla ya watu watano wamepatikana kutoka Wilaya ya Kusini Unguja na wanategemewa kufanyiwa upasuaji katika kipindi hiki. Aidha, uchunguzi ulifanyika katika Shehia 15 za Wilaya ya Kusini Unguja, ambako ugonjwa huu umeenea. Katika uchunguzi huo jumla ya watu 2,275 walichunguzwa, kati yao watu 215 walikuwa na maradhi ya ngozi na watu 40 waligundulika na maradhi ya Ukoma. Matibabu stahiki walipatiwa wale wote waliogunduliwa na maradhi hayo.

Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Mwenyekiti, ni jukumu la Wizara kuhakikisha watoto na mama wajawazito wanapatiwa huduma za chanjo ili kuweza kuwakinga na maradhi mbali mbali. Kwa mwaka 2015/16, Wizara imejipangia kuinua kiwango cha chanjo kufikia asilimia 95 kwa ngazi ya taifa na zaidi ya asilimia 90 katika kila wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba kiwango cha chanjo ya penta 3 kitaifa kimeshuka kutoka asilimia 98.8 kwa mwaka 2014 hadi asilimia 81.1 kwa mwaka 2015. Kwa upande wa chanjo ya surua, kiwango cha chanjo hiyo pia kimeshuka kutoka asilimia 97.7 kwa mwaka 2014 hadi asilimia 92 kwa mwaka 2015. Wakati huo huo asilimia ya watoto waliomaliza chanjo chini ya mwaka mmoja ilikuwa asilimia 93.1 kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 90.7 kwa mwaka 2015. Kiambatisho namba 3 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha kazi za utoaji chanjo kwa watoto, Wizara imetekeleza mikakati mbali mbali ikiwemo; mafunzo kwa watoaji wa chanjo 172 hususan katika wilaya zenye kiwango kidogo cha chanjo, uchapishaji na usambazaji wa vipeperushi 7,250 na mabango 7,500 kwa jamii na vituo vya afya. Vile vile mikutano imefanyika yenye lengo la kushajihisha viongozi kuwaelekeza wananchi juu ya umuhimu wa chanjo ili kuweza kuwafikia watoto wote katika wilaya zilizokuwa na kiwango cha chini cha uchanjaji.

Mhe. Mwenyekiti, muongozo kuhusu maendeleo ya mama mjamzito kabla ya kujifungua umeweza kufanyiwa mapitio. Muongozo huu unaelekeza huduma zinazopaswa kutolewa kwa mama wajawazito wanapohudhuria kliniki. Huduma hizo zinajumuisha kuangalia ukuaji wa mtoto tumboni na uchunguzi wa mama kwa vipimo vya malaria, VVU, sukari, wingi wa damu, minyoo na shindikizo la damu. Aidha, mama wajawazito hupewa elimu juu ya vidokezo vya hatari pamoja na lishe. Pia muongozo wa ufuatiliaji wa vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga umefanyiwa mapitio. Jumla ya wafanyakazi 70 wamepatiwa mafunzo yakutumia muongozo huo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mbinu zinazotumika katika kuhakikisha mama wajawazito wanajifungua katika vituo vya afya na hospitali Wizara imeanzisha mpango maalumu katika wilaya ya Kaskazini B ili kufikia lengo hilo. Mpango huu unatumia wafanyakazi wa jamii wa kujitolea ambao huwatembelea mama wajawazito majumbani mwao kwa lengo la kuwaelimisha juu ya masuala hayo. Jumla ya wajawazito 674 wameshaorodheshwa na wanafaidika na mpango huu tokea mradi huu ulipoanza mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano, Wizara imenunua dawa mbali mbali na vifaa tiba vya kuokoa maisha na kusambazwa katika vituo vya afya Unguja na Pemba. Sambamba na hilo, mafunzo maalum juu ya utumiaji wa miongozo ya ufuatiliaji wa vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga yametolewa kwa wafanyakazi kutoka hospitali mbali mbali za

Unguja na Pemba. Pia mafunzo ya matibabu ya magonjwa kwa uwiano kwa njia ya masafa yamefanyika kwa wafanyakazi 140 wa kada mbali mbali kutoka katika vituo vya afya kwa Wilaya zote za Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za afya kwa vijana vijijini zimefanyika katika shehia 12 za Unguja na Pemba. Mada zilizojadiliwa katika mikutano hio ni mimba za utotoni, dawa za kulevya pamoja na UKIMWI. Jumla ya vijana wanaume 1,145 na wanawake 990 walishiriki. Sambamba na hayo vijana wameweza kupatiwa vipeperushi zaidi ya 10,000 vinavyozungumzia matatizo ya afya. Vile vile jumla ya vijana 544 walichunguzwa virusi vya UKIMWI, kati yao kijana mmoja ndie aliyegunduliwa kuwa na maambukizi ya virusi hivyo.

Huduma za Ufuatiliaji wa Mienendo ya Maradhi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya imeendelea kufuatilia mienendo ya maradhi kwa kutafuta sababu zilizopelekea kutokea kwa maradhi hayo pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana nayo. Pia kukabiliana na majanga mengine ya kiafya yanayoikumba jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi yakiwemo maradhi ya Kuharisha, Surua, Kutafunwa na Wanyama, Homa ya Ini, Homa ya Matumbo, Tete Kuanga umefanyika kwa wilaya zote Kiambatisho namba 4 kinafafanua.

Mhe. Mwenyekiti, ufuatiliaji huo wa maradhi umeenda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa walimu 150 wa skuli za msingi na sekondari juu ya maradhi ya miripuko yanayoingia na yale yanayoibuka. Mafunzo hayo yanahusiana na kujenga uelewa juu ya maradhi hayo.

Huduma za Kupambana na Maradhi Yasiyoambukiza

Mhe. Mwenyekiti, maradhi yasiyoambukiza yanaonekana kuongezeka kwa kasi katika visiwa vyetu kwa miaka ya hivi karibuni. Magonjwa hayo ni pamoja na Shindikizo la Damu, Kisukari, Saratani, Ajali za barabani na magonjwa mengine sugu ikiwemo Pumu. Wizara ina jukumu la kuihamasisha jamii juu ya kujikinga na magonjwa haya kwa kufanya mazoezi, kuepuka matumizi ya pombe na tumbaku pamoja na kuzingatia ulaji bora ambao una lishe kamili.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilitoa elimu kwa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari juu ya vichocheo vinavyopelekea kupata maradhi yasiyoambukiza ukiwemo ugonjwa wa Kisukari ambapo jumla ya wanafunzi 521 (wanaume 204 na wanawake 317) walisomeshwa. Aidha, mafunzo maalumu kwa

waganga wa tiba asili juu ya usahihi wa kupima na kugundua magonjwa hayo yalitolewa. Pamoja na mafunzo hayo, waganga hao waliandaliwa mfumo wa kuwapa rufaa kwenye vituo vya afya na hospitali kwa wale ambao watawagundua na dalili za maradhi haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, huduma za afya ya akili wilayani kupitia huduma masafa (*outreach services)* zimetolewa. Jumla ya wagonjwa 1,037 (wanawake 548 na wanaume 489) walipatiwa huduma hizi karibu na sehemu wanazoishi. Vile vile wafanyakazi wa afya 25 kutoka Pemba na walimu watano kutoka Unguja wanaofanya kazi chini ya mtandao wa watu wenye ulemavu wa akili walipatiwa mafunzo ya afya ya akili ili kusaidia katika kuimarisha huduma hizi kwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa wito kwa wajumbe wa Baraza lako wote wawe na utamaduni wa kuangalia afya zao angalau mara moja kwa mwaka na kutusaidia kuzihamasisha jamii zao katika majimbo yao. Pia kuhakikisha jamii inaelewa umuhimu wa kuepukana na vichocheo vya maradhi yasiyoambukiza. Naomba kuwapongeza Wajumbe wote walokuwa wakishiriki mazoezi kwa nyakati mbali mbali ambao wamepelekea timu zote za Baraza la Wawakilishi kupata ushindi. Jitihada hizi na mazoezi haya yanatakiwa kuwa endelevu ili kujenga afya zetu na kuepuka maradhi yasiyoyakuambukiza.

Huduma za Afya ya Macho

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inaepukana na tatizo la upofu unaoepukika, jitihada mbali mbali zimechukuliwa zikiwemo kutoa huduma za upimaji wa macho pamoja na huduma za upasuaji. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2015/16 watu 19,502 walichunguzwa uoni kilinganisha na 6,534 waliochunguzwa mwaka 2014/15. Ongezeko hili limesababishwa na kuongezeka kwa huduma za uchunguzi kupitia skuli ambapo jumla ya wanafunzi 13,818 walichunguzwa, kati yao 252 (6%) waligunduliwa na matatizo na miongoni mwao 12 walipewa rufaa kwenda hospitali kwa ajili ya kufuatilia matibabu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika uchunguzi uliofanyika katika vituo vya afya Unguja na Pemba ulifanikisha jumla ya watu 5,684 kuchunguzwa. Kati ya hao 4,442 waligunduliwa na matatizo mbali mbali na kupatiwa huduma zinazofaa. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 5.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua nyengine matibabu ya macho yalitolewa kwa kufanya upasuaji kwa watoto wote ambao walibainika kuwa ipo haja ya

kufanyiwa hivyo. Kwa mashirikiano na kitengo cha matibabu ya macho cha watoto cha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kambi nne za matibabu ya pasuaji zilifanyika. Jumla ya watoto 2,089 (1,103 wanawake na 986 wanaume) walichungunzwa, kati yao, 186 walifanyiwa upasuaji (wanawake walikuwa 98 na wanaume 88). Aidha, watoto 15 (wanawake 8 na wanaume 7) walitakiwa kwenda hospitali kwa ajili ya matibabu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za matibabu ya macho mafunzo ya msingi ya matibabu ya macho kwa wafanyakazi wa vituoni yametolewa ili kuweza kuwajengea uwezo na kupanua wigo wa matibabu bora ya afya ya macho ambapo wafanyakazi wa afya 84 walipatiwa mafunzo hayo. Sambamba na hilo, mafunzo ya kuweza kuwatambua watoto wenye matatizo ya macho katika skuli kwa walimu yametolewa, ili kuweza kuwapima uoni wanafunzi na kutoa ushauri unaomlenga mwanafunzi. Aidha, mafunzo ya kuweza kutambua uambukizo wa baadhi ya maradhi ya macho yalitolewa kwa waganga wa tiba asili 62.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi za kutokomeza upofu unaoweza kuzuilika, Wizara imefanya utafiti wa maradhi ya vikope (*Trachoma*) katika wilaya mbili zinazoongoza za Kaskazini A na Micheweni Pemba. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa wilaya ya Micheweni ina maambukizi kwa asilimia 11.2 na Wilaya ya Kaskazini A imebainika kuwa na asilimia 0.21. Wilaya hizi mheshimiwa wakati wa kuchunguza, zimechunguzwa sio wanapata *Trachoma* kwa umaskini wao, lakini ni katika mazingira yao ya kuishi. Hatua inayofuata ni kufanya uchunguzi wa maradhi haya hasa katika Wilaya ya Micheweni, ambako kulionekana kuwa na tatizo kubwa zaidi. Aidha, matibabu yatatolewa kwa wale wote ambao watagunduliwa kuwa na maradhi haya. Sababu kuu iliyozungumzwa na kutajwa katika Mkutano Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, kuwa sio umaskini bali tabia ya kuishi katika mazingira yasiyokuwa masafi.

Huduma za Kupambana na Kichocho, Minyoo na Matende

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mikakati inayotumiwa na Wizara ya Afya katika kupambana na maradhi haya, ni ulishaji wa dawa za Kichocho na Minyoo katika jamii. Katika kipindi cha Julai 2015/16 ulishaji wa dawa ulifanyika ambapo jumla ya watu 735,550 sawa na asilimia (83%) walipewa dawa za kichocho na minyoo, kati ya hao jumla 889,578 waliostahiki kupewa. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuwachunguza wale waliofika katika vituo mbali mbali. Jumla ya watu 1,551 walichunguzwa kichocho katika kituo cha Mianzini, kati yao 1,114 (72%) hao waliochunguzwa waligunduliwa na

maradhi hayo. Kwa upande wa maradhi ya matende jumla ya watu 132 walichunguzwa na hakukuwa na yeyote aliyegunduliwa na maradhi haya. Lakini nashukuru sana kwamba tumeweza kufanikiwa zaidi kwenye masuala ya kupiga vita maradhi ya matende.

Mhe. Mwenyekiti, mkakati mwengine unaotumiwa na Wizara katika kupambana na maradhi haya ni kufanya ukaguzi wa mito, maziwa na mabwawa. Yaliyokuweko katika maeneo mbali mbali katika kulifanikisha hili, taarifa mbali mbali za kimazingira ambazo zinapatikana katika vianzio hivyo hunakiliwa, taarifa hizi zinatoa mwenendo mzima wa mazalio ya makonokono na tabia zao katika sehemu husika. Katika kipindi cha mwaka 2015, jumla ya vianzio vya maambukizi ya maradhi ya Kichocho 56 vilikaguliwa. Aidha, vianzio 35 vya makonokono vilinyunyiziwa dawa ya "*Niclosamide*" ambayo haina athari za mazingira. Kupitia Mkutano Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, makubaliano yaliyofikiwa ni lazima kwa jamii zetu zibadilishe tabia na mwenendo wao wa asili wa kutumia mito na madimbwi kwa kufanyia haja zao ndogo na kubwa. Tutakapoweza kulitimiza hili, kichocho kitakuwa historia tu kwa Zanzibar.

Huduma ya Elimu ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya vipindi 75 vya elimu ya afya vilitolewa kupitia redio na televisheni. Vipindi hivyo vilitoa elimu juu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza. Vile vile utoaji wa elimu ya afya ulifanyika katika skuli 21, mikutano ya kupita nyumba kwa nyumba (100), uoneshaji wa filamu (30) na uchapishaji na usambazaji wa vijarida na vipeperushi 212,606 ulifanyika. Vipindi na vipeperushi hivyo vilizungumzia jinsi ya kujikinga na maradhi yakiwemo ya Kipindupindu pamoja na maradhi mengine ya kuharisha. Aidha, wananchi walipata maelekezo juu ya kujikinga na maradhi ya macho na masikio. Kwa upande mwengine uimarishaji wa afya ya mazingira, lishe bora, afya ya mama na mtoto, athari ya tindi kali na chokaa pia ulielezwa kupitia vipindi hivi.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya afya na mikutano ya kushajihisha jamii juu ya ugonjwa wa Ukoma imefanyika. Jumla ya vijiji 24 vya Unguja na Pemba vilifanyiwa mikutano hiyo na kupatiwa elimu ya Ukoma. Jumla ya watu 1,280 (Unguja 805, Pemba 475) walihudhuria mikutano hiyo.

Huduma za Afya Bandarini

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi wa usafi wa mazingira umefanyika katika eneo la bandari ya abiria na katika mikahawa saba na vioksi vitano. Miongoni mwa mapungufu yaliyobainika ni pamoja na kuziba kwa michirizi ya maji taka ama maji machafu, ubovu na uchakavu wa vyoo, ukosefu wa vifaa vya usafi, kukosekana kwa uchunguzi wa afya za wafanyakazi na kutoridhisha kwa hali ya usafi wa maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kontena 16 za nguo za mitumba na 34 za vifaa vya majumbani vilivyokwishatumika zilikaguliwa yaani. Jumla ya kontena tano za nguo za ndani zilirudishwa zilikotoka na tani 33,000 zimeangamizwa. Aidha, tani tano za nguo zilifukizwa katika bandari ya Zanzibar baada ya kuonekana kidogo kuna kasoro ndani yake. Sambamba na hilo ukaguzi wa vyombo vya usafiri vipatavyo 2,506 vilivyoingia nchini ulifanyika. Tunawaomba wafanyabiashara kuepuka kuagiza nguo za ndani kwani mara nyingi zinaweza kutusababishia gharama kubwa katika upande wa matibabu na tunawaomba wale wananchi wote wajaribu kuepuka kununua nguo za ndani za zilizotumika.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za chanjo ziliendelea kutolewa kwa kufanya ukaguzi wa chanjo ya homa ya manjano kwa wasafiri kupitia bandarini na uwanja wa ndege. Katika ukaguzi huo abiria 131,607 walikaguliwa (71,506 uwanja wa ndege na 60,101 bandarini). Matokeo ya ukaguzi huo yalibainisha kwamba abiria 904 hawakuwa na chanjo ya homa ya manjano, abiria 690 walikuwa na sababu za kiafya na abiria 80 walichanjwa hapo hapo bandarini. Aidha, chanjo kwa wasafiri wa kimataifa 1,313 zilitolewa ukilinganisha na wasafiri 1,052 waliochanjwa mwaka 2014/15. Kati ya hao wasafiri 641 walichanjwa homa ya manjano, 338 homa ya uti wa mgongo na 334 walichanjwa homa ya ini.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za kuchunguza afya za wafanyakazi, hususan katika maeneo ya biashara ya vyakula zimefanyika kwa ufanisi mkubwa na naomba niseme mbele ya Baraza lako tukufu kwamba hili ni zoezi endelevu na na linaendelea.

Kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016. Jumla ya wafanyakazi 6,284 walifanyiwa uchuguzi wa afya, kati yao 85 waligundulika na maambukizi ya njia ya mkojo, 61 shindikizo la damu, wanne homa ya ini, 56 minyoo, 16 uoni hafifu na tisa walikuwa na matatizo ya masikio. Wote waliogundulika na matatizo walipelekwa kwa madaktari husika na kupatiwa matibabu.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi wa maiti 132 na wagonjwa 165 kupitia bandarini na uwanja wa ndege umefanyika. Ukaguzi huo umeonesha kuwa wagonjwa 18 walikuwa na maradhi ya kuambukiza yakiwemo Malaria (3), kuharisha (15) na maradhi yasiyo ya kuambukiza (144).

Huduma ya Afya ya Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanatumia maji safi na salama, uchunguzi wa uwepo wa dawa ya kutibu maji katika jamii na taasisi mbali mbali ulifanyika. Jumla ya sampuli 60 zilichukuliwa, kati ya hizo 34 (57%) zilionekana kuwa na kiwango cha kutosha cha *chlorine* na 26 (43%) hazikuwana kiwango cha kutosha za *Chlorine* ama hazikuwa zimetibiwa. Vile vile jumla ya vidonge 1,952,901 vya dawa za kutibu maji *(water guard)* ziligawiwa kwa wananchi mbali mbali majumbani, katika vituo vya afya, mashuleni, maskani za vijana, madrasa pamoja na kambi za wagonjwa wa Kipindupindu.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kuripuka kwa maradhi ya kipindupindu mafunzo ya namna ya kujikinga na maradhi haya yalitolewa kwa washiriki 487 kutoka taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za serikali ili waweze kutoa elimu ya kujikinga kwa jamii moja kwa moja tunawashukuru wale wote waliojitolea katika kupata elimu hiyo na kutusaidia sisi upande wa Wizara ya Afya pamoja na wafanyakazi wetu kufikisha elimu hiyo moja kwa moja kwa jamii ya Zanzibar. Mafunzo mengine yalitolewa kwa kina mama na baba lishe 200 juu ya kuandaa chakula na kukitunza kwa kuzingatia kanuni za afya na kuhakikisha mazingira wanayofanyia kazi ni salama muda wote kwa wateja wanaowahudumia.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali haikuwa na nia ya kuwafunguia wananchi biasharazao ama kupata rizki zao, ia iliyokuwepo katika Serikali ni moja kwa moja kuwashajihisha ili washiriki katika mafunzo haya waweze kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wao bila ya kusababishia gharama kubwa za afya kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Serikali yao wananchi wote. Sambamba na hilo muongozo wa Maji na Usafi wa Mazingira na Udhibiti wa Maambukizi Wakati wa Utoaji wa Huduma za Afya umetayarishwa. Wafanyakazi 64 Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo ya namna ya kutumia muongozo huo wakati wa utoaji wa huduma.

Huduma za Lishe

Mhe. Mwenyekiti, kampeni ya utoaji wa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 59 ulifanyika. Matokeo yanaonesha kwamba asilimia ya watoto waliopewa matone ya vitamin A imepungua kutoka asilima 104.6 mwaka 2014 hadi asilimia 76 mwaka 2015 na dawa za minyoo imepungua kutoka asilimia 107.5mwaka 2014 hadi asilimia 76 mwaka 2015. Sababu kubwa iliyopelekea kushuka kwa kiwango hiki zinakisiwa kuwa, mwaka 2015 matone ya vitamin A na dawa za minyoo yalitolewa wakati wa kampeni jumuishi ya utoaji wa chanjo ya Surua Rubella ambapo kulikuwa na uhamasishaji mkubwa uliohusisha matumizi makubwa ya vyombo vya habari, mikutano ya jamii na utoaji wa vipeperushi. Kwa hivyo kwa mantiki ukiangalia kwamba asilimia hii haikupungua haswa kama ilivyoelezwa hapa bali ilitolewa pamoja na chanjo nyenginezo, hasa hii chanjo ya surua na Rubella.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya afya pamoja na Shirika la Afya Ulimwenguni Umoja wa Mataifa inatilia mkazo unyonyeshaji wa mtoto bila kupewa chochote hadi miezi sita ya awali, tuna tabia sisi watoto huwa tunachanganyisha na mambo mengine ya ulezi na nini, sasa hili linakatazwa na kuna sababu maalum ya kiafya ambalo hili linakatazwa mtoto miezi sita ya mwanzo awe anatumia maziwa ya mama tu ikiwezekana.

Kwa kushirikiana na Kamisheni ya Kazi, Wizara imefanya maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji kitaifa tarehe 1-7 Agosti, 2015 katika wilaya ya Mkoani, Pemba. Kauli mbiu ikiwa ni "*UNYONYESHAJI NA KAZI INAWEZEKANA".* Hapa imekusudiwa yaani mama ambae anafanya kazi au ni muajiriwa ikiwa Serikalini ikiwa katika sekta binafsi anaweza kumnyonyesha mtoto wake pia katika muda huo wa kazi ni kujipanga tu.

Jambo jengine lililofanyika ni uhimizaji wa utumiaji wa chumvi yenye madini joto ili kuepukana na maradhi ya goita, hivyo Wizara iligawa kilo 200 za *"Potassium Iodate"* na kuisambaza kwa wakulima wa mashamba ya chumvi kwenye maeneo ya Pujini, Minungwini, Mchanga Mdogo na Shengejuu ambako kumeonekana kuwepo kwa matumizi ya chumvi isiyo na madini joto. Tatizo hili linaonekana zaidi kwa upande wa Pemba.

Huduma za Afya Wilayani

Mhe. Mwenyekiti, huduma za afya wilayani zinatolewa kupitia Timu za Afya za Wilaya ziliopo Unguja na Pemba. Timu hizi zina jukumu la kusimamia utekelezaji wa huduma mbali mbali za afya zinazotolewa katika vituo vya afya.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia mripuko wa ugonjwa wa Kipindupindu, kazi za kueleimisha jamii juu ya umuhimu wa usafi ili kujikinga na maradhi hayo zimefanyika katika skuli, mikutano ya kijamii katika maeneo mbali mbali ya wilaya zote Unguja na Pemba. Aidha, shughuli za kufuatilia na kuhimiza usafi kwa kutumia sheria ya afya ya jamii na mazingira namba 11 ya mwaka 2012 ilifanyika katika maeneo ya biashara ikiwemo, hoteli, migahawa, vioski, masoko na katika makaazi ya watu. Msisitizo ukiwa ni utumiaji wa vyoo, kuosha mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni kwa maji ya mtiririko, kuwepo karo na mazingira ya usafi kwa ujumla.

Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote jumla tumeshirikiana pamoja katika kulitekeleza jukumu hili hasa pale tulipokuwa tuna maradhi ya kipindu pindu, lakini niwashukuru sana wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa kuchukua jukumu hilo zito la kukabiliana na maradhi ya kipindupindu ambayo sasa tunaweza kusema kwamba yanaendelea vizuri. Lakini pia naomba nichukue shukurani za pekee kwa wananchi wote waliotupa mashirikiano yao makubwa hadi kuweza kupigana kwa sababu hivi ni vita vyetu sote kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, amri ya kupiga marufuku kwa biashara zote za chakula kilichotayari kuliwa katika maeneo ambayo ni hatarishi ililazimika kutumika katika kupambana na maradhi hayo kwa mujibu wa sheria sio kumuonea mtu. Juhudi hizi pamoja na nyenginezo zilizochukuliwa na Wizara pamoja na taasisi nyengine za serikali zimewezesha kupungua kwa maradhi hayo kwa kiasi kikubwa kutoka wagojwa wapya 15 hadi 33 kwa siku katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Machi na wiki tatu za mwanzo za mwezi wa Aprili na kufikia wagonjwa wanne tu hadi sufuri kwa siku katika mwezi wa Mei, 2016. Naomba tusijipweteke kwa sifa hizi. Kwa ujumla hadi kufikia 10 Juni 2016, wagonjwa 4,213 (Pemba 1,613 na 2,600 Unguja) waliugua maradhi ya kipindupindu, kati yao 66 (49Unguja na 17 Pemba) walifariki dunia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na wananchi wizara imekamilisha ujenzi wa vituo vya afya vya Kinuni, Bumbwisudi, na Ukongoroni na nyumba ya wafanyakazi wa kituo cha afya Kiongwe. Aidha, matengenezo madogo madogo ya vituo vya afya yamefanywa

ikiwa ni pamoja na uwekaji wa umeme katika vituo vya afya Makoongwe na Kisiwa Panza. Vile vile, vituo vya afya Ukunjwi, Jadida, na Mjini Kiuyu vimewekewa mifumo mipya ya maji na umeme, nakumbuka Mhe. Mwakilishi mmoja alizungumzia sana suala la maji katika bajeti wizara iliyokuwa nyengine, kwa hivyo naomba ka sentensi hii tuendelee ilikuwa Mhe. Gerei, tuendelee kumjibu kuwa zoezi hilo ni endelevu na linaendelea matengenezo ya dari na waya za madirisha pia nalo linaendelea, pamoja na kuweka mifumo mipya ya maji na umeme kadri ya uwezo wa kifedha tunapopata.

Mhe. Mwenyekiti, matengenezo mengine yaliyofanywa ni kuweka umeme wa jua katika nyumba za wafanyakazi na vituo vya afya vya Kijini na Nungwi, kuweka tangi jipya la maji katika kituo cha afya cha Fuoni, miundo mbinu ya maji na umeme katika vituo vya afya Donge Vijibweni na matengezo makubwa yamefanywa katika kituo cha afya Bumbwini Misufini.

Kila pale tunapoendelea kupata bajeti hivi sasa ofisini kwangu kuna bajeti kubwa sana ya vituo hivi vya afya vya kwenye wilaya mbali mbali, kila tunapoendelea kupata uwezo tunaendelea kuzungumza na wafadhili mbali mbali kuendelea kuwashajihisha wao, ili kuweza kushirikiana pamoja, ili tuweze kulifikia lengo hilo naomba Wawakilishi walitambue kwamba tutaendelea kulitimiza jukumu hilo.

PROGRAMU NAMBARI 2: HUDUMA ZA TIBA

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Huduma za Tiba inahusika na utoaji wa huduma za matibabu katika hospitali nne za vijiji na tatu za wilaya. Lengo kuu la program hii ni kuimarisha utoaji wa huduma bora zenye viwango na ufanisi katika ngazi zote za hospitali pamoja na huduma za tiba katika kiliniki maalumu zilizomo katika hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za matibabu ya wagonjwa wa nje *(Out Patient)* pamoja na kliniki maalum ziliendelea katika Hospitali za Chake Chake, Abdalla Mzee, Wete, Micheweni, Vitongoji, Makunduchi na Kivunge. Taarifa za wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki zinaonekana katika kiambatanisho namba 6 na 7.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea kutumia mikakati mbali mbali katika kuhakikisha mama wajawazito wanajifungua hospitalini au katika vituo vya afya chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya wajawazito 8,892 walijifungua, kati ya hao 8,303 walijifungua kwa njia ya kawaida na 589 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Aidha, akina mama 32

walifariki dunia kutokana na sababu mbali mbali zinazosababishwa namatatizo ya uzazi, angalia kiambatisho namba 8.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi nyengine za serikali na zisizo za serikali kupambana na tatizo la udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mwaka 2015/16 jumla ya watu 1,914 waliripoti katika vituo sita vya kutoa huduma za mkono kwa mkono Unguja na Pemba. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatisho namba 9.

Mhe. Mwenyekiti, programu ya tiba pia inahusika na upelekaji wagonjwa nje ya nchi baada ya kufanyiwa tathmini na timu ya madaktari wetu waliopo Mnazi Mmoja chini ya bodi ya madaktari. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 jumla ya wagonjwa 448 walifanyiwa tathmini. Kati yao wagonjwa 159 walisafirishwa nje ya nchi na wengine walipelekwa Tanzania Bara. Jumla ya Tsh. 2,168,648,606 zilitumika kusafirisha wagonjwa hao.

Mpango wa Damu Salama

Mhe. Mwenyekiti, uhamasishaji wananchi juu ya uchangiaji wa damu kwa hiari umeweza kuendelea kwa mafanikio. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, Wizara ilipanga kukusanya *"Unit"* 10,500 za damu kutoka kwa wachangiaji wa hiari, hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya '*units'* 6,575 (62%) zilikusanywa. Kama ilivyo kawaida, damu hiyo imefanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya *UKIMWI*, Kaswende na Homa ya Ini kabla ya kusambazwa katika hospitali mbali mbali Unguja na Pemba. Ununuzi, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa, Zana na Vifaa Tiba pia hufanyika pia kwa ajili ya uchunguzi wa damu hiyo na kuhakikisha iko salama.

Mhe. Mwenyekiti, huduma ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji dawa, zana na vifaa tiba zinahakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya dawa hizo. Katika kulifikia lengo hili, Afisi ya Mfamasia Mkuu imepewa dhamana ya kuratibu ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Aidha, Afisi hiyo ina jukumu la kufanya ukaguzi kwenye Hospitali na Vituo vya afya, ili kuhakikisha utunzaji bora na utumiaji sahihi wa dawa na kujua thamani ya dawa na vifaa vyote vilivyosambazwa.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuondoa kabisa tatizo la uhaba wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, jumla ya shilingi bilioni 7.2 zilihitajika. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, jumla ya Tsh. bilioni 1.357 sawa na asilimia 30 tu

zilitumika kwa ununuzi wa dawa, zana na vifaa tiba kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ndio zilizopatikana kati ya Tsh. bilioni 4.336 zilizoidhinishwa katika bajeti hiyo. Kwa upande wa washirika wa maendeleo, jumla ya dawa na vifaa tiba zenye thamani ya Tsh. milioni 749.545 zilipokelewa yaani chini ya bilioni moja bado. Ufafanuzi unapatikana katika kiambatisho namba 10. Licha ya juhudi za serikali za kuhakikisha dawa muhimu zinapatikana, bado Wizara inakabiliwa na deni kubwa ambalo hadi kufikia Machi 2016 jumla ya Tsh bilioni 1.156 hazijalipwa kwa wale ambao wameshatuhudumia dawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu na Wizara ya Afya nzima jambo hili la kutafuta dawa tunalifanyia kazi kwa upana wake wote na pia tunawashajiisha wajumbe wote tuungane nao katika kufanya mazungumzo mbali mbali na katika huo utaratibu unaokuja tunakuwa tunawaalika, ili kuweza kushiriki nao Kamati yetu ya Afya na Ustawi wa jamii katika mazungumzo mbali mbali ambayo tunaendelea kupigiga debe kupata fedha nyingi zaidi za dawa husasan dawa muhimu yaani *essential drug list*.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeanzisha mfumo wa kieletroniki wa kukusanya taarifa za dawa, zana na vifaa tiba (*Electronic Logistical Management Information System, e-LMIS).* Mfumo huu wa kisasa umeshawekwa katika ofisi za Timu za Wilaya zote pamoja na vituo vyote vya Wilaya ya Chake Chake na vituo vinavyotoa huduma za tiba ya ugonjwa wa UKIMWI *(HIV Care and treatment Centres).* Mfumo huu unarahisisha Hospitali na Vituo vya Afya, kuagiza dawa kwa kupitia mtandao pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi ambazo zinaonekana moja kwa moja katika Ofisi ya Mfamasia Mkuu. Lengo la Wizara la kusambaza mfumo huu katika vituo vyote mara tu Komputa na mtandao zitakapopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, lengo hasa la mfumo huu ni kwamba tusipeleke dawa sehemu ambazo hazihitajiki kwa ziada, tuwe tunahakikisha tunapeleka dawa kwa wakati na pale zinapohitajika zaidi. Moja ya kazi inayofanywa na Wizara ni kufanya ufuatiliaji juu ya uhifadhi, upatikanaji na matumizi mazuri ya dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya vyake vyote. Katika kipindi cha mwaka 2015/16 Wizara imebaini kuwa asilimia ya vituo vya afya vinavyohifadhi dawa kiusahihi kwa mujibu wa miongozo imeongezeka kufikia asilimia 94. Hata hivyo kiwango cha upungufu wa dawa muhimu umeongezeka kutoka asilimia 55 hadi asilimia 71.

Mhe. Mwenyekiti, katika mkakati wa kupunguza uhaba wa dawa serikali imeanzisha mfuko maalumu wa dawa *(Essential Medicine Account)* ili kutoa

fursa kwa watu binafsi, washirika wa maendeleo na hata asasi zisizo za kiserikali kuitumia akaunti hii kutoa michango yao kwa upande wa dawa. Nachukua fursa hii kuwakaribisha kwa yoyote mwenye nia ya kuchangia kwa maslahi ya nchi yetu kutumia account hii ya *Essential Medicine Account.*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za usambazaji dawa na vifaa tiba, Wizara inaendelea kuimarisha mfumo wa usambazaji kulingana na mahitaji *(Pull system)* katika vituo vyote vya afya 150 Unguja na Pemba, ambapo mahitaji halisi ya dawa na vifaa tiba hubainishwa na kituo cha afya kupitia Wilaya husika.

Udhibiti wa Kemikali, Dawa, Vifaa tiba, Chakula na Vipodozi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa huduma za kitaalamu na za kisayansi kwa kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka taasisi tofauti vikiwemo vile vinavyohusiana na makosa ya jinai, vinasaba pamoja na sumu. Pia, wakala wa Mkemia huhusika na udhibiti wa kemikali kwa kufanya ukaguzi na usajili wa kemikali, wadau wa kemikali na majengo yanayotumika kwa shughuli za kemikali. Aidha, kupitia Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi Wizara ina jukumu la kuhakikisha kwamba chakula, dawa na vipodozi vinavyoingizwa nchini vina ubora wa hali ya juu kabisa unaotakiwa na ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara pia ina jukumu la kusimamia na kusajili waganga wa kienyeji, vilinge, maduka ya dawa na Kliniki za tiba asili na tiba mbadala, pamoja na kudhibiti matangazo yanayokwenda kinyume na sheria ili kusaidia maendeleo ya shughuli za tiba asili kwa kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hapa nitaeleweka yaani pamoja na yale matangazo kusema kwamba unaponyesha maradhi yote wakati huwezi kuponyesha maradhi yote.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2015 – Machi, 2016 jumla sampuli 1,528 zikiwemo 1,292 za chakula, 73 za vipodozi na 163 za dawa za mitishamba zilichunguzwa. Katika uchunguzi huo Wizara ilibaini ni sampuli mbili tu za chakula ndio zilionekana hazifai kwa matumizi ya binadamu. Sambamba na hilo, jumla ya tani 339.2 na lita 200,000 za bidhaa za Chakula na tani nane za bidhaa za dawa na vipodozi zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zilizokamatwa wakati wa ukaguzi ziliteketezwa.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya maeneo 1,501 sawa na asilimia 93.8 ya maeneo 1,600 ambayo Wizara ilijipanga kuyakagua yanayoendesha biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yamekaguliwa. Katika ukaguzi huo hatua mbali mbali zilichukuliwa kwa waliobainika na kasoro zikiwemo kupewa elimu ya usajili wa biashara zao, kupewa muda wa kuweka bidhaa katika mpangilio mzuri, kusafisha maeneo yao ya biashara na hata kuchukuliwa hatua za kisheria**.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuangalia ubora na usalama wa chakula na dawa zinazozalishwa ambazo zinaingizwa nchini, Wizara imefanikiwa kukagua viwanda vinavyozalisha bidhaa nje ya nchi *(GMP inspection)* ambapo jumla ya viwanda 13 (vya vyakula 5 na dawa 8) viliweza kutembelewa na kukaguliwa na wataalam wetu. Nchi hizo ambazo wataalamu wa Wizara wamekwenda na kukagua hivyo viwanda pamoja na hivyo vyakula ni Marekani, China, India, Moroco na Oman. Kwa hivyo, vyote vile vinavyoletwa kutoka nchi hiyo ambavyo vimeshapata ukaguzi wetu kwa hapa Zanzibar ni salama. Vilivyokuwa havijapata ukaguzi wetu hivyo lazima vikaguliwe si salama mpaka vikaguliwe.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ilisajili jumla ya maeneo 1,197 ya biashara za chakula, dawa na vipodozi, bidhaa 4 za dawa, bidhaa 28 za chakula. Aidha, Bodi iliweza kuwasajili waingizaji chakula 65, wasafirishaji chakula 22, wafamasia 15 na wafamasia wasaidizi 51.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya udhibiti wa kemikali zinazotumika majumbani na viwandani imeanza rasmi katika mwezi wa Disemba 2015 baada ya kukamilika kwa kazi ya matayarisho ya kanuni ya kemikali. Kazi ya ukaguzi na usajili wa kemikali, wadau wakemikali na majengo yanayotumika kwa shughuli za kemikikali nayo pia imeanza. Katika kulisimamia hilo ukaguzi umefanyika katika maeneo yakiwemo bandari, viwandani na maghala, pia mbali na hayo usajili wa wajasiri amali, wazalishaji na wasafirishaji pia umefanyika. Pia, maabara imefanikiwa kutoa vibali vya kuingiza kemikali 317 nchini hadi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, uchunguzi wa vielelezo 271 ambavyo vinatoka Jeshi la Polisi, taasisi mbalimbali pamoja na watu binafsi umefanyika. Ufafanuzi wa uchunguzi huo unaonekana katika kiambatisho namba 11. Matokeo ya uchunguzi wa vielelezo vingi kati ya hivyo hutumika kama ni ushahidi katika kesi mbali mbali zinazoendeshwa katika Mahakama mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za maabara ya Mkemia Mkuu Wizara imekamilisha hatua zote za zabuni na kumpata mkandarasi wa ujenzi wa maabara. Kwa sasa kazi ya ujenzi inaendelea kufanyika ambapo msingi na nguzo tayari zimeshasimamishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala imesajili jumla ya waganga 298, vilinge 165, wasaidizi waganga 47, kliniki 29 na maduka ya dawa za asili 61. Aidha, vituo vinne vilifungiwa kutoa huduma kutokana na kukiuka maadili ya utoaji wa Tiba Asili na Tiba Mbadala na viwili vilitoleshwa faini kwa kukiuka maadilin hayo.

Usimamizi wa Hospitali Binafsi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Hospitali Binafsi ina jukumu la kusimamia uanzishaji wa hospitali binafsi pamoja na utekelezaji wa sheria namba 4, ya mwaka 1994 ya kusimamia uendeshaji wa hospitali binafsi. Katika kutekeleza majukumu hayo, jumla ya vituo na hospitali binafsi 68 (Unguja 58 na Pemba 10) vilipatiwa vibali vya kuendesha huduma kwa mwaka 2015/16. Vile vile ukaguzi wa hospitali binafsi uliendelea kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Jumla ya vituo na hospitali binafsi 68 vimekaguliwa, kati ya hivyo vituo 12 vilipewa onyo kali sana baada ya kukutikana na kasoro kadhaa na vituo 10 vilichukuliwa hatua ya mara moja kwa kusimamisha kwa muda kutoa huduma hizo.

Usajili na Uratibu wa Wauguzi na Wakunga

Mhe. Mwenyekiti, kuzingatia maadili kazini kwa wauguzi na wakunga ni jambo linalotiliwa mkazo mkubwa sana. Maana mkunga au muuguzi asipokuwa na usajili anafanya kazi kinyume cha sheria. Kwa mantiki hiyo, Baraza la Wauguzi na Wakunga limetengeneza mwongozo na kanuni za maadili wakati wote wa utoaji wa huduma za uuguzi. Aidha, utayarishaji wa mipaka ya kazi za Wauguzi na Wakunga pamoja na kanuni ya sheria ya Baraza la Wauguzi na Wakunga imekamilika. Naomba niwapongeze sana kwa kazi hiyo nzito waliofanya Baraza hilo. Mategemeo yetu makubwa kwa upande wa Wizara kanuni hizo zitasaidia sana katika kurudisha hadhi na taswira ya Uuguzi na Ukunga hapa Zanzibar pia na kupunguza lawama kubwa tunazozipata kupitia Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwa Wawakilishi wanapolalamika pale kutokana na lugha na mambo mengine ya kimaadili. Jumla ya wauguzi na wakunga 147

tayari wameshasajiliwa katika kipindi cha Agosti, 2015 hadi Machi, 2016. Onyo kali la kisheria limetolewa kwa kuhakikisha kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, mwisho wa bajeti zetu hizi maana bajeti mpya inaanza tarehe 1 Julai, kama kutakuwa na muuguzi anayefanya kazi hospitali yoyote iwe ya serikali iwe ya binafsi, hala leseni ya Uuguzi itakuwa sawa na dereva gari bila ya leseni atakuwa anafanya kazi kinyume na sharia na atastahiki kuchukuliwa hatua za kali sana za kisheria ikiwemo kusimamishwa kazi na hatua nyenginezo. Nadhani onyo hilo lishafika kwa wahusika.

Huduma za Kupandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Vijiji

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa kupandisha hadhi hospitali za vijiji kuwa za wilaya na wilaya kuwa za mkoa kwa kuimarisha majengo na kuongeza huduma, vifaa na rasilimaliwatu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, ujenzi wa hospitali ya Abdalla Mzee umekamilika kwa asilimia 90 na tunatarajia kukabidhiwa rasmi ifikapo mwezi wa Septemba mwaka huu. Kwa wale Wawakilishi wanaotokea Kisiwa cha Pemba watakuwa walitembelea eneo hili na kuona hali iliyofikia hospitali hii ya Abdalla Mzee. Kukamilika kwa ujenzi huo kutafanikisha kupatikana kwa jengo la Ofisi, jengo la huduma za dharura, jengo la huduma za wagonjwa wa nje, jengo la huduma za uchunguzi (Maabara, *X-ray*, *CT–Scan* na *Ultra-Sound*), jengo la kuhifadhi dawa na vifaa tiba, wodi ya wagonjwa mahututi na vyumba vinne vya upasuaji na wodi nyenginezo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa wodi ya wanawake na wanaume katika Hospitali ya Micheweni na ukarabati wa nyumba za madaktari katika hospitali hiyo umekamilika. Sambamba na hilo, ujenzi wa chumba cha upasuaji katika Hospitali hiyo ya Micheweni uko kwenye hatua za mwisho. Jumla ya Tsh. Milioni 36 kutoka Serikalini zimetumika. Aidha, ujenzi wa wodi mbili za wanaume na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Kivunge nao pia umekamilika. Mhe. Mwenyekiti, changamoto yetu kuu kwa upande wa wizara sasa itakuwa ni kutafuta wafanyakazi mahiri na wa kutosha kwa ajili ya huduma hizo zitakapoanza huko Kisiwani Pemba.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kuu la idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa hasa wale wa rufaa kutoka katika vituo

vya afya, hospitali za vijiji na hospitali za Wilaya ziliopo nchini. Huduma hizi hutolewa katika hospitali zake ambazo ni Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Hospitali ya wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu. Maana Mnazi Mmoja inafanyika kwa hospitali tatu, yaani Mnazi Mmoja yenyewe, Muembeladu na Kidongo chekundu Hospitali hizi pia hutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kada za afya wanaotoka katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Idara imekuwa ikitekeleza programu kuu mbili ambazo ni programu ya huduma za uchunguzi na matibabu na programu ya pili ni ya uongozi wa hospitali na utawala.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA MWAKA 2015/2016 YA UCHUNGUZI NA MATIBABU

Mhe. Mwenyekiti, program ya uchunguzi na matibabu imetekeleza kazi zifuatazo:-

Mhe. Mwenyekiti, ya kwanza kabisa katika juhudi za kupunguza idadi ya wagojwa kupelekwa nje ya nchi, Idara imeendelea kuendesha kambi mbali mbali za matibabu, jumla ya kambi 13 zimeendeshwa zikiwemo kambi mbili za *Plastic Surgery*, *Paediatric Surgery* moja na kambi tisa za *Neuro Surgery*. Katika kambi hizo jumla ya wagojwa 875 walihudumiwa na madaktari bingwa tofauti na kutoka sehemu mbali mbali na kupewa matibabu stahiki, kati yao 250 walifanyiwa upasuaji mkubwa hapa kwetu Zanzibar. Huduma hizi zimeleta faraja kwa wananchi na kuipunguzia mzigo mkubwa serikali mzigo wa gharama za kusafirisha wagonjwa kwenda nchi za nje pamoja na nchini India. Tunawashukuru wale wote, wale madaktari wetu wa meli kutoka Spain wakiongozwa na Profesor Hozei Piker na wafanyakazi wetu wote wa Wizara ya Afya hasa kitengo kile *Neuro Surgery* kwa kufanya kazi hii kwani wamekuwa wakiipunguzia serikali yetu gharama kubwa sana ni kwenye mabilioni huko wanaipunguzia. Tulikuwa tunajaribu kupiga hesabu ya haraka haraka tu zaidi ya bilioni 2 hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za uchunguzi ni sehemu muhimu sana inayomsaidia daktari kuweza kuelewa maradhi ya mgonjwa ili kuweza kumpa matibabu anayostahiki. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 jumla ya vipimo vya uchunguzi 79,061 vilifanyika katika hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake. Haya yanakwenda sambamba na wale wanaosema huduma za maabara hazipo lakini huduma hizi zimetolewa kwa idadi hiyo niliyoitaja ya 79,061. Vipimo hivyo vinajumuisha uchunguzi wa *X-ray* (13,897), *CT-Scan* (4,338), *Ultra-Sound* (14,787), *blood transfusion* (5,440), uchunguzi wa sampuli za vimelea

vinavyoishi kwenye maji (40), *mortuary* (202) na vipimo vyenginevyo vya maabara ya afya (40,357).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/16, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanzisha kliniki maalum kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa saratani na wale wanaoshukiwa kuwa na maradhi hayo ya saratani. Uanzishaji wa huduma hii ulioanza Februari 2016 umewezekana baada ya kurejea masomoni daktari wetu bingwa pekee tuliyenaye, mzalendo wa maradhi ya saratani. Leo tumemualika hapa yupo juu mtamuona baadae kwa wale watakaotaka kumuona. Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wagonjwa wa saratani 150 walihudumiwa na kupewa ushauri na matibabu yaliyowezekana tokea kliniki hiyo ilipoanzishwa. Hapo kabla Mhe. Mwenyekiti, wagonjwa hawa wote wanakwenda *Ocean Road* Dar-es -Salaam lakini hivi sasa tumeweza kutoa baadhi ya huduma hizo, hatua kwa hatua tutafika. Wagonjwa 20 kati yao walipewa rufaa kwenda Tanzania Bara kwa matibabu zaidi na wengine wote kupata matibabu hapa hapa Zanzibar. Ni nia ya wizara kuendelea kuziimarisha huduma hizi hatua kwa hatua kwa kila uwezo unapopatikana ili tuweze kufikia lengo ya sisi pia kuwa na kituo chetu wenyewe cha saratani tukawa hatuna haja ya kwenda kwa wenzetu, twende kule pale inapobidi tu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imelitekeleza kwa ukamilifu agizo la serikali la kufuta uchangiaji katika huduma za *X-ray, Ultra-Sound* na *CT-Scan* na huduma hizo sasa zinatolewa bure kwa wananchi wote. Maamuzi haya yamewawezesha wananchi wenye kipato cha chini nao pia kuweza kutumia huduma hizo pale inapohitajika. Hali hii imepelekea kuongezeka sana kwa wagonjwa waliohudumiwa katika huduma hizo ambapo wastani wa wagonjwa 374 hupatiwa huduma za *CT-Scan* kwa mwezi ukilinganisha na wastani wa wagonjwa 120 hapo kabla kwa hiyo ongezeko hilo linaonekana wazi kutokana na kwamba huduma hizi kutokuwa na malipo. Kabla ya tangazo hilo la serikali wagonjwa hao wameongezeka zaidi ya mara mbili.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa, kliniki maalum na waliojifungua katika katika Hospitali ya Mwembeladu, Mnazi Mmoja na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu inaonekana katika kiambatisho 12 hadi 13.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA UTAWALA

Mhe. Mwenyekiti, katika kutimiza azma ya kuifanya hospitali hii kuwa ni taasisi yenye kujitegemea, wizara iliwasilisha waraka wenye lengo hilo ambao ulijadiliwa na kupitishwa katika vikao vyote stahiki vya serikali kuanzia

Makatibu Wakuu mpaka kikao cha Baraza la Mawaziri. Pia rasimu ya sheria ya kutekeleza lengo hilo imeshatayarishwa tayari na kuwasilishwa katika Baraza hili katika kikao hiki kinachoendelea na imo katika ratiba nadhani ni tarehe 27.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeendeleza mashirikiano na taasisi mbali mbali ulimwenguni za Kimataifa ikiwemo hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland Norway kwa nia ya kubadilishana wataalamu na kwa lengo la kupata ujuzi wa utoaji wa huduma za afya. Kwa mwaka huu wa fedha jumla ya wafanyakazi nane waliweza kupata fursa hiyo. Vitengo vilivyohusika na mafunzo hayo ni wodi ya watoto, kitengo cha afya ya akili na kitengo cha matibabu ya ndani (*Internal Medicine*). Naomba tutoe shukurani zetu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Huekland cha nchini Norway kwa msaada wao mkubwa sana kwa Mnazi Mmoja ambao tunaendelea kushirikiana katika maeneo mengine mbali mbali.

Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja Kuwa ya Rufaa

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika bajeti za wizara zilizopita na katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, ni nia ya serikali kuipandisha hadhi hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa. Azma hii itawezekana kwa kuongeza majengo mapya, kuongeza vifaa vya kisasa na kuimarisha rasilimali watu. Tayari majengo upande ule wa Mradi wa *ORIO* ama ile iliyokuwa Kiwanda cha Madawa tayari imeshaanza kuonekana hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara ya Afya ya mwaka 2015/16 ilielezwa kuanzishwa kwa ujenzi wa jengo jipya litakalokuwa na wodi ya watoto yenye vitanda 94, wodi ya kitengo cha kusafishia damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo (*Dialysis Unit*) yenye vitanda sita na chumba cha maabara. Napenda kulijuilisha Baraza lako kuwa ujenzi wa jengo hilo tayari sasa hivi umefikia zaidi ya asilimia thamanini na kazi inayoendelea kwa sasa ni kuweka madirisha, kupaka rangi na kuweka vifaa stahiki. Baada ya hapo tutasheherekea sote pamoja katika ufunguzi na kuanza kazi mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio ya wizara kuwa ujenzi huo pamoja na uwekaji wa vifaa utakamilika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2016/17. Kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza sana usumbufu wa wagonjwa hasa watoto kulazwa katika kitanda kimoja watoto wawili hadi watatu, hali ambayo inajitokeza kwa baadhi ya wakati tunapozidiwa na wagonjwa inakuwa hatuna budi. Aidha, kutatoa fursa kwa kuanzisha huduma mpya ya kusafisha damu

kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo ambayo hivi sasa hawapati huduma na mara nyingi huishia kwenda nje ya Zanzibar kwa ajili ya kupata huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya ukarabati wa jengo lililokuwa kiwanda cha dawa unaendelea na sasa uko takriban asilimia 50. Ukarabati huo utakapomalizika utakuwa na wodi ya wazazi kabla kujifungua yenye vitanda 42, chumba cha kujifungulia kitakachokuwa na vitanda sita vya kisasa na ni vya aina yake, mzazi akienda kujifungua pale anacheka kabisa hanuni hata siku moja, wodi ya wazazi baada ya kujifungua itakayokuwa na vitanda 30, vyumba viwili vya upasuaji na wodi ya wagonjwa mahututi yenye vitanda sita. Hawatokwenda tena katika mazingira kidogo yenye kutisha hivi sasa wanakokwenda, kule kutakuwa na mazingira tofauti kabisa, tunaomba watuvumilie tu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile jengo hilo litakuwa na wodi ya watoto wachanga yenye vitanda nane, wodi ya huduma kwa watoto waliozaliwa kabla ya miezi tisa (kangaroo *care*)" yenye vitanda sita**,** kitengo cha huduma za dharura (*Accident and Emergency*), kliniki za maradhi mbali mbali, ununuzi wa jenereta na mashine ya kuchomea takataka za hospitali. Mheshimiwa hivi sasa tunaendelea kutumia kitengo kile cha *emergency* lakini kitengo kile pale *outpatient* ukiingia hospitali kitahamia chote katika jengo jipya na itakuwa ni ya kisasa, ile *ambulance* itakuwa tena hamna ile kushusha kubeba inaingia moja kwa moja mpaka kwenye chumba cha *emergency* kama wenzetu wanavyofanya nchi zilizoendelea Mabara, Ulaya na kwengineko.

PROGRAMU NAMB. 3: USIMAMIZI WA SERA ZA AFYA NA UTAWALA

Mhe. Mwenyekiti, programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala inalenga kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma bora kwa mujibu wa sheria na miongozo yenye misingi ya uwazi, uwajibikaji, ushiriki na ushirikishwaji wa jamii katika kutoa maamuzi kwenye mambo yanayohusiana na afya katika ngazi zote.

Utawala, Sera, Mipango, Utafiti na Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba Nguvu Kazi ya Sekta ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, ni azma ya wizara kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanaendelezwa kitaaluma ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na utendaji wao. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 jumla ya wafanyakazi 134 wanaendelea na masomo ndani na nje ya nchi. Ufafanuzi wa

taarifa hizi unaonekana katika kiambatisho namba 14. Aidha, jumla ya wafanyakazi 72 wamerudi kutoka masomoni na kupangiwa kazi katika sehemu tofauti. Katika historia ya Wizara ya Afya katika mwaka iliyovunja rikodi na tunaomba tumshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein, maana yeye ndiye aliyelisisitiza jambo hili la wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwenda kupata elimu zaidi, katika mwaka uliovunja rikodi ni mwaka 2015/2016 haijapata kutokezea Wizara ya Afya kupeleka idadi kubwa ya wafanyakazi wake kwenda kusoma kama hivi. Hii inatokana na kauli na muongozo wake mwenyewe Rais ambaye analisimamia jambo hili na kutushahisha kwamba mwaka huu tupitilize kiwango hiki Mwenyezi Mungu akitujaalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wizara inapata wafanyakazi wapya wenye taaluma ya afya imekuwa ikichukua jitihada maalumu katika kutoa mafunzo ya afya kupitia Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kilichopo Mbweni. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 1,043 wa kada mbali mbali ambao wanaendelea na masomo. Halikadhalika, wanafunzi 12 wanaendelea na fani ya udaktari katika Chuo cha Kusomesha Madaktari na wanategemea kumaliza masomo yao Julai, 2016 na baada ya hapo wataungana na sisi katika kujumuika kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, jumla wafanyakazi 27 wakiwemo madaktari 25, Mtalaamu wa Mionzi mmoja na Mtaalamu wa Viungo Bandia mmoja wameajiriwa. Sambamba na hilo, wafanyakazi 66 wa kada mbali mbali wamestaafu kazi kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma, wafanyakazi 10 wa kada mbali mbali wamekimbia kazini na wafanyakazi tisa wamefariki dunia (Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, *amin*).

Sera, Mipango na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti, pale kwenye kukimbia huwa mimi mara nyingi sipendi sana kusema kukimbia, wamepata ofa zaidi kwa hiyo wamekwenda kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inatarajia kuanzisha mfuko wa bima ya afya kwa nia ya kuhakikisha upatikanaji mahiri wa fedha endelevu kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya kwa wananchi na kuwapunguzia mzigo mkubwa wa kugharamia huduma hizo. Hatua kadhaa zimeshafanyika ikiwemo kuliwasilisha na kulijadili suala hili katika vikao mbali mbali vya serikali na kwa sasa wizara imo katika kutayarisha sheria ya kuanzisha mfuko huo ambayo itawasilishwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi baada ya kukamilika hatua zote hizo za kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa 10 wa mapitio ya Sekta ya Afya umefanyika, mkutano huo umewashirikisha wadau mbali mbali na kutoa mapendekezo ambayo yametumika katika kutayarisha mpango kazi wa mwakawa wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mwaka huu kauli mbiu ya mkutano ililenga kwenye kuwepo kwa uwajibikaji katika utoaji *wa* huduma endelevu za afya *"Stronger Commitment to Health for Sustainable Development".* Katika mkutano huo mapendekezo mbali mbali yalitolewa ikiwa ni pamoja na kuimarisha mashirikiano baina ya wizara, washirika wa maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi zisizo za kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutathmini utekelezaji wa mpango mkakati wa wizara, ripoti ya utekelezaji (*Health Sector Annual Performance Report*) kwa mwaka 2014/15 ilitayarishwa. Ripoti hii ilianisha utekelezaji wa wizara kwa kutumia viashiria vilivyomo katika Mpango Mkakati wa Tatu wa Wizara. Tayari ripoti imeshasambazwa kwa wadau mbali mbali katika mkutano wa kumi wa mapitio ya sekta ya afya uliofanyika Machi, 2016.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii iliibua changamoto mbali na kutoa mapendekezo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuunda Baraza la Maafisa Afya ya Mazingira na Bodi ya Ushauri ya Afya ya Mazingira, kuanzisha kitengo kitakachosimamia uhakika wa ubora wa huduma za afya (*Quality Assurance Unit*), kufanya mapitio ya Kitita cha Msingi cha Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi (*Essential Health Care Package*), kufanya mapitio ya Mpango wa Mahitaji ya Wafanyakazi (*Minimum Staff Requirement*), kuharakisha uanzishwaji wa bima ya afya na kuimarisha huduma za maabara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha tafiti zote zinazofanyika katika wizara, zinaendana na maadili ya afya, jumla ya maombi 12 ya tafiti za afya zilipokelewa na kuruhusiwa kufanyika.

Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba programu ndogo ya kuratibu shughuli za afya Pemba inatekeleza kazi na majukumu ya programu za Kinga, Tiba na Sera na utawala kama zilivyoelezwa katika utekelezaji wake.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana hayatokani na juhudi ya Wizara ya Afya pekee bali pia kwa mashirikiano na wadau mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi pamoja na wananchi wote kwa jumla, Taasisi za

Serikali na zisizo za Serikali, sekta binafsi,wananchi wa ndani na nje ya nchi pia. Wizara ya Afya inawashukuru sana na kwa dhati kubwa na inawaomba wasichoke kwani misaada yao ina thamani kubwa kwetu sisi na inaokoa maisha pale inapobidi, tunaomba waendelee kutuunga mkono pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa unyenyekevu kabisa. Shukrani makhsusi ziende kwa Serikali ya Denmark ambao wamekuwa wakitutolea msaada mkubwa sana, wa pili ni China, Sultanate of Oman, Cuba, Canada, Uholanzi, Israel, Norway, Misri, Ujerumani, Korea, Uturuki, India, Kuwait, Marekani, Italy, Saudi Arabia, Qatar na Uingereza.

Mhe. Mwenyekiti, aidha shukrani zetu za kipekee pia ziwaendee mashirika mbali mbali ya ndani na nje ya nchi ambao wamekuwa wakituunga mkono sana hata katika jitihada zetu za kipindupindu na daima tunapowaendea milango yao inakuwa wazi na ndio wanaotusaidia. Naomba michango ya Waheshimiwa Wawakilishi wayaelekeze pia kuwapongeza mashirika haya kwani kila tukiwapa moyo ndipo watakapoweza kutusaidia zaidi katika hii hali tuliyokuwa nayo. Mhe. Mwenyekiti, mashirika yenyewe ni kama ifuatavyo:-

WHO, GLOBAL FUND, UNDP, UNFPA, UNICEF, DANIDA, D-TREE INTERNATIONAL, SAVE THE CHILDREN, JHIEPIGO, SIGHT SAVERS, PATH FINDER, HIPZ, CLINTON FOUNDATION, IVO DE CARNERI, KOICA, JSI, WORLD BANK, RED CROSS, USAID, ZIDO, PEPFAR, MILELE FOUNDATION, WATER AID, ROTARY UK na wale wote ambao sikuweza kuwaorodhesha kwenye orodha hii kubwa na hotuba hii ndefu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukrani maalum ziwaendee Mhe. Naibu Waziri wa Afya Mhe. Harusi Said Suleiman naomba usimame kidogo uonekane, Katibu Mkuu wangu Dkt. Juma Malik Akil naomba usimame, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Halima Maulid Salum, Mkurugenzi Mkuu Dkt. Jamala Adam Taib, Afisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba Dr. Mkasha Hija Mkasha, Wakurugenzi wote wa wizara kwa pamoja naomba msimame na timu ya wataalamu kwa utayarishaji wa hotuba hii naomba msimame, naomba nisimsahau Dkt. Mohammed Saleh Jidawi aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya na hivi juzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein amemtua rasmi kuwa Mshauri Mkuu wa Waziri wa Afya, naomba bila ya kuwasahau Wajumbe wote wa Bodi zetu mbali mbali naomba wasimame wakiwemo Bodi ya Uuguzi, Wagonjwa wa Akili wote kwa jumla naomba wasimame. Mheshimiwa hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana na ndio tuliyofikia katika hali hii. Ahsanteni sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako pia naomba niwapongeze Washirika wetu wote wa Maendeleo waliohudhuria hapa ambao tumewaalika, naomba wasimame pia nao tuwaone tujue Washirika wetu wa Maendeleo. *Development Partners* wengine hawazungumzi Kiswahili *please*, mheshimiwa kidogo utaniruhusu nipige Kiingereza kidogo kwa sababu wapate kunisikia. *All what I say is to thank you very much for your supportive initiative that you have taken through out this budget and your continue supporters. We say thank you very much.*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali za Wizara ya Afya kwa kusimamia na kunishauri hali iliyopelekea kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi za wizara na utoaji wa huduma bora kwa wananchi wakiwemo naomba niwataje Mzee Masauni Hamad Masauni Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali Binafsi, Dkt. Juma Omar Khatib Mwenyekiti wa Bodi ya Afya ya Mazingira na Profesa Amina Abdul-Kadir Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Wakunga.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hitimisho hilo sasa naliomba Baraza lako lijadili, liikubali bila ya mabuti na kuipitisha bajeti hii ya Wizara ya Afya. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, wizara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 59,228,631,000 kati ya hizo Tsh. 11,893,300,000 kwa kazi za kawaida, Tsh.17,332,500,000 kwa mishahara na maposho na Tsh.1,496,600,000 ni ruzuku kutoka serikalini. Aidha, naomba Baraza hili liidhinishe jumla ya Tsh. 4,900,000,000 kwa kazizamaendeleo kutoka serikalini na Tsh. 23,606,231,000 kutoka washirika wa maendeleo ambao wale niliowasimamisha wanachangia kiwango hichi ni kiwango kikubwa sana Mhe. Mwenyekiti. Pia naomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Tsh. 8,605,800,000 kwa Hospitali ya MnaziMmojaikiwa Tsh. 7,470,800,000 kwa ajili ya mishahara na maposho, na Tsh.1,135,000,000 kwa kazi zakawaida. Vile vile Wizara yangu imepangiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu waSerikali jumla ya Tsh 188,011,000 kwa mwaka 2016/17 na kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja Tsh 1,014,302,000 Kiambatisho namba 15 kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima tena naomba sasa kutoa hoja rasmi kukubaliwa maombi hayo.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wa hotuba yako ya Wizara ya Afya, sasa tunaendelea kwa kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ili na yeye awasilishe hotuba yake, karibu sana.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (**Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii)**: Nakushukuru sana kunipa wasaa huu kuwasilisha maoni ya kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kuwasilisha hotuba hii ya maoni ya kamati ya Maendeleo ya Wanaweke na Ustawi wa Jamii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kuendelea vyema na siku nyengine ya mfungo katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani. Baraza lako tukufu litajadili na baadaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe binafsi kama nilivyosema kwa kunipa muda huu mchache kusimama mbele ya Baraza lako kuwasilisha maoni ya kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa fursa hii kumshukuru Waziri wa Afya kwa kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Afya Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo, Mwakilishi wa kudumu wa Jimbo la Kiembe samaki kwa uwasilishaji wake makini na mahiri katika niseme kipindi hichi kidogo alichoondoka hapa na zaidi kwa mashirikiano aliyotupatia yeye na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Harous Said Suleiman nae mwakilishi wa Jimbo la Wete kule Pemba. Mhe. Harous tuliekuwa naye muda wote katika ziara zetu na tunamshukuru sana kwa kipindi kifupi tulichofanya kazi naye. *(Makofi)*

Naomba nitoe shukurani pia Mhe. Mwenyekiti, kwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu, Wakurugenzi wote, Afisa Mdhamini pamoja na Maafisa wote na watendaji kwa ujumla waliosaidia kamati kwanza kufahamu muundo na shughuli za kila idara, taasisi na vitengo vya Wizara ya Afya pamoja na maelezo ya ufafanuzi wa mambo mbali mbali ya kisera, kisheria na kitaalamu ya Wizara hiyo hasa pale kamati ilipotembelea baadhi ya taasisi za Wizara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee kwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambao kwa muda wote wamejitolea kufanyakazi bila ya kuchoka katika kutekeleza majukumu yao. Kwa heshima kubwa na kwa kuthamini mchango na juhudi zao hizo naomba niwatambuwe kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini	Mwenyekiti
2.	Mhe. Tatu Mohamed ussi	M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe

4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mjumbe
5. Mhe. Makame Said Juma Mjumbe
6. Mhe. Hidaya Ali Makame Mjumbe
7. Mhe. Ame Ali Haji Mjumbe
8. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mjumbe

Pamoja na Makatibu wetu:-

Ndg. Aziza Waziri Kheri; na
Ndg. Khamis Hamad Haji

Wote tunasema shukurani na pongezi zetu za dhati kabisa kwa kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, nitangulie kulieleza Baraza lako kuwa Kamati yangu ilipata nafasi ya kufanya ziara kwenye wodi ya wazazi (*maternity*) hapa Mnazimmoja Hospitali, maabara iliyopo hapa Mnazimmoja, kitengo chawagonjwa wa nje, kitengo cha *X-Ray* na *CT-Scan* katika Hospitali ya Mnazimmoja. Vile vile tulipata wasaa wa kutembelea Bohari Kuu ya dawa iliyopo Maruhubi, ujenzi wa ofisi ya Mkemia Mkuu kule kule Maruhubi pamoja na hatimae kumaliza ziara yetu katika hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili pale kidongo chekundu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali tuliyoikuta inahitaji kuendelezwa sana na kuboreshwa kwa nguvu zinazostahiki kwa vile nguvu kazi kubwa ya nchi hii inategemea kupata huduma za afya katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja na Hospitali nyengine za Wilaya, basi lazima bajeti yao yaani ya Wizara iongezwe mara dufu ili Wizara iweze kukabiliana na kikamilifu na ongezeko kubwa la shughuli za afya nchini. Tusijidanganye sisi ndio tunaotegemea huduma za afya zinazotolewa nchini, lakini kwa hali tuliyoikuta na bajeti wanayopata Wizaraya Afya kwa kweli lazima tupige konde, kwa ufupi Mheshimiwa nilitaka kusisitiza bajeti wanayopata Wizara ya Afya kuiendelea sekta ya afya nchi hii haitoshi, hivyo Serikali lazima tuiambie wazi wazi hali tuliyoikuta kwa kweli hairidhishi hata kidogo na wala hatuitendei haki Wizara ya Afya kwa bajeti wanayo-*operate*, huo ni ukweli lazima tuiombe sana serikali yetu panga panguwa Mhe. Mwenyekiti, lakini kuendeleza sekta ya afya kwa hali tuliyoiona inasitikisha.

Mhe. Mwenyekiti, wengine bahati nzuri tulifanya kazi Hospitali ile na nilikuwa waziri na tulivyoiona hali ile na tulivyo sasa kwa kweli tunahitaji mabadiliko makubwa sana kuweza ku-*sustain services* katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara yetu ya Hospitali ya Mnazimmoja tumekuta majengo mengi yanahitaji matengenezo ya haraka kunusuru vifaa na zana za tiba zilizopo. Kitengo cha *X-Ray* kinavuja, *x-ray* iliyopo hivi sasa ni ile ya *'mobile'* na ile ya kawaida imekufa muda mrefu sana. Kwenye kitengo cha maabara hakuna vitendanishi yaani *'reagents'* lakini pia dari ya maabara hiyo pia inavujiwa na kuhatarisha usalama wa vyombo kama *'solar panel' na 'server'*, vile vile chumba cha uchunguzi cha *'parasitology'* na *'clinical chemistry'* navyo vinavujiwa huku dari yake ikianza kuporomoka na kudondosha saruji iliyotiwa ya zege kwa sababu ya kuvujiwa. Kwa ufupi paa lote la jengo la maabara bovu linahitaji kujengwa upya HARAKA IWEZEKANAVYO.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara tuliyofanya Bohari Kuu ya Dawa, tumekuta wenzetu wanafanyakazi nzuri, na wanastahili pongezi, hata hivyo bado kuna upungufu wa dawa katika bohari yetu pamoja na ufinyu wa bajeti. Kamati imeambiwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa dawa za *'emergency',* dawa muhimu kwenye wodi ya wazazi na *ICU*, vifaa vya maabara na *x-ray*.

Aidha, changamoto nyengine ambayo kamati yangu imeikuta ni malipo ya posho la kazi ngumu kwa wafanyakazi wa Boharim Kuku. Kamati tunaiomba Wizara katika bajeti ijayo waanze kuwalipa wafanyakazi wa Bohari Kuu posho la kazi ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu, ina matatizo mengi sana na tumejulishwa kwamba kule imekuwa ni dumping place ya wafanyakazi waliokosa kwengine kuwa wanatupwa kule na pili hata wale wagonjwa nao, kwa kweli ukenda kule kunasikitisha na ningeomba sana kiongozi wa shughuli za serikali hapa tungefanya juhudi wawakilishi wote tukenda kutembelea Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kujionea hali ilivyo na tuweze kuchangia kidogo ile hali tuirejeshe ilivyo. Kwa kweli wagonjwa wa akili ni kama wagonjwa wengine, tusiwafanyie *stigmatization* kwa kweli haifurahishi.

Mhe. Mwenyekiti, Uhaba wa wafanyakazi tuliogunduwa, uhaba wa wafanyakazi hasa wahudumu (*orderlies*), waliopo ni wachache na wanazidiwa na idadi ya wagonjwa; kuna wauguzi tumejuilishwa pale 22 yaani *'Psychiatric Nurses'* lakini hawafanyikazi wodini hatujui wako wapi. Daktari dhamana wa Hospitali tumejuilishwa kwamba kwa kweli yeye hana utaratibu wa kufanya round wodini anawaachia wasaidizi wake lakini kwa inavyopaswa yeye awasimamie wasaidizi wake na wasaidizi wake bahati nzuri wanafanya

kazinzuri tunajulishwa kwamba hao ndio wanafanya round na alhamdullillahi kazi zote wanzifanya pale, kidogo hali hii haikutupendezesha.

Mhe. Mwenyekiti, Kuimarishwa uongozi wa Hospitali nako kunahitajika, kamati imebaini kuna changamoto kubwa ya nidhamu kwa baadhi ya wafanyakazi, kwa sababu wengine wanahalifu sheria, wanahalifu sheria wakihukumiwa basi mkuu anawatetea kwa kweli haifurahishi, yaani suala zima la uongozi au *management* nalo linahitaji kuitiwa upya itizamwe kwa mapana yake. Mheshimiwa ipo haja pale *Mental* Hospitali arudishwe yule Mkurugenzi Dhamana anaitwa *Mental Superintendent* kusimamia vyema na mfuko wake na bajeti yake ile hospitali nayo iende ipasavyo. Tunashukuru sana tumeambiwa pale kuna mfadhili mzuri anapeleka mikate mia mbili kila siku anafadhili yeye kwa ukosefu wa bajeti na wale wagonjwa wa akili wanakula kweli kweli na wana nguvu kweli kweli wale. Mimi zamani nakumbuka wengi na Uniform zao wana kifuko cha njugu wale kila mara wanakula njugu nyasa tu, wao madaktari wenyewe wanajua nini umuhimu wa njugu nyasa kwa wagonjwa wa akili, narudia kwa wagonjwa wa akili.

Mhe. Mwenyekiti, Kama nilivyosema kuna upungufu tumegunduwa wa uhaba wa bajeti na vitendea kazina hasa kwa kutegemea kwamba wao wako chini ya Mnazimmoja Hospitali, ingekuwa vyema wakawa na bajeti yao na mwenendo wao wa kazi peke yao Uchakavu wa Majengo na wodi za wagonjwa wa Mental Hospitali ni mbaya sana sana, kwa kweli vyoo pale ndio hatari zaidi na wagonjwa wale wanakata magodoro ah! simalizi hapa mtamaliza wenyewe, wanakata magodoro kutumia uwani, sasa kutokana na maji kutotoka mda wote mda kwa sababu bili ya maji wanayotumia ni kubwa, pesa wanazopata kidogo, kwa hiyo mara nyingi maji yale *pump* inazimwa ili ku-*serve* bajeti ndogo ya nini hii. Kwa hiyo kwa ujumla ninataka kusema suala la *Mental Hospital* ninaiomba sana Mhe. Wizara Mhe. Waziri ulitupie jicho la huruma kwa haraka sana hali tuliyoikuta kule kwa kweli hairidhishi hata kidogo, hawana hata usafiri gari iko moja tu ya wagonjwa ambayo tumeambiwa imeshaharibika.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna ukosefu wa ulinzi, wodi za wanawake kule ukuta upo mkubwa lakini wahalifu wanachupia wanaingia wodi za wanawake, wanaiba vilivyopo na kufanya mambo mengine ambayo hata hayazungumziki, ukuta ule nao umetobolewa, wahalifu kule nje wametoboa, ili maji yasituwame kwenye nyumba zao yale maji sasa yanaingia *Mental Hospital* na ndiyo yaliyosababisha kuleta kipindu pindu ndani kwasababu wamekwenda wameingia mpaka kwenye kisima maji machafu yale. Mhe. Mwenyekiti, sisi kamati tulipokwenda jana kama nilivyosema haya tumeyaona wenyewe si ya kusimuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia tumejuilishwa kwamba malipo ya posho la mazingira magumu kwa wafanyakazi ambao wanahudumia wagonjwa wenye changamoto zisizo za kawaida.

Aidha, wapatiwe sare na usafiri. Kwa sababu hakuna sare hata za wagonjwa, basi matokeo yake wagonjwa wanakwenda na nguo zao, leo katika wodi za *Mental Hospitali* kuna kunguni huwezi kuamini kabisa, kuna kunguni, kuna mchwa kwenye wodi ile mbaya kabisa, hayo tumeyaona jana wenyewe kwa macho yetu.

Mhe. Mwenyekiti, malalamiko makubwa kila tulipopita ni ukosefu wa vitendea kazi kutokana na ufinyu wa bajeti. Kamati inaiomba sana Serikali kuitizama tena bajeti ya Wizara ya Afya kama nilivyosema. Suala la afya ya wananchi wetu halina mjadala, madaktari wazuri wao, wamesoma vizuri, wana sifa nzuri tena wamesoma kwenye vyuo vinavyotambulika, lakini kama hakuna bajeti, hakuna vitendea kazi, wagonjwa wanakufa mikononi mwao wanawaona, kwa kweli inatia uchungu sana, inatia uchungu sana sana sana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tulichogunduwa kwa ujumla kwamba iko haja ya Mhe. Waziri tujipange vizuri katika suala zima la *management*, suala zima la utawala na uongozi kidogo tumekuta hakuna ku-streemline, hakuna mtiririko wa amri za kazi, mkubwa wa kazi anampa mdogo wa kazi amri hafanyi anakuwa jeuri na bado yupo kazini, kwa kweli lazima *disciplinary measure*s zichukuliwe kwa watu kama hao.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Wazazi pamoja na Mwembeladu wanahitaji milioni tisiini kwa mwezi, Maabara pia wanahitaji milioni mia moja kwa mwezi, Pemba nako wanahitaji si chini ya milioni ya miliioni mia mbili katika vitengo kama hivyo kwa mwezi ku-sustain hayo mambo ya wazazi na mengineyo, maabara na kwa ujumla. Hayo nimesema kwa ufupi tu lakini kwa kweli tumekwenda Maabara wanasema hatuna vitendea kazi, hakuna *reagency t*utafanya kazi vipi, madaktari wana *order* kufanya *test* hii hii hii, lakini wanashindwa kufanya kazi. Kwa hiyo tunaiomba sana serikali bahati mbaya kiongozi wa shughuli za serikali yeye hayupo pamoja na Waziri mwenyewe wa Nchi naye hayupo, lakini bila shaka walipo wananisikia. Haya tuliyoyaona nasisitiza sana, kwamba haya ndio tuliyoyabaini na mimi ningemuomba sana kiongozi wa shughuli za serikali akaitembelea kwanza Hospitali ya Mnazi Mmoja aone hasa hali ilivyo.

Pili, aitembelee *Mental Hospital* aone hali ilivyo, naamini wakishatembelea hospitali hizi mbili watajua wapi tupunguze bajeti tuiongezee Wizara ya Afya. Hapa tunaitetea sana Wizara ya Afya ndio kimbilio letu wanyonge, wagonjwa, wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa waziri lakini haya sikuyaona undani wake kwa Wizara ya Afya, sasa niko *backbencher* natembea, nazungumza huko nimeyaona. Kwa hivyo, ninayosema haya natoa moyoni na anayekupenda Mhe. Waziri anakwambia. Hilo ni gumu sana, anayekupenda anakwambia akinyamaza kimya anakuharibu. Kwa hiyo, hii tunachukulia ni kama *Constructive criticism*, yaanio tunakosoa kwa kuelekeza nini kifanywe tupate maendeleo katika nchi yetu, tusiyafiche matatizo. Matatizo tumeyaona tuyashughulikie.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kwa ufupi haraka haraka niendelee na idara zako.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, programu za wizara hii jumla yake ni tano, wizara wenyewe wanasema tatu lakini sisi tumejumlisha ni tano, ambazo zimewekwa katika mafungu mawili ya H01 na H02, programu zenyewe ni kama ifuatavyo:-

- Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;
- Programu ya Tiba;
- Programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala;
- Programu ya Uchunguzi na Matibabu; na
- Programu ya Uongozi na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu H02, ni fungu la Hospitali ya Mnazimmoja lenye program kuu mbili, moja ni Program ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu na ya pili ni Program ya Uongozi na Utawala. Katika Programu Kuu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu, kuna programu ndogo moja tu ya Huduma za Matibabu. Kamati yangu inashauri kuwa ni vyema Programu Kuu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu ikawa na programu ndogo mbili ambazo ni Huduma za Uchunguzi na Huduma za Matibabu, kwa vile huduma zote hizo kila moja ni muhimu na inahitaji kuwa na bajeti ya peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoelezea Mhe. Waziri katika hotuba yake kuwa zipo changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji mashirikiano yetu sote

kuzitatuwa, na sisi kama Kamati tunaungana naye katika kusaidia mawazo na fikra ya kusaidia kuzitatuwa changamo hizo.

Kwenye changamoto ya uhaba wa fedha Kamati inaiomba kama nilivyosema hapo awali serikali kwa makusudi kabisa kuongeza bajeti kwenye ununuzi wa dawa, kununua vitendanishi na vifaa tiba, ili kukidhi ongezeko la wagonjwa hasa pale serikali tunaposisitiza ule mtizamo wetu kwamba afya kwa Zanzibar ni bila ya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye changamoto ya ongezeko la maradhi yasiyoambukiza kama vile shindikizo la damu, kisukari, saratani na ajali za barabarani, kamati yangu inaiomba wizara kuongeza elimu ya afya na wananchi washauriwe na kuhamasishwa kubadili tabia na kupima afya zao. Suala la afya ya jamii lipewe mkazo unaostahili, miongozo ya utekelezaji na kusimamiwa kisheria na Manispaa na Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, pia changamoto ya kuharibika mara kwa mara vifaa tiba na upungufu wa wataalamu, kama alivyoeleza Mhe. Waziri na sisi kamati pia tumeshuhudia wakati wa ziara yetu. Kamati yangu inashauri waajiriwe mafundi wa kudumu '*biomedical engineers'*, mafundi wa zana za hospitali tumejulishwa kuwa hakuna, vifaa vikiharibika vimelala tunangoja kununua chengine, kipya nacho kikiharibika kimelala. Kwa hiyo, tunaombma sana mafundi hawa waajiriwe haraka sana na haya malalamiko makubwa tumeyakuta huko tulipotembea hasa katika Hospitali ya Mnazimmoja na Hospitali kubwa za Wilaya ambao watashughulikia utengenezaji wa vifaa tiba vilivyoharibika pamoja na kuongeza bajeti ya matengenezo. Zana na vifaa vingi vilivyoharibika inshindikana kutengenezwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kamati vile vile inashauri mafunzo maalumu ya namna bora ya kutumia vifaa tiba kama vile '*CT-Scan*' na kadhalika yafanywe kwa mafundi wetu sambamba na kuwepo mikataba ambayo itatowa waranti ya angalau miaka mitatu kwa vifaa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya kuongezeka bidhaa ambazo hazikidhi viwango zinazoletwa na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kupitia bandari na njia zisizo rasmi ni kweli zina athari kubwa kwa afya ya jamii na watumiaji kwa ujumla. Hivyo, kamati yangu inashauri serikali kuchukuwa hatua kali kwa atakaebainika kuleta bidhaa mbovu nchini ikiwemo kubeba gharama za kuziangamiza na hata kuzirejesha zilikotoka kwa gharama zake. Kamati yangu inaunga mkono juhudu za serikali kupiga marufuku uingizaji

bidhaa mbovu zilizo chini ya viwango kama vile nguo za mitumba, vifaa vilivyokwishatumika na kadhalika ili nchi yetu isigeuzwe jaa la bidhaa mbovu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapongeza mpango wa ukaguzi wa kuangalia usalama wa chakula na dawa zinazoingizwa nchini, ambapo wataalamu wetu wanakwenda nje ya nchi kufanya ukaguzi wa vyakula na dawa hizo. Hata hivyo, katika ukaguzi wa mchele na nafaka nyengine zinazoingizwa nchini ukaguzi ufanyike kabla ya kupakiwa (*pre shipment*) na baada ya kupakiwa (*post shipment),* ukaguzi huo ufanyike sambamba na upatikanaji wa nyaraka halisi zinazoambatana na cheti cha upakizi wa mzigo (*Bill of lading)*. Hii kwa kweli ni *practice* ya kawaida inafanywa, lakini tunaomba kusisitia kwamba kusiwepo na *laxity* katika suala hili, lazima tuwe wakali tufuate taratibu kuepukana na kuletewa michele mibovu, nyunga na vitu vingine vibovu.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapongeza juhudi kubwa zilizofanywa na serikali na wizara kwa ujumla katika kutokomeza maradhi ya malaria hasa kwenye mkakati wa usambazaji wa vyandarua, utiaji dawa za kuulia mbu waenezao malaria, uchunguzi sahihi wa wagonjwa wa malaria, ufuatiliaji wa wagonjwa wa malaria pamoja na kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari. Kwa mara nyengine tena kamati yangu inapongeza juhudi hizi, hii ni heshima kubwa kwa Zanzibar. Tumeonesha mfano kilimwengu kwamba suala hili la kupambana na maradhi na kuyatokomeza linawezekana au limewezekana Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Afya, licha ya mafanikio hayo ya kupunguza malaria chini ya asilimia 0.5, zipo wilaya ambazo bado maradhi haya yanaripotiwa kuwepo, kama vile Wilaya za Kati, Kusini, Kaskazini A na B na Magharibi kwa Unguja na kwa Pemba Mhe. Waziri katueleza Wilaya za Micheweni na Wete. Kamati yangu inatoa msisitizo kwa wilaya hizi zinazoendelea kuripoti kesi za malaria katika kipindi chote cha mwaka kuwa lazima Kampeni ya "Tokomeza Malaria" iimarishwe kupitia Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Kamati yangu inashauri yawepo mashirikiano kupitia uongozi wa wilaya kila mwaka kuhakikisha wilaya haitoi wagonjwa wa Malaria.

UDHIBITI WA MARADHI YA UKIMWI NA VVU

Mhe. Mwenyekiti, maradhi ya Ukimwi bado ni tishio katika jamii yetu, ugonjwa huu bado upo na mpaka hivi sasa hauna tiba, wala tusijidanganye.

Mhe. Waziri ametueleza hapa kuwa zipo kliniki 12 zinazotoa huduma kwa wanaoishi na VVU, hadi mwezi Disemba, 2015 wagonjwa 8,721 wamesajiliwa katika kliniki hizo. Bado nasisitiza kuwa dawa za maradhi hayo haijapatikana, dawa zilizopo ni za kupunguza makali tu ya VVU na kurefusha maisha tu.

Mhe. Mwenyekiti, baya zaidi baadhi ya wagonjwa wameanzishwa dawa za kupunguza makali ya *VVU*, lakini cha kusikitisha hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu ni wagonjwa 3,978 wamebaki. Kamati inaiomba wizara kufuatilia wagonjwa hawa kwa makini na kuzidisha elimu ya afya kwa jamii kuhusu huduma zinazopatikana kwa wanaoishi na *VVU* ili wasichukue nafasi ya kusambaza zaidi.

WAATHIRIKA WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa makundi ya vijana yameleta athati mbaya kwa vijana hao ambao ndiyo tunaowategemea kama nguvu kazi ya nchi yetu siku za mbele. Tunapongeza jitihada za serikali kuendelea na juhudi za kuwapatia walioathirika dawa ya *'methadone',* kamati yangu imeshuhudia vijana hao wakifika katika kituo maalumu kilichopo katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili iliyopo Kidongo Chekundu. Ni jambo jema sana kuwatibu walioathirika, hata hivyo, kamati inashauri mkazo uwekwe katika kukinga matumizi ya dawa za kulevya.

HUDUMA ZA CHANJO

Mhe. Mwenyekiti, katika huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Mhe. Waziri, ametueleza kuwa chanjo ya penta kitaifa imeshuka kutoka asilimia 98.8 kwa mwaka 2014 hadi 81.1 kwa mwaka 2015. Kwa ujumla kamati yangu inaridhika na kazi za utoaji chanjo. Hata hivyo, kushuka kwa chanjo ya Penta kutoka asilimia 98.8 hadi asilimia 81.1 kunahitaji kufuatiliwa kwa umakini kujuwa nini tatizo la upungufu huu.

HUDUMA ZA ELIMU KWA WAJAWAZITO

Mhe. Mwenyekiti, katika mafunzo yanayotolewa kwa wafanyakazi kuhusu muongozo wa maendeleo ya mama mjamzito kabla ya kujifungua, kamati inashauri kuwa wafanyakazi waliopatiwa mafunzo waandae mafunzo mengine kama wakufunzi kwa wafanyakazi waliopo vijijini *'trainer training'.* Sambamba na mpango huo kamati yangu inaipongeza wizara kwa kuanzisha mpango wa kuwatembelea mama wajawazito kwa lengo la kuwaelimisha, mpango ambao umeanza katika Wilaya ya Kaskazini B. Kamati inashauri mpango huu mzuri uwe endelevu katika wilaya nyengine za Zanzibar.

HUDUMA ZA AFYA MASKULINI

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza wizara kwa kuendeleza huduma za uchunguzi kwa uoni katika maskuli na vyuo. Vile vile kamati inashauri kutolewa miwani kwa bei nafuu kwa wanafunzi ili kurekebisha matatizo madogo madogo yanayobainika mapema. Suala la *'outreach services'* vijijini liendelee kwa wananchi waliopo vijijini ingawa kambi kadhaa za uchunguzi wa macho na matibabu zimefunguliwa na taasisi zisizokuwa za kiserikali.

VITUO VYA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kuimarisha sekta ya afya inakwenda sambamba na uimarishaji vituo vya afya, tunapongeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wananchi katika kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vya Kinuni, Bumbwisudi, na Ukongoroni. Kamati yangu inataka kujuwa Wizara ya Afya imejipangaje kuhakikisha vituo hivyo vinapata zana na wafanyakazi wa kutoa huduma.

IDARA YA TIBA

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefahamishwa kuwa Ofisi ya Mfamasia Mkuu ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kununuwa dawa na vifaa tiba. Kamati yangu inataka kufahamu utaratibu unaotumika wa kununua dawa kupitia Ofisi ya Mfamasia Mkuu. Bohari Kuu kupitia mtandao wao unaoviunganisha vituo vyote vya afya ndio wanaopanga mahitaji ya dawa na kiasi kinachohitajika na shughuli za uratibu wa manunuzi zifanywe na taasisi inayohusika na manunuzi. Njia hii itarahisisha kupunguza mlolongo mrefu wa upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya afya mpaka kwenye wodi.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri alivyotuleza kuhusu mfumo mpya wa ukusanyaji wa taarifa za dawa, zana na vifaa tiba *(Electronic Logistic Management Information System-eLMIS),* mfumo ambao kamati yangu ilioneshwa namna unavyofanya kazi na sisi kama kamati tunaipongeza wizara kwa kuja na mpango huo ambao utahakikisha vituo vyetu vya afya vinakuwa na dawa muda wote kadiri inavyowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, uhaba wa dawa katika vituo vya afya na hospitali zetu unatokana na uhaba wa fedha ambapo miongoni mwa dawa zinazokosekana katika vituo vyetu ni zile dawa muhimu. Kamati yangu ilipofanya ziara katika

Hospitali ya Mnazi Mmoja imeshuhudia kuwa *'dispensary'* ya Hospitali ipo wazi kwa masaa 24, lakini dawa nyingi hazipo.

Mhe. Mwenyekiti, mahitaji hayo ya dawa yapo pia katika wodi ya wazazi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo kama nilivyotanguli kusema kamati imepata fursa ya kutembelea. Kamati imeelezwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 90 zinahitajika kwa mwezi ili wodi ya wazazi iweze kutoa huduma zake ipasavyo bila malipo.

Mhe. Mwenyekiti, gari za kusambazia dawa nazo ni tatizo, ambapo kamati imebaini kuwa Bohari Kuu ya dawa ya serikali inazo gari mbili tu, moja Unguja na nyengine Pemba. Kamati inashauri kuwa ipatikane gari moja ya usambazaji dawa kwa kila Mkoa kwa ajili ya kusafirisha dawa katika vituo vya Mkoa husika.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na wodi ya wazazi, kitengo cha wagonjwa wa ungalizi maalumu (*ICU*) kuna ukosefu wa dawa muhimu '*essential drugs',* kamati pia imegunduwa upungufu wa dawa za dharura '*emergence drugs'*, kama nilivyosema pale awali, upungufu wa vifaa kwenye mashine ya *x-ray* na maabara. Kama tulivyoshahuri hapo awali tunasisitiza tena kuwa bajeti iongezwe ili dawa na vifaa tiba vipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali na vituo vya afya binafsi ni muhimu katika kusaidiana na serikali kuimarisha sekta ya afya na ustaawi wa jamii yetu. Kamati inaheshimu na kupongeza kwa dhati juhudi za sekta binafsi kwenye sekta ya afya. Hospitali binafsi ingawa zinatoa tiba lakini zinaendeshwa kibiashara, huo ndio ukweli wenyewe, hivyo ni muhimu sana Bodi ya Hospitali Binafsi kusimamia vyema uendeshaji wa hospitali binafsi. Kamati inasisitiza wizara kufanya ukaguzi wa hospitali binafsi na ihakikishe kuwa famasi na maduka ya dawa binafsi hawamuuzii dawa zisio baridi mgonjwa bila kuja na cheti cha Daktari *'doctor's prescription';* lazima apeleke cheti auziwe dawa, lakini hali nyingi utakuta kwamba mtu anakwenda anajieleza mwenyewe anauziwa dawa. Kwa kweli hali ile ni hatari na inatisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee unaendelea vizuri kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba, mwezi wa Septemba, 2016 wanatarajia itakamilika na umeshafikia asilimia 90. Tunampongeza sana Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Ali Mohammed Shein kwa maelekezo na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanikisha kuanza kwa ujenzi wa hospitali hiyo ambayo inatarajiwa kufunguliwa mwezi Septemba mwaka huu.

Lakini hapa hapa nilitaka kusahau tumejulishwa kwamba pale palikuwa na wafanyakazi 100 katika Hospitali ya Abdalla Mzee, na ikikamilika hospitali wafanyakazi wanaohitajika si chini ya 500. Sasa tunaiomba sana wizara kujitayarisha mapema katika suala zima la *staffing* isifike hospitali inafunguliwa vitengo vipo lakini *staff* hakuna.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZIMMOJA

Mhe. Mwenyekiti, tunampongeza sana Mhe. Waziri kama alivyotueleza kwamba juhudi za kupunguza wagonjwa kupelekwa nje ya nchi zinafanyika kwa kuendesha kambi mbali mbali za matibabu kama vile hudma za *'plastic surgery'*, *paediatric surgery'* na '*neuro surgery'*, huduma ambazo zimeleta faraja kwa wananchi na kuipunguzia serikali gharama za kusafirisha wagonjwa nje ya nchi. Pamoja na hali hiyo, lakini hali ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kama tulivyoeleza hapo awali, inahitaji kuimarishwa kwa kuongezewa fedha, dawa na vifaa tiba kwa uhakika na kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zimedhihirisha azma ya serikali ya kutoa huduma za afya bila ya malipo, idadi ya wagonjwa wengi wamefanyiwa vipimo mbali mbali vikiwemo '*x-ray'* na '*CT -Scan'* kama Mhe. Waziri alivyotoa takwimu. Lakini pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto kubwa ya upatikanaji nyenzo kama tulivyotanguliza kueleza kwa kirefu, baya zaidi *'films'* huwa mara nyingi zinakwisha na haziwi *replaced* haraka iwezekanavyo. Madaktari wanalazimika kudai filamu wazione wenyewe mbali na ripoti ya *'radiographer',* matokeo yake wagonjwa inabidi waende hospitali binafsi na kulipa shilingi 250,000/= ili baada ya kupigwa *CT- Scan* lakini pia wanapata ile *film* yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzishwa kwa kliniki maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa saratani ni jambo la kupongezwa sana. Kamati inashauri wizara, mtaalamu aliyekuwepo kwa kazi hii ni daktari bingwa ambaye anatoa huduma hizo katika chumba kimoja kilichopo Mapinduzi Kongwe, tunaomba mtaalamu huyu apatiwe jengo lake kwa ajili ya kuotowa huduma zake katika wigo mpana zaidi na tunampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameianza.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia tunapongeza kazi nzuri ya kuendeleza mashirikiano baina ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na taasisi mbali mbali za kimataifa kama alivyozitaja Mhe. Waziri, kamati tunaomba mashirikiano hayo yaendelezwe na wataalamu wetu na wao wapate fursa ya kujifunza namna wenzetu walivyopiga hatua katika maeneo mbali mbali ya huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ni wa kupongeza na ni muono wa muda mrefu.

Hata hivyo, kamati inasisitiza pamoja na juhudi mbali mbali zilizochukuliwa na ambazo tumepanga kuzichukua kufikia azma hiyo, kamati yangu inashauri kuendelezwa na kuimarishwa huduma zinazoendelea kutolewa na na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mapungufu ya vitu kama *'gloves'* na '*reagents'* kwenye hospitali kama hiyo hayakubaliki.

MUUNDO WA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, katika programu ya uendeshaji na utawala, kamati inapendekeza kufanyiwa tathmini na kupitiwa upya muundo wa wizara kwa kutizama ukubwa na uzito wa kazi za wizara. Kuwa na idara tatu kamati inaona kwamba hazikidhi haja ya utendaji mzuri katika kuimarisha bara bara huduma za Wizara ya Afya. Ingawa yapo Mabaraza ya Bodi ya Madaktari, Bodi ya Hospitali Binafsi, Bodi ya Ushauri wa Afya ya Jamii na Bodi ya Baraza la Wauguzi. Lakini Bodi na Mabaraza hayo hayafanyikazi kila siku, kamati inapendekeza kuundwa Idara mpya mbili, kwanza Idara ya Afya ya Jamii na ya pili, Idara ya Wauguzi na Wakunga.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeona kuwa kuna muingiliano mkubwa wa kazi za kinga na tiba ingawa hatuwezi kuzitenganisha, hata hivyo, tumegunduwa kuwa, mkazo mkubwa unawekwa kwenye tiba na fedha nyingi zinatumika kwenye tiba kuliko kinga hasa kwenye afya ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za afya ya jamii, ikiwemo usafi zinafanywa na Mabaraza ya Mji na Manispaa, hata hivyo, kamati inashauri kuwa idara hii itakapoanzishwa iwe ndiyo msimamizi mkuu wa suala zima la afya ya jamii kwenye shehia, wadi, Wilaya na Mkoa kwa kushirikisha na kusimamia ipasavyo Manispaa na Halmashauri za Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa tathmini hii kamati yangu inashauri kurejesha nafazi za *'Chief Medical Office', Chief Nursing Officer', 'Chief Laboratory Technologist', na 'Chief Public Health Officer'* ambapo nafasi hizi tunashauri zirejeshwe chini ya Idara kamili, kama wanavyofanya wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi jirani ya Kenya ambayo wemediriki hata kuanzisha Wizara nzima ya *'Public Health and Sanitation'.*

Hivi sasa vituo vya afya vya vijijini na Wilaya vipo chini ya Idara ya Kinga chini ya ofisi ya *zone* (*DHMT*) badala ya Idara ya Tiba, kwasababu pia vinafanyakazi ya kutibu. Maana yake ni kuwa mkazo mkubwa umewekwa katika kutibu na siyo kukinga, muundo huu ukibadilishwa na kuwa Idara ya Afya ya jamii *'department of public health'* vituo hivi vitasaidia katika jukukumu zito la kukinga maradhi kama haya ya kipindupindi yaliyotokea hivi karibuni na ambayo yanatokea mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri katika hili ni mripuko wa maradhi ya kipindupindu ambapo tulichukuwa nguvu kubwa kwenye kutibu kuliko kukinga wakati maradhi haya yameshaingia nchini. Inapofikia hatua kama hii hali inakuwa mbaya sana, huwezi kuamini mgonjwa mmoja ambaye ameshakuwa taabani anawekwa chupa mpaka nne za dripu kwa wakati mmoja kuokoa maisha yake na jambo ambalo tungeweza kulikinga.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Cholera tumejifunza sana na inabidi kwa kweli tuiombe sana wizara suala zima la Afya ya Jamii tulitilie mkazo sana "kinga ni bora kuliko Tiba" tusifanya masihara kwenye afya. Afya ya bianaadamu ndio kila kitu. Kwa hiyo, tunapoweza kukinga tukinge, tusiachie watu maji yale ya visima kuchimbwa ovyo taratibu zipo watu kwenda kujisafisha kwenye mito, kuuza bishara holela holela.

Tunampongeza sana Mkurugezi wa Kinga kwa juhudi ambazo azimechukuwa hivi sasa kudhibiti maradhi haya, tunaambiwa yanapunguka yanarudi kwa sababu baadhi ya watu wamekuwa wakaidi katika kufata taratibu zilizowekwa. Tunaiomba sana wizara na serikali kwa kweli katika hili tusilifanyie masihara, wengi hatujamuona mgonjwa wa cholera anavyokufa. Lakini ukimuona mgonjwa wa cholera anavyokufa huwezi kwa kweli kufanya masihara hata kidogo na maradhi hata kidogo na maradhi haya. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri suala la kampeni hii alizidishe liwe marudifu.

Naomba nimalizie Mhe. Mwenyekiti, muda uliobaki ni mchache na mimi namalizia nisema kwamba haya yanahitaji juhudi zetu za pamoja sisi wana siasa, sisi Wawakilishi, Wabunge Wakuu wa Mkoa, jamii yote suala la kinga suala la kutumia vyoo, suala la usafi hili ni letu sote na sisi kama ni Wawakilishi kama tulivyosimamia mengine basi na hili naliomba sana tulisimamie ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza mpango wa serikali wa kuunganisha Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kilichopo Mbweni kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Kamati tunaitaka wizara kuwa wakali katika

kusimami sifa za wanafunzi watakaodahiliwa au kufanyiwa *interview* kuingia chuo hicho. Tunahitaji wataalamu wenye sifa na ujuzi.

Tumesikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli, alivyodhamiria kuondoa wanafunzi wasiokuwa na sifa katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, niwaomba Waheshmiwa Wajumbe, katika hili tusije na sisi tukalazimisha vijana wetu lazima wachukuliwe japo hawana sifa haitotusaidia tunapeleka wataalamu ambao hawasomesheki au watakuja kufeli au tutakuwa na madaktari ambao hawatafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tunaomba sana wizara suala la sifa kuingia katika Chuo cha Afya lazima isimamiwe ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia Afya ndio hazina ya nchi. Lazima tukinge maradhi kwa juhudi zote na kutoa matibabu stahiki kwa wakati pale inapohitajika ili tuweze kuepuka kupoteza nguvu kazi ya nchi ya nchi yetu waswahili wamesema "kinga ni bora kuliko tiba".

Kwa ujumla tunaishukuru sana serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutanua wigo wa huduma za afya kuanzia vitengo vya afya, hospitali, *clinic* na kuwasomesha wafanyakazi. Kubwa zaidi sas twende kwenye usimamizi na utendaji mzuri ili tupate *delivery* ya *hall system* katika nchi yetu hilo ndio suala la msingi ndio suala la msingi inafaa tuzingatie.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji wako wa ripoti hiyo na sasa muda uliobakia ni dakika 10 nitampa mchangiaji mmoja ambaye ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Tafadhali tumia muda huo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, muda ni mdogo utakuwa hujanitendea haki kabisa kabisa. Hii wizara nzito nyeti Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii kazungumza .....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado sijakusikia unasema.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nasema muda ni mdogo dakika 9 zilizobaki si 15 tena kwa hiyo mimi bora....

Mhe. Mwenyekiti: Tumia hizo zilizopo baadae utakuja kumalizia kesho dakika 5.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu inabidi nizungumze haraka haraka kutokana na mambo niliyokuwa nayo. Lakini vile vile nimpe pole Waziri wa wizara hii wala simpongezi, nimpe pole. Hata hivyo amekuwa akijitahidi kwa hali na mali kuhangaikia michango bila ya kuitumia serikali. Amejitahidi sana Mhe. Waziri, hilo nikupongeze. Lakini foleni kubwa zaidi kuliko jitihada unazofanya.

Nichukuwe fursa hii nilikuwa nishataka kujilaumu hapa Mhe. Waziri wa Fedha simuoni. Lakini nashukuru Mhe. Waziri wa Fedha ameshafika. Mhe. Mwenyekiti, tunajadili maisha ya wapiga kura wetu, kunajadiliwa maisha ya wananchi wetu kila kiumbe hai anahitaji afya, hata wale ng'ombe waliokamatwa kule wanahitaji afya bila ya afya huwezi kufanya chochote.

Nichukuwe fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa ndani ya nafsi yangu Mhe. Dkt. Ali Mohd Shein na hii Ramadhani jinsi alivyojitahidi kwenye wizara hii. Alikuwa Naibu Waziri 1995 sijui kipindi hicho mpaka 2000, anaijua wizara hii. Amechukuwa jitihada kubwa sana likiwemo suala *ICU*, nilipiga kelele sana katika Baraza hili. Nikawaambia kuwa kule si *ICU* kule ni gereji, ukweli kauona Mhe. Rais. *ICU* iliyoko Mnazi Mmoja sasa hivi sijui kama ***Aga Khan*** kajenga lakini hata Tanzinia *ICU* bora iko huko Mnazi mmoja.

Nilipiga kelele suala la uzazi; watu kujifungua humu watu walikuwa wananiona sijui mwendawazimu au vipi, ni aibu. Mtu anachukuwa mimba miezi 9, hajui kama atapona au haponi akifika pale anaambiwa atoe shilingi elfu arubaini, wakabisha sana Mawaziri waliokuwemo humu ndani. Mtu anafika kuweka simu yake rehani pale hospitali apate vitu vya kujifungulia shilingi arubaini elfu. Wengine wanavua bangili zao za dhahabu, wengine TV zile ndogo ndogo wanaweka pale ili wapate pesa, wakawa wanabisha Mawaziri humu ndani. Naendelea kumshukuru tena Dkt. Ali Mohd Shein baada ya kuona ukweli kaweka bure jinsi anavyowajali wananchi wake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, bajeti kaiongeza amekuwa akijitahidi katika wizara hii. Lakini nisiwakatishe moyo madaktari itakuwa si vizuri, wamejitahidi kwa kiasi fulani madaktari wetu pamoja na misuko suko kidogo kidogo, wamejitadi lakini bado.

Mhe. Mwenyekiti tuanze kufungua katika vitabu nakuombeni Waheshimiwa mnisikilize kwa makini, mfungue kitabu hiki.

Kitabu H ukurasa wa 14 Waheshimiwa nakuombeni sana tusaidiane kitabu kikubwa hiki cha Bajeti humu ndio yamo mambo.

Mhe. Waziri Bajeti yako ni ndogo tena hairidhishi na ikiwa tunafanya mas-hara ya maisha yetu Bajeti zote za wizara kweli lakini hii serikali lazima ijivute ikitaka isitake, wenzetu Wabunge Uganda walikacha wakatoka nje. Wizara zote tufanye masihara lakini hapa si pahali pa kufanya masihara.

Serikali ijikubalishe, kwa hili hatuwezi kuweka rehani maisha yetu na wananchi wetu. Hii haielekei makadirio ya kawaida bililioni kumi na saba laki tatu; mishahara bilioni kumi na moja, ruzuku 1.4, ndio serikali hapa tunafanya nini. Serikali haijawa tayari kuwatumikia kiafya wananchi wake ndio ukweli ulivyo, wala tusibishane ushahidi huu hapa si maneno yangu.

Mhe. Waziri kamata kifungu uzuri hiki bajeti ni ndogo hapa pesa zilizoko ni za mishahara tu na *OC*, Maendeleo yako wapi?

Mhe. Mwenyekiti, isije kufika nikataka kuja kulia usije kushangaa humu ndani, *wallah* usije kushangaa.

(Hapa Mheshimiwa Jaku alilia kwa huzuni)

Mhe. Mwenyekiti, hii ni dhambi kubwa mno tunaweka rehani maisha yetu. Mhe. Mwenyekiti, leo tunaipanga Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ya rufaa bilioni 7.5 wakati vipimo havipo, tunafanya nini sisi kweli humu ndani. Kipimo hakipo hiyo *CT-Scan* utafikiri mvua za masika hata mwaka baada ya bajeti ndio inafanyakazi saa hizi. Tunafanya nini sisi hapa! Kweli hii serikali ipo kutumikia wananchi, sisi tukija kuwasemea Mawaziri kule tunaambiwa siasa. Siasa iko wapi hapa, hawa ni wapiga kura wetu. Sisi tuna jukumu kwa Mwenyezi Mungu, kupitisha bajeti hii ni dhima, tunaenda kuulizwa vyeo vyetu hii.

Leo bilioni saba Mhe. Waziri fungu hili, mpango wenu wa kufanya Hospitali ya Rufaa hii haupiti hapa Wajumbe nisaidieni hili, bilioni 7.5 kufanya Hospitali ya Rifaa wakati vipimo havipo, Hospitali ya Rufaa, macho hayapo ukapime Mikunguni hili haliwezekani. Kanuni hazikatazi kupitisha bajeti, hili fungu tunalitoa Wajumbe mnifahamu, angalieni kifungu PH 102, SH 010201 pesa yake ni 7.5 kufanya Rufaa iangalieni Waheshimiwa tusije tukakubali.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nikulaumu sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, nakulaumu sana, nikusifu na nikulaumu hii mnakuja kutuletea humu kwani sisi

tumelewa humu ndani. Hii mnata ku- *upgrade* wakati vitu vingine havipatikani mta- *upgrade* vipi hii hospitali vipimo havipo, dawa hamna. Leo chanjo ya mtoto hatari kubwa "*inna lillah waina illah rajiun"*. Chanjo ya mtoto haipatikani halafu tunataka ku-*upgrade*.

Fungu hili serikali kakaeni mliondoe hatujafika kufanyisha Hopsitali ya Rufaa "mbuzi anakula majani kutokana na urefu wa kamba yake". Mimi nitataka mchanganuo Mhe. Waziri wa Afya. Mheshimiwa nisikilize Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe zungumza na kiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayob: Hasikiliza sasa atakuja kujibu hoja itakuwa kama wale kina Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Simai Mohammed Said hoja tatu tunasokotwa tu na kanuni haziruhusu. Ukurasa wa 18 nataka mchanganuo wa hizi pesa bilioni 54.7. Huduma za utunzaji na usambazaji.

Leo Pemba sawa zimapelekwa kwa vihuri kweli ndio mahitaji halisi ya bilioni hamsini na nane hizi hapa basi angalau bilioni mia moja na hamsini. Nilikuwa Mjumbe wa Kamati mimi hiki kifungu kwa kweli kina mtihani, hatuwezi kwenda Mheshimiwa mambo ya ajabu ajabu, tunafanyiwa humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nije nimuombe Mhe. Rais ikiwa tumefika kununua meli ya bilioni ngapi, mashine ya *X-ray* ni aibu mno, dhambi kubwa iliyoje. Hiyo *Mobile X-ray* aliyoisema Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, uwezo wake ni kupiga *X-ray* 20 tu inalazimisha mpaka 80. Mie nilikuwepo jana jioni magharibi tumekutana huyu bwana mkubwa Waziri *Mental* akamata kichwa , ile *X ray Mobile* kuna vipimo huwezi kupata, cha paja huwezi kupiga, cha mgongo hakipatikani, cha kichwa hakipatikani mnataka kuifanya ile Hospitali ya Rufaa, ile msitufanyie hivyo.

Hili halipiti, Wajumbe nakuombeni kwa hili na tutakwenda kuulizwa. Hizi bilioni 7.5 zende kwenye madawa na
X-ray machine. (*Makofi*)

Mwaka jana nilizungumza ndani mie *hansard* zipo, hii ni dharau tunayofanyiana. Kweli serikali pana jenereta, halipo tumekuja hapa *X-ray machine*, na *oxygen* haipo, dawa za chanjo hazipo, pesa hizi Mhe. Waziri wa Afya kwa heshima na taadhima zihamishe hatujafikia Hospitali ya Rufaa Wajumbe tufahamiane suala hili, tusije kupitisha jambo ambalo ni dhambi tupu. Vipimo havipo, pesa hizi ziende kwenye dawa na *X-ray machine*.

Mhe. Mwenyekiti, chanjo, tunafanya nini hicho kipimo cha uzazi, kujifungua bado mtu anachangia mpaka leo ukanunue *drip*, ukanunue hutoki kama hujapeleka chupa ya Jik pamoja na Mhe. Rais kutangaza kama kujifungua bure, hili haliwezekani.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe muda hauturuhusu tena utakuwa unadai dakika zako 5 kesho asubuhi utamalizia tukijaaliwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwataje wale watakaochangia kesho asubuhi baada ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atakuwa ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman na Mhe. Suleiman Sarahan, kwa wakati huo wa asubuhi tukijaaliwa.

Baada ya hapo naomba niwashukuru sana kwa michango yenu na kwa utulivu wenu. Naomba niliakhirishe Baraza hadi kesho mnamo saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 8.58 Mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 21/06/2016 Saa 3.00 asubuhi)